
# Kiswahili

## Kitabu cha Mwanafunzi

## Darasa la Sita




Taasisi ya Elimu Tanzania

*Mali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hakiuzwi*

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Kiswahili

## Kitabu cha Mwanafunzi

## Darasa la Sita



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 223

Jina la Chapisho: Kiswahili Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Sita

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Taasisi ya Elimu Tanzania

ISBN: 978-9987-09-049-5

Kitabu hiki kimeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 22 Septemba, 2019 kuwa Kitabu cha Kiada kwa ajili ya Mwanafunzi wa Darasa la Sita katika ngazi ya elimu ya Msingi nchini Tanzania kulingana na Muhtasari wa Mwaka 2016.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kaimu Kamishna wa Elimu.

### Taasisi ya Elimu Tanzania

FOR ONLINE USE ONLY

KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 1 26/07/2021 16:25

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

© Taasisi ya Elimu Tanzania, 2019

Toleo la Kwanza 2019

Chapa ya Pili 2021

ISBN: 978-9987-09-049-5

Taasisi ya Elimu Tanzania

S.L.P. 35094

Dar es Salaam - Tanzania

Simu: +255 735 041 170 /+255 735 041 168

Baruapepe: director.general@tie.go.tz

Tovuti: www.tie.go.tz

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kukitoa kitabu hiki kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 2 26/07/2021 16:25

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Yaliyomo

Ukurasa

**Utangulizi**.....v

**Shukurani**.....vi

**Sura ya Kwanza**
Kuimba wimbo wa kizalendo.....1

**Sura ya Pili**
Shairi.....10

**Sura yaTatu**
Igizo la elimu ya biashara.....21

**Sura ya Nne**
Hadithi.....28

**Sura ya Tano**
Taswira za nahau.....39

**Sura ya Sita**
Ziara.....46

**Sura ya Saba**
Mawasiliano ya simu.....55

**Sura ya Nane**
Aina za maneno.....66

**Sura ya Tisa**
Risala.....75

**Sura ya Kumi**
Kutumia kamusi.....84

**Sura ya Kumi na Moja**
Matangazo ya biashara.....93

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 3 26/07/2021 16:25

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Sura ya Kumi na Mbili**
Uundaji wa maneno....102

**Sura ya Kumi na Tatu**
Ufupisho....107

**Sura ya Kumi na Nne**
Kumbukumbu za mikutano....116

**Sura ya Kumi na Tano**
Umiliki katika lugha....128

**Sura ya Kumi na Sita**
Kuandika habari....136

**Sura ya Kumi na Saba**
Shairi la mabadiliko ya hali ya hewa....145

**Sura ya Kumi na Nane**
Kusikiliza habari ya madhara ya rushwa....154

**Sura ya Kumi na Tisa**
Kubaini hoja katika majadiliano....165

**Sura ya Ishirini**
Kusoma kwa ufasaha....172

**Sura ya Ishirini na Moja**
Kusoma kwa burudani....179

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 4 26/07/2021 16:25

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Utangulizi

Kitabu hiki ni cha nne katika mfululizo wa vitabu vya Kiswahili kilichoandaliwa mahususi kwa ajili ya mwanafunzi wa Darasa la Sita. Kitabu kinalenga kukuza uwezo wako wa kuzungumza, kusikiliza, kusoma na kuandika kwa lugha ya Kiswahili. Pia, kitabu kimelenga kukuwezesha kutumia msamiati wa lugha ya Kiswahili kwa namna mbalimbali, hivyo, kukujengea uwezo wa kupanga mawazo kwa mpangilio na mtiririko unaotakiwa.

Kitabu kina hadithi, habari, mashairi, ngonjera, igizo, mdahalo na majigambo. Vyote hivyo vitakuwezesha kujifunza kwa ufasaha. Kitabu kimesheheni maswali ya kupima ufahamu na mazoezi mbalimbali yanayojenga ujuzi wako katika somo la Kiswahili.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 5 26/07/2021 16:25

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Shukurani

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini mchango muhimu wa waliofanikisha uandishi wa kitabu hiki cha mwanafunzi.

TET inatoa shukurani za dhati kwa mchango uliotolewa na wataalamu wafuatao walioshiriki kutayarisha kitabu hiki:

**Waandishi:** Mwl. Rose S. Chipindula, Mwl. Melina A. Yohana, Mwl. Samwel M. Magutu, Mwl. Tumaini M. Mahendeka na Mwl. Adelgot J. B. Mapunda

**Wahariri:** Prof. David P. B. Massamba, Dkt. Faraja J. Mwendamseke (Mwenyekiti wa jopo la uhariri wa maudhui) na Bw. Mussa R. Kaoneka (Lugha - BAKITA)

**Msanifu:** Bw. Kuyonza K. Kuyonza

**Wachoraji:** Bw. Fikiri A. Msimbe na Alama Art and Media Production Limited

**Mratibu:** Mwl. Rose S. Chipindula

Pia, TET inatoa shukurani kwa walimu wote walioshiriki katika ujaribishaji wa kitabu hiki. Vilevile, TET inatoa shukurani za pekee kwa shirika la "Global Partnership for Education (GPE)" kupitia mradi wa Kukuza Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) uitwao "Literacy and Numeracy Education Support (LANES II)" kwa ufadhili wao uliofanikisha kazi ya kuchapisha kitabu hiki.

Aidha, TET inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kutoa rasilimali fedha iliyofanikisha uandishi wa kitabu hiki.



Dkt. Aneth A. Komba
Mkurugenzi Mkuu
Taasisi ya Elimu Tanzania

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 6 26/07/2021 16:25

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kwanza

## Kuimba wimbo wa kizalendo

### Utangulizi

*Katika sura hii, utaimba wimbo wa Tanzania Tanzania na kughani shairi linalohusu uzalendo. Pia, utajifunza mambo mbalimbali ikiwemo sifa za nchi ya Tanzania, Watanzania na mashujaa wa Tanzania.*

### Fikiri



1. Kwa nini ni vizuri kuipenda nchi yako?
2. Kuna faida gani ya kuilinda nchi yako?
3. Mambo gani yanakufanya uipende nchi yako?

### Ufahamu

*Soma, imba wimbo na shairi lifuatalo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

### Wimbo wa Tanzania Tanzania

*1. Tanzania Tanzania,*
*Nakupenda kwa moyo wote,*
*Nchi yangu Tanzania,*
*Jina lako ni tamu sana,*
*Nilalapo nakuota wewe,*
*Niamkapo ni heri mama wee,*
*Tanzania Tanzania,*
*Nakupenda kwa moyo wote.*

*2. Tanzania Tanzania,*
*Ninapokwenda safarini,*
*Kutazama maajabu biashara nayo makazi,*
*Sitaweza kusahau mimi,*
*Mambo mema ya kwetu kabisa,*
*Tanzania Tanzania,*
*Nakupenda kwa moyo wote.*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. *Tanzania Tanzania,*
   *Watu wako ni wema sana,*
   *Nchi nyingi zakuota,*
   *Nuru yako hakuna tena,*
   *Na wageni wakukimbilia,*
   *Ngome yako imara kweli wee,*
   *Tanzania Tanzania,*
   *Heri yako kwa mataifa.*

4. *Tanzania Tanzania,*
   *Karibu wasio na kwao,*
   *Wenye shida na taabu,*
   *Kukimbizwa na walowezi,*
   *Tanzania yawakaribisha,*
   *Mpigane kiume chema wee,*
   *Tanzania Tanzania,*
   *Mola awe nawe daima.*

FOR ONLINE USE ONLY

### Shairi la Tanzania yangu

1. Sauti yangu napaza, namuomba Rahamani,
   Nianze kuzungumza, sikizeni kwa makini,
   Haya niliyoyawaza, humu mwangu akilini,
   Naisifu nchi yangu, kwa **nudhumu** maarufu.

2. Kwa nudhumu maarufu, na vina kupangilia,
   Mizani kama mkufu, beti kuzishikilia,
   Na mishororo mirefu, mantiki kupangilia,
   Karibu utiririke, malenga nikupeleke.

3. Nchi yangu ya thamani, mimi kweli naipenda,
   Wale wasoithamini, naona wafanya **inda**,
   Hata sijui kwa nini, kwa nchi yao wakonda,
   Hakika tuithamini, kwa moyo mweupe kwatu.



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 2 26/07/2021 16:25

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

4. Nchi ninayoipenda, popote ulimwenguni,
Kila utakapokwenda, nchi yetu ina shani,
Kila mtu anapenda, nchi yetu ya thamani,
Kwa kweli usipopenda, nakuona **hayawani**.

5. Nakuona hayawani, mimi ninakuhesabu,
Unachofanya ni nini, na wala huoni tabu,
Hata ng'ambo hupaoni, umekuwa kama dubu,
Nchi ya kujivunia, wala sioni aibu.

6. Wala siioni soni, nchi yangu kuisifu,
Hebu chunguza amani, hakika ni utukufu,
Hata uvue miwani, utauona mkufu,
Nchi hii burudani, imenikuna mtima.

7. Mtima imenikuna, kwa **dafina** teletele,
Samaki wa kumimina, changu, sato, kolekole,
Ziwa la kirefu kina, kina kirefu milele,
Thamani ya nchi yangu, hai**mithili**ki kamwe.

8. Kamwe haimithiliki, ukitazama bahari,
Bandari hazipimiki, mimi naona fahari,
Uvuvi haushikiki, pwani yote i tayari,
Nani bado haelewi? Ajikune nimuone.

9. Ajikune nimuone, aone ule mlima,
Kwanza Mawenzi aone, kilele kimesimama,
Kisha Kibo apaone, theluji isiyohama,
Kuipenda nchi yangu, hakika ni maridadi.

10. Ni maridadi hakika, wala sioni hiyana,
Unguja inashikika, historia bayana,
Pemba nayo kwa hakika, marashi yake mwanana,
Nchi yangu maridadi, sichoki kujivunia.

11. Sichoki kujivunia, wanyama wa kupendeza,
Mikumi najivunia, Serengeti yapendeza,
Wanyama wang'ang'ania, mbugani wajipenyeza,
Nani bado ana swali? Mwambieni aulize.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 3 26/07/2021 16:25

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

12. Aulize mwambieni, nimpeleke Ruaha,
Au Mikumi twendeni, akaipate furaha,
Hata Gombe mwambieni, twendeni aonje raha,
Nchi yangu kusifia, mimi naona fahari.

13. Fahari bado naona, kuzungumzia mito,
Malagarasi mwaona, Rufiji siyo kijito,
Ruvu, Kagera mwanana, Pangani pia ni mito,
Hakika siwezi choka, mimi ninajivunia.

14. Nchi ninajivunia, ni haki na ni wajibu,
Vito vya kujivunia, almasi na dhahabu,
Tanzanaiti sikia, rubi na gesi nasibu,
Asiyejua ni nani, tumwoneshe mashujaa.

15. Mashujaa wa uhuru, Nyerere naye Karume,
Wengine walio huru, Mwinyi na tena Karume,
Mkapa, Jakaya nuru, She'ni, Pombe wanaume,
Amani wameitunza, viongozi wetu safi.

16. Viongozi walitamba, sera wakazianzisha,
Ujamaa ukapamba, azimio likatisha,
Utandawazi twaomba, kasi mpya nakumbusha,
Ikafata hapa kazi, matokeo yote chanya.

17. Matokeo yote chanya, mijini na vijijini,
Umeme ninawatonya, hadi huko vijijini,
Barabara nawakanya, msilime kwa mipini,
Nani ambaye haoni, ujenzi wa reli mpya?

18. Ujenzi mpya wa reli, na wa anga usafiri,
Watalii mbalimbali, salama wataabiri,
Hakuna tena pa mbali, wala ya mbali safari,
Nchi inasonga mbele, vijijini na mijini.

19. Mijini na vijijini, elimu bila malipo,
Afya hata vijijini, zahanati sasa zipo,
Tunaona na mijini, madaraja sasa yapo,
Tazama fahari yangu, kuitwa Mtanzania.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

20. Kuitwa Mtanzania, fahari yangu na yako,
Utaifa ndiyo nia, umoja ndiyo mashiko,
Nchi nitapigania, vurugu kwetu ni mwiko,
Yapo mengi ya msingi, siwezi kuyamaliza.

21. Siwezi kuyamaliza, hadi yale ya kilimo,
Ardhi yajitambaza, rutuba isokikomo,
Hata mvua ya ku**saza**, tena bila ya kikomo,
Niishilie kunena, **kaditama** nifichame.

22. Kaditama na**fichama**, sala nampa Rabana,
Tuepushie nakama, madhila kwetu hapana,
Fanaka kwetu **adhama**, nakuomba Maulana,
Kwa **fuadi** natuama, amani utujalie.

## Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Taja ujumbe katika wimbo wa Tanzania Tanzania.
2. Shairi hili linahusu nini?
3. Taja mashujaa waliotajwa katika shairi.
4. Taja sifa za Tanzania zilizoandikwa katika shairi.
5. Taja vilele viwili vya Mlima Kilimanjaro vilivyotajwa na mshairi.
6. Kwa nini unasisitizwa kuipenda nchi yako?
7. Orodhesha shughuli za kiuchumi zilizotajwa katika shairi.
8. Mshairi anaposema “marashi yake mwanana” anamaanisha nini?
9. Mwandishi anaposema “nchi najivunia” anamaanisha nini?
10. Kama wewe ungekuwa mwandishi wa shairi hili ungeongeza sifa gani za nchi yako?
11. Umejifunza nini kutokana na shairi ulilolisoma?

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 5 26/07/2021 16:25

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la pili: Msamiati

**Oanisha maneno ya sehemu A na maana zake katika sehemu B.**

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| (i) nudhumu | (a) mwisho au kikomo cha jambo |
| (ii) inda | (b) tabia ya mtu kutopenda mafanikio ya mtu mwingine |
| (iii) hayawani | (c) mfano wa |
| (iv) dafina | (d) utungo wa kishairi |
| (v) mithili | (e) moyo |
| (vi) saza | (f) jambo kubwa la heshima na fahari |
| (vii) kaditama | (g) mtu asiye na ubinadamu |
| (viii) fichama | (h) mali iliyofukiwa chini ya ardhi kwa lengo la kufichwa |
| (ix) adhama | (i) bakiza sehemu ya kitu unachotumia au unachokichukua |
| (x) fuadi | (j) jificha kwa kujibanza ili kutoonekana na watu kwa urahisi |

## Zoezi la 3: Methali

**Kamilisha methali zifuatazo:**

**Mfano:** Mfukuzwa kwao, ……………….

Mfukuzwa kwao, hana pa kwenda.

1. Manahodha wengi, ………………….
2. ………………., hutumbua usaha.
3. Kutoa ni moyo, ………..
4. …………., hakuna wajenzi.
5. Ada ya mja hunena, …………
6. …………………, vya kuchinja haviwezi.
7. Achezaye na tope, ………………
8. ………………, haangukiwi na mti.
9. Amani haiji, …………………
10. ……………….., akichoka keshapata.



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 6 26/07/2021 16:25

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 4: Vitendawili

### Tegua vitendawili vifuatavyo:

1. Gari langu halitumii mafuta. ____________
2. Shamba langu kubwa lina kisiki kimoja. __________
3. Saa yangu haijasimama tangu itiwe ufunguo. _____________
4. Wanangu hawapandi mlima bali huteremka daima. __________
5. Garimoshi relini. ____________
6. Mavuno ya shamba zima hayajazi kiganja. ____________
7. Mazishi yake ni furaha kwa watu. ___________
8. Chungu cha mwitu hakiwapiki wapishi wake wakaiva. ____________
9. Kwa mfalme, hawa wanatoka hawa wanaingia. ____________
10. Nacheza ngoma lakini wapigaji wake wako ughaibuni. _________

## Zoezi la 5: Mazoezi ya lugha

### A. Andika maneno yenye maana sawa na maneno yafuatayo:

**Mfano:** mnadi - *dalali*
karaha - *kero*

(i) fuadi ______________
(ii) kaditama ______________
(iii) jibanza ______________
(iv) bakiza ______________
(v) onya ______________
(vi) husuda ______________
(vii) shujaa ______________
(viii) mshororo ______________
(ix) kera ______________
(x) nakama ______________

### B. Pigia mstari neno lililo tofauti.

(i) mpasuko, mshikamano, ushirikiano, umoja
(ii) figo, mtima, fuadi, moyo
(iii) kazi, saza, shughuli, wajibu
(iv) mzalendo, mzaha, mwenyeji, mzawa
(v) kodi, rushwa, ushuru, ada
(vi) kubali, shawishi, bembeleza, hamasisha
(vii) dhahabu, lulu, udongo, almasi
(viii) tiririka, miminika, mwagika, zoleka

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 7 26/07/2021 16:25

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(ix) tamka, sema, nyamaza, zungumza, ongea
(x) bashiri, patia, kisia, tabiri
(xi) paramia, pindua, dandia, panda

## C. Andika neno sahihi badala ya maneno yaliyokolezwa.

**Mfano:** Mayai yote **amevunjika**.
Mayai yote **yamevunjika**.

(i) Tuliimba **nyimbo ya** kuisifu nchi yetu.
(ii) Mwanafunzi **yoyote** aje mbele.
(iii) Tunatakiwa kuthamini **feza** kwa kuzitunza.
(iv) Rushwa ni **hadui** wa haki.
(v) Tanzania ni nchi ya **hamani**.
(vi) Mimi naipenda **inchi** yangu.
(vii) **Tunathoma** vitabu ili kupata maarifa.
(viii) **Luaha** ni mto uliotajwa katika **shaili**.
(ix) **Luga** ya Taifa la Tanzania ni **Kiswaili**.
(x) **Mwarimu** wetu anafundisha **visuli**.

## D. Jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kutumia maneno yaliyo katika kisanduku.

| |
|---|
| mzalendo, kaulimbiu, kibwagizo, rasilimali, rambirambi, mtiifu, kusoma, samani, bustani, misitu. |

(i) Fedha au kitu anachopewa mtu kama pole anapofiwa, huitwa_____________
(ii) Mtu anayeipenda nchi yake na kuitumikia kwa moyo na uadilifu, huitwa _______________
(iii) __________ za viongozi mbalimbali hulenga katika kuhamasisha watu kufanya kazi kwa bidii.
(iv) Wananchi wasingalichoma_________, kusingalikuwa na ukame.
(v) Shule yetu ina ___________ nzuri ya maua.
(vi) _____________ni maneno yanayojirudia katika wimbo au shairi.
(vii) Tunatakiwa kutunza ______________ za nchi yetu kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vya baadaye.
(viii) _____________kwa bidii ni mbinu ya kufaulu mitihani.
(ix) Ofisi ya Mwalimu Mkuu ina __________ za aina mbalimbali.
(x) Kalumekenge angelikuwa ________, asingelifukuzwa shule.



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 8 26/07/2021 16:25

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**E. Andika NDIYO au HAPANA katika sentensi zifuatazo:**

(i) Mzalendo ni mtu anayependa nchi ya wenzake. __________
(ii) Kiburi si maungwana. __________
(iii) Kuwa macho maana yake ni kuamka mapema. __________
(iv) Mwanafunzi kuwahi shule si jambo la muhimu. __________
(v) Mtoto mwenye adabu ni yule anayekaidi maagizo ya ndugu zake. __________
(vi) Familia ni baba, mama na watoto. __________
(vii) Shule zote zinapaswa kuwa na walimu wa kutosha. __________
(viii) Barua ya kikazi ina anuani moja. __________
(ix) Shairi huandikwa kwa lugha ya mkato. __________
(x) Maneno huundwa na silabi. __________

**F. Jibu maswali yafuatayo:**

(i) Bendera ya taifa letu ina rangi ngapi? Zitaje.
(ii) Kwa nini kila mtu anapaswa kuipenda nchi yake?
(iii) Tunapaswa kufanya nini kuhusu rasilimali za nchi yetu?
(iv) Nani ana jukumu la kuilinda nchi yetu?
(v) Mtu asiye na uzalendo kwa nchi yake anaitwaje?

**G. Badili sentensi zifuatazo kuwa katika wingi.**

(i) Tamka neno hili kwa ufasaha.
(ii) Ghani shairi hili kwa mbwembwe.
(iii) Wimbo huu unaitukuza nchi yetu.
(iv) Alama hii ya uandishi ni ya muhimu sana katika uandishi.
(v) Sentensi hii ipo katika wakati uliopo.
(vi) Mwanafunzi lazima afuate ratiba ya shule.
(vii) Sare ya shule yetu ni shati la rangi nyeupe.
(viii) Kisima changu kimejaa maji tele.
(ix) Paka shume amemkamata kuku wangu.
(x) Mimi na ndugu yangu ni wazawa wa nchi hii.

## Zoezi la 6: Utungaji

**Tunga habari yenye maneno yasiyozidi mia moja (100) inayohusu kiongozi wako wa darasa.**

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 9 26/07/2021 16:25

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Pili

## Shairi

### Utangulizi

*Katika sura hii, utajifunza kughani shairi na kubaini mawazo makuu yanayopatikana katika shairi. Pia, utajifunza kutunga shairi la kimapokeo kwa kuzingatia kanuni zake. Utafafanua maana za taswira zilizomo katika shairi na kuzihusianisha na maisha ya kila siku. Hii itakusaidia kuwa mtunzi mahiri wa mashairi na nyimbo mbalimbali.*

### Fikiri



1. Shairi ni nini?
2. Je, nani kati yenu anapenda kughani shairi? Kwa nini?

### Ufahamu

*Soma na ghani shairi lifuatalo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

1. Elimu kwa mwanadamu, ndiyo silaha imara,
   Imekuwepo **dawamu**, hata kwa wale **sonara**,
   Tajua wake utamu, ukipitishwa kwa sura,
   *Usilikose darasa, kwa kufuata **mkumbo**.*

2. Nakupatia **nudhumu**, taona nayo **tijara**,
   Ujifunze na elimu, ya kuucheza mpira,
   Uinoe yako timu, kisha kuanza ziara,
   *Usilikose darasa, kwa kufuata mkumbo.*

3. Na **ving'ora** vya kudumu, adui kuteka nyara,
   Kwa yote yalo magumu, ni shime kuyazingira,
   Kukazania elimu, kuuzika u**fukara**,
   *Usilikose darasa, kwa kufuata mkumbo.*

4. Kusoma kunawakimu, vijana kuwa imara,
   Kupambana na magumu, kwenye uwanja wa **dura**,
   Watu kushika **hatamu**, huwa na nyingi fikira,
   *Usilikose darasa, kwa kufuata mkumbo.*

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 10 26/07/2021 16:25

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

5. Rafiki yangu Adamu, kwepa ya ujinga **nira,**
Usijekosa fahamu, kupata ari na **ghera**,
Mkumbo ni kama sumu, utakukosesha dira,
*Usilikose darasa, kwa kufuata mkumbo.*

6. Liyotukuka elimu, hufunza na biashara,
Yafaa kuwa timamu, kujipatia **ajira**,
Maisha hana karimu, ukikosea ubora,
*Usilikose darasa, kwa kufuata mkumbo.*

7. Sheria ni msumeno, hukata huko na huku,
Elimu nayo ni meno, pia ni kama sumaku,
Yaweza leta unono, mithili ngoma **chiriku**,
*Usilikose darasa, kwa kufuata mkumbo.*

8. Aliye moyo mgumu, hatima katia fora,
Kaitunga na hukumu, ya kuhimiza fikira,
Kaupata ufahamu, wa ku**ng'amua** taswira,
*Usilikose darasa, kwa kufuata mkumbo.*

9. Ukiwepo darasani, mwalimu msikilize,
Kisichotiwa **mizani**, angalia usimeze,
Kilopita kipimoni, ndicho ukitekeleze,
*Usilikose darasa, kwa kufuata mkumbo.*

10. Mazoezi darasani, yatakufanya uweze,
La kufanya akilini, kuchagua ipendeze,
Ujuzio ubaini, jamii usipumbaze,
*Usilikose darasa, kwa kufuata mkumbo.*

11. Utakuwa hatiani, masomo kuyapuuza,
Kuishi kama **kunguni**, hakika inaumiza,
Bora uishi porini, na majini kama pweza,
*Usilikose darasa, kwa kufuata mkumbo.*

12. Kwa walimu na wazazi, nidhamu uidumishe,
Na mambo yalo **azizi**, pekee jishughulishe,
Tabia ya uchokozi, kamwe usijifundishe,
*Usilikose darasa, kwa kufuata mkumbo.*

13. Tabia mbaya ya wizi, elimu iikomeshe,
Madhara ya udokozi, jamii uifundishe,
Mwenendo kama wa mbuzi, daima ujiepushe,
*Usilikose darasa, kwa kufuata mkumbo.*

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 11 26/07/2021 16:25

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

14. Fanikiwa hatimaye, ni mfano maishani,
Tegemea cha nduguye, hufa hali masikini,
Mwanafunzi asomaye, apaswa awe kifani,
*Usilikose darasa, kwa kufuata mkumbo.*

15. Kijana naku**usia**, usiachie na hisa,
Masomo kung'ang'ania, nakupatia **hamasa**,
Ndani ya historia, jinalo lipate nasa,
*Usilikose darasa, kwa kufuata mkumbo.*

16. Ya viwandani elimu, lazima uzingatie,
Wanafunzi wahitimu, ujuzi washikilie,
Wa viwanda ufahamu, hakika wakumbatie,
*Usilikose darasa, kwa kufuata mkumbo.*

17. Naweka chini kalamu, tamati nimefikia,
Labaki lako jukumu, nasaha ku**charukia**,
Usiache ufahamu, sukari kukimbilia,
*Usilikose darasa, kwa kufuata mkumbo.*

## Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Shairi hili lina jumla ya beti ngapi?
2. Taja vina vya mwisho katika ubeti wa nne.
3. Taja vina vya kati na vya mwisho katika ubeti wa kumi na nne.
4. Kila ubeti wa shairi hili una mishororo mingapi?
5. Mstari unaojirudiarudia katika kila ubeti unaitwaje?
6. Taja mambo matatu yanayozungumziwa katika shairi hili.
7. Mshairi anaposema katika ubeti wa tisa kuwa "Kisichotiwa mizani, angalia usimeze" anamaanisha nini?
8. Taja mambo mawili katika ubeti wa kumi na tatu ambayo hayafai kuigwa na jamii.
9. Taja faida tatu za kuwapo kwa viwanda nchini.
10. Pendekeza kichwa cha shairi hili.

## Zoezi la pili: Msamiati

**Tunga sentensi moja kwa kila neno.**

**Mfano:** ajira

*Elimu bora huongeza ajira kwa vijana.*

*Watu hupata vipato vyao kutokana na ajira mbalimbali.*

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 12 26/07/2021 16:25

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. dawamu | 6. ving'ora | 11. ghera | 16. kunguni |
| 2. sonara | 7. fukara | 12. ajira | 17. azizi |
| 3. mkumbo | 8. dura | 13. chiriku | 18. usia |
| 4. nudhumu | 9. hatamu | 14. ng'amua | 19. hamasa |
| 5. tijara | 10. nira | 15. mizani | 20. charukia |

## Zoezi la 3: Methali

### Kamilisha methali zifuatazo:

(i) Mtegemea cha nduguye, ………………………
(ii) ………………………, huonekana asubuhi.
(iii) ………………………., katika tumbo la heri.
(iv) Sheria ni msumeno, ………………………
(v) ………………………, hawiki penye jogoo.
(vi) Elimu bila adili, ………………………
(vii) Udugu wa nazi, ………………………
(viii) Nguvu ya mamba, ………………………
(ix) ………………………, si mwisho wa uhunzi.
(x) ………………………, hukosa yote.

## Zoezi la 4: Mazoezi ya lugha

### A. Pigia mstari neno lenye maana tofauti na mengine.

**Mfano:** maarifa, elimu, lami, ujuzi
(i) shairi, utendi, hadithi, ngonjera
(ii) kunde, njegere, maharage, mahindi
(iii) kengele, king'ora, tarumbeta, mlio
(iv) gazeti, sheria, kanuni, katiba
(v) vina, silabi, mizani, aya
(vi) gilasi, bilauri, kikombe, sahani
(vii) sangara, kamongo, pweza, chiriku
(viii) ujangili, wizi, ulevi, ujambazi
(ix) kunguni, panzi, nzige, senene

### B. Chagua jibu sahihi katika maswali haya.

(i) Mtu anayetunga mashairi anaitwa ___________.

(a) mghani
(b) mhunzi



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(c) mshairi
(d) mwandishi

(ii) Shairi huweza kuimbwa au ___________.

(a) kughaniwa
(b) kuchezwa
(c) kutambwa
(d) kutegwa

(iii) Kituo ni mstari wa ___________unaojirudiarudia katika kila ubeti wa shairi.

(a) kwanza
(b) pili
(c) kati
(d) mwisho

(iv) Katika shairi la kimapokeo ___________vya kati na vya mwisho katika ubeti hufanana.

(a) beti
(b) vina
(c) mizani
(d) silabi

(v) Idadi ya silabi katika mshororo huitwa ___________.

(a) mizani
(b) kituo
(c) vina
(d) herufi

(vi) Kila ubeti wa shairi lazima ubebe angalau wazo ___________. muhimu.

(a) tata
(b) shinikizi
(c) moja
(d) kinzani

(vii) Ubeti wa shairi wenye mistari minne huitwa ___________.

(a) kibwagizo
(b) kituo
(c) mshororo
(d) tarbia

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 14 26/07/2021 16:25

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(viii) Mstari katika ubeti wa shairi unaweza pia kuitwa ___________.

(a) nudhumu
(b) mshororo
(c) mizani
(d) kituo

(ix) Nini maana ya kughani shairi?

(a) kusoma shairi
(b) kuimba shairi
(c) kuelezea shairi
(d) kuandika shairi

(x) Utungo wa kifasihi unaotumia lugha ya mkato kuwasilisha ujumbe kwa hadhira huitwa ___________.

(a) insha
(b) sanaa
(c) fasihi
(d) shairi

## C. Eleza maana ya taswira zilizotumika katika shairi ulilosoma.

(i) ukipitishwa kwa sura
(ii) mpira
(iii) uwanja wa dura
(iv) nira
(v) meno
(vi) mizani
(vii) kunguni
(viii) udokozi
(ix) mbuzi
(x) msumeno

## D. Tunga sentensi kumi (10) kwa kutumia jedwali lifuatalo:

**Mfano:** *Juma aliweza kuwahi ingawa alikuwa mgonjwa.*
*Joshua alitembea kwa miguu ijapokuwa mvua ilinyesha.*

| | | |
|---|---|---|
| Mtoto alimudu kutembea<br>Juma aliweza kuwahi<br>Joshua alitembea kwa miguu | ingawa<br>ijapokuwa | hakuwa na viatu<br>mvua ilinyesha<br>alikuwa mgonjwa |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**E. Andika wingi wa maneno yafuatayo:**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| (i) mbuzi | __________ |
| (ii) shairi | __________ |
| (iii) elimu | __________ |
| (iv) msumeno | __________ |
| (v) mwezi | __________ |
| (vi) ubeti | __________ |
| (vii) nchi | __________ |
| (viii) sonara | __________ |
| (ix) king'ora | __________ |
| (x) nira | __________ |

**F. Kanusha sentensi zifuatazo:**

**Mfano:** Pili anakula chungwa.

*Pili hali chungwa.*

(i) Shairi linaigizwa.
(ii) Nikiwa mkubwa nitakuwa mcheza masumbwi.
(iii) Baba ana kiwanda cha sabuni.
(iv) Shairi ni lazima liwe na beti kumi.
(v) Kiswahili ni lugha ya kigeni Tanzania.
(vi) Nimepata maswali yote.
(vii) Mwanafunzi anasoma kamusi ya Kiswahili.
(viii) Nyumbani kwetu ni mbali.
(ix) Eva anapalilia bustani ya babu yake.
(x) Mwandiko mzuri ni wa Chausiku tu.

**G. Panga herufi zilizochanganywa ili zilete neno sahihi.**

**Mfano:** luime - *elimu*
yinbom - *nyimbo*

(i) hanasa ____________
(ii) mitata ____________
(iii) kulama ____________
(iv) ruchaka ____________
(v) ngilu ____________
(vi) rasada ____________
(vii) ombukm ____________
(viii) windava ____________

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 16 26/07/2021 16:25

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(ix) katenijolo ____________

(x) sadidi ____________

## H. Tumia maneno uliyopewa kwa kila sentensi kujaza nafasi zilizoachwa wazi.

(i) Watoto _______chakula kitamu.
(wanapenda, watalia, wanaimba, walitenda)

(ii) Otaigo alipofika sokoni, __________ mjomba anauza viatu.
(atamkuta, hukuta, alimkuta, angemkuta)

(iii) Baba yake Eliza ___________ Akida.
(ataita, anaitwa, anaitika, ameitwa)

(iv) Kesho jioni __________ mtoni.
(nitakwenda, nilienda, nimekwenda, nimeenda)

(v) Leo mwalimu ____________ elimu kwa vitendo.
(himiza, alihimiza, huhimiza, anahimiza)

(vi) Mwasile atakapokuwa mkubwa, ___________ghorofa.
(anajenga, hujenga, atajenga, akijenga)

(vii) Kijana yule angalighani shairi, _____________ mtukutu.
(asingalikuwa, asingelikuwa, asingekuwa, angekuwa)

(viii) Mama ___________ sasa hivi kwenda dukani.
(aliondoka, alikwishaondoka, ameondoka, keshaondoka)

(ix) Kila siku _____________ shuleni kwa miguu.
(tulikwenda, tumekwenda, tunakwenda, tutakwenda)

(x) Jana ____________ kitabu kinachoelezea utii wa watoto kwa wazazi na walimu.
(nimesoma, nilisoma, nitasoma, anasoma)

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 17 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**I. Oanisha maelezo kutoka sehemu B na uyatumie kukamilisha sentensi katika maelezo ya sehemu A kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye nafasi zilizoachwa wazi.**

**Mfano:** Nitakapokuwa mkubwa d

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| (i) Hakubali kuonewa ________. | (a) ingawa alikuwa mgonjwa |
| (ii) Mtoto aliyepotea ________. | (b) huna budi kulighani |
| (iii) ________ hakuweza kuchuma pera. | (c) walikuwa na silaha |
| (iv) Askari waliokuwa lindoni ________. | (d) nitamjengea bibi nyumba nzuri |
| (v) Sote tulikula chakula ________. | (e) sihimili kishindo |
| (vi) Manamba angalimsikiliza baba yake ________. | (f) amepatikana leo |
| (vii) Nitakapokuwa mkubwa ________. | (g) utakapokuwa mkubwa |
| (viii) Baba alimudu kutembea ________. | (h) japokuwa ni mtoto |
| (ix) Ukilitunga shairi ________. | (i) isipokuwa mjomba |
| (x) Mimi nyumba ya udongo ________. | (j) anakula wali |
| (xi) John ________ kwa mikono. | (k) pamoja na urefu wake |
| (xii) Utayajua maisha ________. | (l) asingaliumia mguu |

## Zoezi la 5: Nahau

**Eleza maana ya nahau zifuatazo kwa kutumia maana ulizopewa kwenye kisanduku.**

| |
|---|
| fanya uamuzi kwa muda mwafaka bila kukawia, takiana heri, tembea bega kwa bega au ubavu kwa ubavu, vaa nguo nzuri na mpya, fuatilia, kuwa na mamlaka, weka mashakani, kuwa kigeugeu, fanya jambo vizuri, chukua kitu au mtu kwa nguvu, pata kibali au ruhusa, mfanye mtu asikate tamaa |

**Mfano:** valia njuga – *fuatilia*
toa mtu upepo – *kumwomba mtu kitu fulani*

(i) teka nyara ……………………………………..
(ii) shika hatamu ……………………………………



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 18 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(iii) pata muhuri ……………………………………..
(iv) tia mtegoni ……………………………………..
(v) tia moyo ……………………………………..
(vi) vaa cheche ……………………………………..
(vii) wahi chuma kingali moto ……………………..
(viii) kuwa na ndimi mbili ………………………………….
(ix) gongeana bilauri ……………………………………..
(x) enda sambamba ……………………………………..

## Ufahamu

*Soma shairi lifuatalo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Mwanangu sogea hapa, keti chini nakuasa,
Wosia huu nakupa, usije pata **mikasa**,
Dunia hii si kapa, kuna mengi yanatesa,
Mwanangu hii dunia, kweli usi**takabari**.

Mosi, kiburi sitaki, **hadaa** hii dunia,
Kama upole hutaki, hekima kusukumia,
Utapata ya samaki, machozi ninakwambia,
Mwanangu hii dunia, kweli usitakabari.

Pili, dharau ni mwiko, heshima kwa kila mtu,
Binadamu ndugu zako, kila mara kwako **utu,**
Wakubwa ni **tunu** kwako, dharau kwako si kitu,
Mwanangu hii dunia, kweli usitakabari.

Tatu, sichekee **ufa**, utaujenga ukuta,
Wala sitafute sifa, mwisho wake utajuta,
Kumbuka mpenda sifa, moyo wake wafukuta,
Mwanangu hii dunia, kweli usitakabari.

Nne, uepuke **hila**, nakuomba zingatia,
Fitina siyo chakula, hiyo siyo yako njia,
Mpanga kifo kwa hila, hufa mshika **jambia,**
Mwanangu hii dunia, kweli usitakabari.

Tano, sijitie wizi, cheo hutojamiliki,
Nataka ufanye kazi, mali utaimiliki,
Ukiichagua nazi, **koroma** utamiliki,
Mwanangu hii dunia, kweli usitakabari.

Sita, ishike **karima**, kunyoa au kusuka,
Kutembea kusimama, au fanya ulotaka,
M**chutama** husimama, msimama huanguka,
Mwanangu hii dunia, kweli usitakabari.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 19 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Saba, situsi **mkunga**, nawe ungali mzazi,
Kwa kiburi utapanga, ya Muumba ndiyo kazi,
Mdomo sijekuchonga, ukauachia wazi,
Mwanangu hii dunia, kweli usitakabari.

Nane, Mola atowaye, na humpa binadamu,
Humpa amtakaye, hutaweza kudhulumu,
Yule mvua sifuye, humnyia kuhukumu,
Mwanangu hii dunia, kweli usitakabari.

Kenda, ninakukumbusha, mshike sana elimu,
Kama moto utawasha, sihofu kuvuja damu,
Ukisoma na kukesha, kileleni utadumu,
Mwanangu hii dunia, kweli usitakabari.

Kumi, **nanga** naitua, nakuachia bahari,
Nanga ukiifyatua, kamtafute jodari,
Akili kisukutua, moja ni yako **dahari**,
Mwanangu hii dunia, kweli usitakabari.

## Zoezi la 6: Ufahamu

1. Shairi hili lina beti ngapi?
2. Taja vina vya kati katika ubeti wa kwanza.
3. Mstari wa pili katika ubeti wa kumi na moja una mizani ngapi?
4. Mshairi ana maana gani anaposema mshike sana elimu?
5. Katika ubeti wa tano, kwa nini mwandishi anasema fitina siyo chakula?
6. Neno "mosi" kama lilivyotumika katika ubeti wa pili lina maana gani?
7. Neno kenda maana yake ni __________.
8. Taja mawazo mawili muhimu yatokanayo na shairi hili.
9. Mshairi anaposema "sichekee ufa" anamaanisha nini?
10. Kwa mawazo yako, pendekeza kichwa cha shairi hili.

## Zoezi la 7: Msamiati

**Eleza maana ya msamiati ufuatao:**

1. mikasa
2. takabari
3. hadaa
4. utu
5. tunu
6. ufa
7. hila
8. jambia
9. koroma
10. karima
11. chutama
12. mkunga
13. nanga
14. dahari

## Zoezi la 8: Utungaji

**Tunga shairi la kimapokeo lenye beti tano linalohusu umuhimu wa kilimo.**



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tatu

## Igizo la elimu ya biashara

### Utangulizi

*Katika sura hii, utajifunza elimu ya biashara. Utasoma na kuigiza igizo la elimu ya biashara. Hii itakusaidia kuanzisha biashara kwa kuzingatia wazo, uthubutu, mahitaji sahihi ya wateja, mahali sahihi pa kuweka biashara na mtaji. Pia, utajifunza kuweka viambishi katika vitenzi vya lugha ya Kiswahili.*

### Fikiri



1. Je, ulishawahi kuuza au kununua kitu chochote?
2. Ulishawahi kulima zao lolote? Uliyatumiaje mazao hayo?
3. Ulishawahi kuigiza? Uliigiza kama nani?

### Ufahamu

*Soma igizo lifuatalo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

**Elimu ya biashara**

Ilikuwa tarehe saba mwezi wa saba. Siku ya kilele cha maonesho ya wafanyabiashara nchini Tanzania ijulikanayo kama Sabasaba. Kilele cha maonesho haya huadhimishwa kila ifikapo tarehe saba mwezi wa saba kila mwaka. Siku hiyo huwa na maonesho ya bidhaa mbalimbali katika Uwanja wa Sabasaba ulioko jijini Dar es Salaam. Nilipata bahati ya kufika katika uwanja huo. Watu walikuwa na furaha na pilikapilika za kuuza na kununua bidhaa mbalimbali. Kulikuwa na kila aina ya burudani kutoka katika vikundi mbalimbali vya sanaa. Tulifika katika banda mojawapo na tulikuta kikundi kinaingia kwa mbwembwe **jukwaa**ni. Watu wote waliwashangilia waigizaji. Nilipotupa macho jukwaani, nilifurahi kumwona rafiki yangu ambaye alikuwa miongoni mwa **waigizaji.** Mara igizo lilianza.

**Wote:** Sisi ni kikundi cha sanaa cha Tupendane, tunawaletea igizo la **Elimu** ya **Biashara**. Karibuni.

**Watazamaji:** (*Wanapiga makofi kwa wingi.)*

**Mtambaji:** Hahahaaa! Amkeni amkeni! Leo ndiyo leo! Hata lepe la usingizi silitaki! Elimu ya biashara si ya kukosa! Hahaa...!



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 21 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Lusulo:** Hivi ndugu zangu mnajua umuhimu wa biashara nani anaweza kuniambia? (*Anasogea mbele ya waigizaji wenzake, anawauliza watazamaji huku akiwa ameshikilia sikio lake akionesha utayari wa kusikiliza majibu yao.)*



**Watazamaji:** (*Wanajibu kila mtu na jibu lake, mtazamaji mmoja anasikika akisema, "Biashara ilinitenda. Sina hamu…!")*

**Mtambaji:** Hahahaa! Biashara ilikutenda? Sasa leo tulieni tulii … mpate kuelewa. Hahaa! *(Anaondoka. Jukwaani panaonekana duka lililo**sheheni** bidhaa mbalimbali na genge la vitunguu nje. Ndani ya duka anaonekana Hadikwa aliyeachia tabasamu pana akimkaribisha mteja.)*

**Hadikwa:** Karibu … !

**Matika:** Ninahitaji madaftari matano na penseli sita haraka.

**Hadikwa:** Umepata rafiki yangu. Je, unahitaji bidhaa nyingine?

*(Anaonekana akimfungia Matika bidhaa huku akitabasamu.)*

**Matika:** Haswaa! Nipe rula moja na vifutio vitatu. Jumla ni shilingi ngapi?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Hadikwa:** Jumla ni shilingi elfu nne na mia tano. (*Alimjibu huku akichukua rula na vifutio kwa haraka na kumwekea kwenye mfuko.*)

**Matika:** Chukua na ninaomba chenji! *(Anatoa noti ya shilingi elfu tano mfukoni na kumkabidhi Hadikwa.)*

**Hadikwa:** (*Anapokea na kumrudishia shilingi mia tano pamoja na vitu alivyonunua.*) Asante sana! Karibu tena.

**Matika:** (*Anapokea chenji na kuondoka.)*

**Hadikwa:** Karibuni! Karibuni! (*Amezungukwa na wateja* ***lukuki****. Anawahudumia mmojammoja kwa haraka na kwa furaha huku wateja wengine wakipiga* ***soga****. Anaonekana Edo, Lusulo na Mlonji wakiongelea biashara ya Hadikwa.*)

**Edo:** Hadikwa ana kila aina ya bidhaa dukani.

**Lusulo:** Pia, anatumia lugha nzuri kwa wateja wake. Hachoki. Anajibu kila swali la mteja, tena kwa upole. Anawaonesha kila bidhaa wanayoihitaji wateja wake waione hata kama hawainunui.

**Mlonji:** Hadikwa ni mfanyabiashara mzuri. Ameanzisha shamba kubwa la vitunguu na ametoa ajira kwa vijana wengi.

**Edo:** Tena, anaendesha biashara kwa **faida**. Ana **ujuzi** wa kutosha wa kuendesha biashara yake. Vilevile, ana **mtaji** wa kutosha na anajua mahitaji sahihi ya **wateja** wake. Pia, ana uthubutu. Anasema kweli daima na amejua mahali sahihi pa kuweka biashara yake.

**Mlonji:** Haswaa! Hadikwa anatuuzia vitunguu wanakijiji wote. Tena nimesikia kutokana na ubora wa vitunguu vyake amepata soko la nje ya nchi. Kweli inabidi tubadilike tuache ujinga. Tutumie muda wetu vizuri tujipatie kipato kwa kufanya biashara yoyote halali.

**Wote:** (*Wanaonekana wakipeana mikono kuonesha kuwa wameelewa, kisha wanaondoka.)*

**Mtambaji:** Hahaaa …! Tupendane jamani! Kweli leo mmetupa raha. Shauri yenu wenzangu msipoyafanyia kazi. Mmesikia nini kuhusu kuanzisha biashara? Ngoja niwadokezee.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 23 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kwanza, ni wazo; pili, uthubutu; tatu, mahitaji sahihi kwa wateja; nne, mahali sahihi pa kuiweka biashara; tano, mtaji; sita, ukweli; saba je …?

**Watazamaji:** (Wote kwa pamoja *wanajibu kwa sauti za kuingiliana.)* Saba ni lugha nzuri kwa wateja!

**Mtambaji:** Hahaaa …! *(Anaondoka jukwaani huku akiwa anayumbayumba na watazamaji wanavunjika mbavu na kupiga makofi.)*

## Zoezi la Kwanza: Ufahamu

1. Taja jina la kikundi kilichoonesha igizo.
2. Nani alikuwa muuza duka?
3. Unadhani ni kwa nini waigizaji hawa waliigiza igizo hili?
4. Vitu gani muhimu vya kuzingatia katika kufanya biashara?
5. Taja idadi ya wahusika katika igizo.
6. Ungepewa nafasi ya kuigiza igizo hili ungeigiza nafasi ya nani? Kwa nini?
7. Taja kitu kingine muhimu cha kuzingatia wakati wa kufanya biashara.
8. Je, unadhani watazamaji walilipenda igizo hili?
9. Kwa nini wahusika hawa walipeana mikono?
10. Igizo hili linatufundisha nini?

## Zoezi la pili: Kazi ya kufanya

**Igiza na wenzako igizo ulilolisoma.**

## Zoezi la 3: Msamiati

**Tunga sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo:**

1. jukwaa
2. waigizaji
3. elimu
4. biashara
5. sheheni
6. lukuki
7. soga
8. faida
9. ujuzi
10. mtaji
11. wateja

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 24 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 4: Mazoezi ya lugha

### A. Badili sentensi zifuatazo kuwa katika kauli ya kutendewa.

**Mfano:** Anaanika nyavu zake zikauke.
*Anaanikiwa nyavu zake zikauke.*

(i) Anacheza ngoma kwa ustadi mkubwa.
(ii) Tumemsaidia bibi kusaga karanga.
(iii) Dada alipiga simu asubuhi na mapema.
(iv) Tumepiga pasi nguo zetu.
(v) Walipanga nini katika mkutano wa tarafa?
(vi) Aisha anakaanga mihogo kwa ajili ya watoto wake.
(vii) Timu yetu ilicheza mechi vizuri.
(viii) Mgeni rasmi alisoma risala kwa ustadi mkubwa.
(ix) Wanafunzi waligonga kengele ya mapumziko.
(x) Panya alisumbua ghalani.

### B. Badili vitendo vifuatavyo kuwa katika kauli ya kutendeka.

**Mfano:** shika - *shikika*
toboa - *toboka*

(i) tosha (iii) tenda (v) pika (vii) futa
(ii) andika (iv) ng'ata (vi) ita (viii) sikia

### C. Badili vitenzi kuwa katika kauli za utendaji zifuatazo: kutendwa, kutendea, kutendewa, kutendeana, kutendesha, kutendana na kutendeka.

| Na. | kutenda | kutendwa | kutendea | kutendewa | kutendeana | kutendesha | kutendana | kutendeka |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mfano | *tuma* | *tumwa* | *tumia* | *tumiwa* | *tumiana* | *tumisha* | *tumana* | *tumika* |
| (i) | andika | | | | | | | |
| (ii) | kusanya | | | | | | | |
| (iii) | peleka | | | | | | | |
| (iv) | kanda | | | | | | | |
| (v) | funga | | | | | | | |
| (vi) | chunga | | | | | | | |
| (vii) | sema | | | | | | | |
| (viii) | chora | | | | | | | |
| (ix) | tazama | | | | | | | |
| (x) | piga | | | | | | | |

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 25 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**D. Unganisha sentensi zifuatazo kwa kutumia irabu "u" na "e" bila kutumia kiunganishi.**

**Mfano:** Lamba asali. Pata utamu.
*Lamba asali* ***u****pat****e*** *utamu.*

(i) Fungua mlango. Ingia ndani.
(ii) Vaa miwani. Soma sentensi hizi.
(iii) Igiza igizo. Shangiliwa kwa mbwembwe.
(iv) Chota maji. Mimina kwenye pipa.
(v) Nenda sokoni. Nunua nyanya.
(vi) Pukuchua mahindi. Weka kwenye gunia.
(vii) Fuga nyuki. Rina asali.
(viii) Andika barua. Tuma kwa njia ya posta.
(ix) Soma kwa bidii. Fanikiwa katika maisha yako.
(x) Ongea Kiswahili fasaha. Kuza lugha ya Taifa.

**E. Bainisha kauli za utendaji katika sentensi zifuatazo:**

**Mfano:** Kokoto na mchanga zimechanganyika vizuri. *Kauli ya kutendeka*
Majibu yaliendana na maswali. *Kauli ya kutendana*

(i) Karunguyeye na Nungunungu wanapigana. .........................
(ii) Viongozi wa kata ya Mbuyuni hutembeleana mara mbili kwa mwezi. ..........................
(iii) Dada anamsomesha kaka yetu wa kwanza. ..........................
(iv) Kande zilipikwa vizuri na mama. ..........................
(v) Mlima unamiminika theluji mithili ya mto. ..........................
(vi) Walimu na wanafunzi wa Shule ya Msingi Tupendane tunashirikiana kwa kila jambo. ..........................
(vii) Zamoyoni alishinda mbio za nyika na kurudi na medali. .........................
(viii) Mwalimu wetu ana utaratibu wa kuandikiwa majina ya wasumbufu darasani. ........................

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 26 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**F. Jaza nafasi zilizo wazi katika jedwali lifuatalo kwa kuzingatia kauli za utendaji:**

| Na. | kutenda | kutendwa | kutendewa | kutendeana | kutendea | kutendeka |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mfano | pika | pikwa | pikiwa | pikiana | pikia | pikika |
| (i) | ______ | ______ | ______ | ______ | tupia | ______ |
| (ii) | ______ | ______ | ______ | imbiana | ______ | ______ |
| (iii) | kata | ______ | ______ | ______ | ______ | ______ |
| (iv) | ruka | ______ | ______ | ______ | ______ | ______ |
| (v) | teka | ______ | ______ | ______ | ______ | ______ |

## Zoezi la 5: Utungaji

**Tunga habari yenye maneno mia moja (100) kuhusu biashara unayoipenda ukizingatia yafuatayo:**

(a) Jina la biashara yako.

(b) Inahusu nini?

(c) Faida uzipatazo kwenye biashara yako.

(d) Changamoto zake.

(e) Namna ya kukabiliana na changamoto hizo.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 27 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Nne

## Hadithi

### Utangulizi

*Katika sura hii, utajifunza kusimulia hadithi yenye methali na kuelezea mafunzo ya methali hizo. Pia, utajifunza mianzo na miisho ya hadithi. Vilevile, utajifunza methali nyingine zenye maana zinazofanana na methali zilizotajwa katika hadithi. Zaidi ya hayo, utajifunza methali nyingine zenye maana iliyo kinyume na zile zilizotajwa katika hadithi. Maarifa haya utayatumia katika utunzi wa hadithi mbalimbali.*

### Fikiri



1. Je, umewahi kusimulia hadithi?
2. Hadithi hiyo ilihusu nini?
3. Je, ulijifunza nini kutokana na hadithi hiyo?

### Ufahamu

*Soma hadithi ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

**Umoja ni nguvu**

Katika kijiji cha Songambele, kulikuwa na vijana wawili marafiki. Kijana mmoja aliitwa Mayumba na mwingine aliitwa Madeha. Mayumba na Madeha walikuwa marafiki sana. Mara nyingi, walishirikiana katika shida na raha.

Vijana wa Songambele na wakazi wengine wa kijiji hicho walijishughulisha sana na kazi mbalimbali. Kuna waliofanya **uashi**, **useremala,** ukulima, uvuvi na wengine walifanya biashara na kazi nyingine nyingi. Mayumba na Madeha walifanya kazi za ufundi. Mayumba alikuwa fundi mwashi na Madeha alikuwa seremala.

Siku moja Madeha alimtembelea Mayumba mahali pake pa kazi. Mayumba alikuwa amepewa kazi ya kujenga nyumba na Bwana Chaburuma. Madeha alipofika mahali pale, alikuta mzozo mkubwa kati ya Bwana Chaburuma na fundi Mayumba.

Kuona hivyo, Madeha alitaka kujua sababu ya mzozo huo. Bwana Chaburuma akamweleza kuwa Mayumba alikuwa hajengi nyumba yake vizuri.

Tena, akadai kwamba alikuwa anajenga polepole sana wakati anafahamu



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 28 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kuwa mvua za masika zimekaribia. Bwana Chaburuma alihofia kuwa mvua ingesomba mchanga na kumletea hasara.

Mayumba aliposikia hivyo, akaanza kujitetea. Alidai kuwa alijenga polepole kwa sababu alikuwa na **kibarua** mmoja tu. Akaongeza kusema kuwa hiyo ilitokana na bwana Chaburuma mwenyewe kumlipa **ujira** mdogo. Akadai kuwa kwa vile hakulipwa fedha za kutosha, asingeweza kuajiri vibarua wa kutosha. Tena, akajitetea kwa utani kuwa **polepole ndio mwendo** na **harakaharaka haina baraka**. Bwana Chaburuma aliposikia hivyo, aka**hamaki**.

Madeha akaanza kutafakari namna ya kusuluhisha mzozo ule. Wakati akifikiria cha kufanya, simu yake ikaita mfukoni. Alipoitoa, aliona jina la mtu aliyekuwa akimpigia simu, akaangalia muda, akashtuka! Alikuwa anapigiwa simu na mteja wake aliyetaka atengenezewe kitanda. Madeha hakuwa amemaliza kukitengeneza. Alikimbia haraka kurudi kazini kwake pasi na kuaga ili kwenda kukimalizia. Alijisemea kimoyomoyo, "**Mwenzako akinyolewa, wewe tia maji.**"



Wakati Mayumba na mwenye nyumba wakiendelea kuzozana, alipita mtu wa **makamo** aliyeitwa Hekima. Aliwa**sabahi**, kisha akawauliza, "Ndugu zangu, mbona mnazozana, kulikoni?" Bwana Chaburuma akajibu, "Nimempa Mayumba kazi ya kujenga nyumba, lakini kasi ya ujenzi ni ndogo sana. Hana wasaidizi wa kutosha, halafu sababu anazonipa si za msingi. Vilevile, majibu yake yananikera."



FOR ONLINE USE ONLY

KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 29 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Bwana Hekima alizidi kuwa**dodosa** kwa maswali ya hapa na pale ili ajue namna ya kuwasaidia. Alimuuliza Mayumba swali juu ya swali. Akataka hata kujua namna walivyokubaliana alipwe jasho lake. Kwa bahati nzuri, kila mmoja alijibu maswali yake kadiri ilivyotakiwa. Baada ya kupata taarifa zote hizo, Hekima aligundua kuwa Mayumba ndiye aliyekuwa na makosa. Alikuwa amekiuka makubaliano waliyowekeana awali kwamba ajenge nyumba kwa muda mfupi. Badala yake, alikuwa ameshatumia muda zaidi ya ule waliokubaliana. Tena, malipo ya kazi aliyoomba na kukubaliwa, yalikuwa makubwa mno kuliko yale waliyolipwa mafundi wengine kijijini. Hekima alitikisa kichwa, akasema kwa masikitiko, "Kwa kweli, **upele humwota asiye na kucha**."

Mayumba aliposikia hayo, akauliza, "Una maana gani Bwana Hekima?" Hekima akamjibu, "Vijana wengi hapa kijijini wana ujuzi kama wako, na walitamani kupewa kazi hii ili wajipatie kipato. Bahati hiyo iliangukia kwako, lakini hutaki kufanya kazi kwa bidii kama mlivyokubaliana na mwenye nyumba." Kumbuka wahenga walisema, **"Bahati ikibisha hodi, sharti ufungue mlango mwenyewe**."

Mayumba ali**duwaa** aliposikia maneno yale ya Bwana Hekima. Hakujua maana yake. Akamuuliza, "Hapo una maana gani Bwana Hekima?" Bwana Hekima akamjibu, "Wahenga walisema, "**Asiyejua maana, haambiwi maana; akiambiwa maana, haelewi maana.**" Hata hivyo, mimi ninakupenda sana, kijana wangu. Ninapenda kukuona unapata maendeleo. Ukipata maendeleo, utanufaika wewe mwenyewe, familia yako, na utaleta maendeleo kijijini kwetu na kwenye taifa letu. Ninataka nikueleze kwamba unapopewa kazi, huna budi kuifanya vizuri. Ukiifanya vizuri, italeta manufaa mengi kwa watu wengi. Vinginevyo, ukiifanya vibaya, italeta hasara kubwa kwako na kwa watu wengine. Aliyekupa hiyo kazi hatafurahi kukuona ukiharibu kazi yake. Anaweza kukunyang'anya. Kumbuka Waswahili wanasema, "**Kazi mbaya si mchezo mwema**."

Bwana Hekima alibaini kuwa Mayumba alikuwa **mbinafsi**. Hakutaka kuajiri wasaidizi wengi ili abakiwe na fedha nyingi atakayolipwa baada ya kumaliza kazi.

Bwana Hekima alipokuwa akiendelea kufikiria namna nzuri ya kumaliza mzozo ule, ngurumo kubwa ilisikika upande wa Mashariki. Wingu kubwa lilianza ku**tanda** angani pia.

Kila mmoja alishtuka. "Mungu wangu!", alisema Chaburuma, huku macho



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 30 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

yamemtoka kwa hofu ya kupata hasara kama mvua kubwa ingenyesha. Kisha aka**ng'aka**, "**Dalili ya mvua ni mawingu.** Hii mvua itanyesha muda si mrefu," alimwambia fundi wake, kisha akamuuliza, "Hivi, fundi, hiyo hasara itakuwa ya nani kama hii mvua itashuka sasa hivi?"

Mayumba aliposikia hivyo, alipandwa na **ghadhabu**. Akamjibu Chaburuma kwa jeuri, "Kama unaona sifanyi kazi yako vizuri, tafuta fundi mwingine!"

Bwana Hekima aliingilia kati harakaharaka, "Kijana wangu Mayumba, **kiburi si maungwana**! Wa kale walisema, "**Hasira, hasara**." Tena, **hasira ya mkizi ni furaha ya mvuvi**. Kwa nini usitafute vibarua wengine wa kukusaidia ili umalize kazi hii haraka?"

Wakati huo, Mayumba hakutaka kumsikiliza mtu yeyote. Alikusanya kila kilicho chake, akatoa pesa mfukoni na kumlipa yule kibarua aliyekuja naye, akaondoka zake. Kila mmoja aliyekuwa pale, alibaki mdomo wazi kwa matendo ya Mayumba. Bwana Hekima akashika tama na kusema, "Kweli, **sikio la kufa halisikii dawa**!"

Muda si mrefu tangu Mayumba alipoondoka mahali pale, mafundi wengine walifika na kuanza kujenga kwa kasi na ujuzi wa hali ya juu. "**Mungu si Athumani**," mawingu yalitawanyika na mvua haikunyesha siku hiyo na kwa wiki nzima iliyofuata. Wale mafundi walifanikiwa kumaliza kazi yao kwa muda mfupi. Bwana Chaburuma alifurahi sana na aliwalipa stahiki zao zote.

Mayumba aliposikia habari hiyo, alijuta sana. Alidhani kuwa Bwana Chaburuma angemwita tena licha ya kuondoka siku ile. Sasa hakuwa na pesa yoyote, na hakuweza kujinunulia mahitaji mbalimbali. Alianza kuyaelewa maneno aliyokuwa akiambiwa na bwana Hekima siku ile. Kwa hakika, "**Majuto ni mjukuu, huja baada ya kitendo**."

Watu wengi kijijini Songambele walisikia habari za wale mafundi. Walianza kuwapa kazi za kujenga nyumba zao. Wale mafundi walijipatia fedha nyingi sana siku hadi siku. Maisha yao yakastawi kwa sababu ya kufanya kazi kwa kujituma, kwa uhodari, na kwa umoja wao. Kwa hakika, "**Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu**."

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 31 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Katika hadithi uliyoisoma, vijana gani walikuwa marafiki?
2. Marafiki hao walishirikiana katika mambo gani?
3. Je, fundi mwashi aliitwa nani?
4. Je, Madeha alikuwa anafanya kazi gani?
5. Kwa nini Bwana Chaburuma alitafuta mafundi wengine?
6. Nani alikuta mzozo kati ya Mayumba na Bwana Chaburuma?
7. Kwa nini Bwana Chaburuma alitaka nyumba yake ijengwe haraka?
8. Madeha aliondoka haraka kurudi kazini kwake ili kufanya nini?
9. Kwa nini Mayumba hakutaka kuajiri vibarua wengine?
10. Umejifunza nini kutokana na hadithi uliyoisoma?

## Zoezi la pili: Msamiati

**Tunga sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo:**

1. uashi
2. useremala
3. kibarua
4. ujira
5. hamaki
6. makamo
7. sabahi
8. dodosa
9. duwaa
10. mbinafsi
11. tanda
12. ng'aka
13. ghadhabu

## Zoezi la 3: Mazoezi ya lugha

**A. Eleza maana za methali zifuatazo:**

**Mfano:** Bila silaha, usiingie vitani.

**Maana yake:** *Ni muhimu kujiandaa vizuri kabla ya kuanza shughuli fulani.*

Afadhali juhudi kuliko pendeleo.

**Maana yake:** *Bora kupata kitu kutokana na bidii au juhudi yako kuliko kupendelewa.*

(i) Polepole ndiyo mwendo.
(ii) Harakaharaka, haina baraka.
(iii) Mwenzako akinyolewa, wewe tia maji.
(iv) Upele humwota, asiye na kucha.
(v) Bahati ikibisha hodi, sharti ufungue mlango mwenyewe.
(vi) Kazi mbaya si mchezo mwema.
(vii) Dalili ya mvua ni mawingu.
(viii) Kiburi si maungwana.
(ix) Hasira, hasara.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 32 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(x) Hasira ya mkizi, ni furaha ya mvuvi.
(xi) Sikio la kufa, halisikii dawa.
(xii) Mungu si Athumani.
(xiii) Majuto ni mjukuu, huja baada ya kitendo.
(xiv) Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu.

**B. Chagua methali kutoka kwenye kisanduku, kisha iandike mbele ya maelezo yanayoendana nayo.**

**Mfano:** Siame alikuwa kiongozi wa darasa. Wanafunzi wenzake walimchukia kwa sababu alikuwa ni mtu wa kufuata sheria. Halikadhalika, Siame alikuwa mtetezi wa wenzake pale walipoonewa na viranja wa shule. Wanafunzi wa darasani kwake Siame walipenda kusema baniani mbaya kiatu chake dawa.

| |
|---|
| chanda chema huvikwa pete, fedha fedheha, penye nia pana njia,<br>cha mlevi huliwa na mgema, fimbo ya mnyonge hulipwa na Mungu,<br>baniani mbaya kiatu chake dawa, funzo la mjinga ni taabu,<br>hasara humfika mwenye mabezo, heri jirani karibu kuliko ndugu mbali,<br>kazi isiyo na manufaa kutenda si inda, msahau kwao ni mtumwa |

(i) Baba Pendo alimhimiza mwanawe kufanya bidii katika masomo yake ili aweze kufaulu vizuri. Mara nyingi, Baba Pendo alisikika akisema, "Mwanangu, kumbuka kuwa ________________ ."

(ii) Matajiri wengi hujisahau na kudhani kuwa maskini si watu. Wanasahau kuwa ________________ .

(iii) Adili alidhulumiwa fedha na rafiki yake. Watu walimshauri ampeleke polisi, lakini yeye alisema, "Nimeamua kuachana naye kwani ________________ ."

(iv) Chausiku alikuwa mwanafunzi mwenye bidii shuleni. Kila muhula alikuwa wa kwanza darasani. Alipenda sana kuendelea na masomo ya juu atakapohitimu elimu ya msingi. Alipomaliza Darasa la Saba, alifaulu mtihani wake, akachaguliwa kujiunga na elimu ya sekondari. Chausiku akakumbuka methali isemayo ________________.

(v) Kijana mmoja alikuwa na mali nyingi, lakini hakupenda kuweka akiba. Hakusikiliza ushauri wa wenzake walipomshauri kuweka akiba. Siku moja wezi walimvamia dukani kwake na kuiba kila kitu, akafilisika. Hapo ndipo alipogundua kuwa ________________ .



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 33 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(vi) Mtu mmoja aliwadharau majirani zake kwa sababu ndugu zake walikuwa ni matajiri. Siku moja aliingiliwa na wezi usiku. Alipiga kelele kuomba msaada, majirani zake wakatoka kumsaidia. Mtu huyo aliwashukuru na kusema, “ _________________.”

(vii) Siyawezi alikuwa anafuga kuku wa kienyeji. Kila mara kuku wake walipokuwa wakubwa, waliibwa. Mwishowe alichoka, akaamua kuacha ufugaji. Siyawezi aliona kuwa _________________ .

(viii) Mwenyekiti aliwaonya vijana waliotumia fedha zao kwa mambo ya anasa. Vijana hao walimdharau mwenyekiti wao. Walimdhihaki na kumwambia, “Fedha ni matumizi.” Yeye aliwajibu kwa kuwaambia, “Kumbukeni, _________________ .”

(ix) Mateso alienda kuishi kijiji cha jirani. Aliishi huko kwa muda mrefu. Aliwasahau ndugu na jamaa zake. Akiwa ugenini, alipata taabu nyingi sana, lakini aliona aibu kurudi kwao kwani hakuwa na mawasiliano na ndugu zake kwa muda mrefu. Mateso alijutia tabia yake na kusema, “Kwa hakika, _________________ .”

**C. Oanisha maneno kutoka Sehemu A na vinyume vyake kutoka Sehemu B kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye nafasi iliyoachwa wazi.**

| Na. | Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|---|
| (i) | funga _______ | (a) dharau |
| (ii) | funika _______ | (b) karipia |
| (iii) | tengeneza _______ | (c) tenganisha |
| (iv) | swali _______ | (d) futa |
| (v) | unganisha _______ | (e) tajiri |
| (vi) | bembeleza _______ | (f) haribu |
| (vii) | amani _______ | (g) zima |
| (viii) | maskini _______ | (h) fungua |
| (ix) | washa _______ | (i) mjini |
| (x) | kijijini _______ | (j) vita |
| | | (k) funua |
| | | (l) jibu |

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 34 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**D. Andika methali sahihi kumi (10) kutokana na jedwali lifuatalo:**

**Mfano:** *Moja shika si kumi nenda rudi.*
*Ajengaye si alalaye.*

| | | |
|---|---|---|
| Atafutaye upotovu<br>Afya<br>Afungaye kibwebwe<br>Elimu maisha<br>Ajengaye<br>Hata kiporo<br>Kila mshupavu<br>Kuishi kwingi<br>Kumpa mwenzako<br>Kila mnyamavu<br>Moja shika | si<br><br>ni | mwerevu<br>kutupa<br>mali<br>alalaye<br>bure ana mchezo<br>kumi nenda rudi<br>mpumbavu<br>vitabu<br>ugali<br>kizuri<br>kuona mengi |

**E. Chagua jibu lililo sahihi katika maswali yafuatayo:**

(i) Ujumbe unabebwa na ____________ katika hadithi.
(a) wahusika
(b) watu
(c) wanyama
(d) viongozi

(ii) Kazi ya fundi mwashi ni:
(a) kupiga deki
(b) kujenga
(c) kulima bustani
(d) kumwagilia

(iii) Maneno yafuatayo ni mianzo ya hadithi isipokuwa ____________ .
(a) Kitendawili ...
(b) Paukwa ...
(c) Hapo kale ...
(d) Siku moja ...

(iv) Jiwe lilitumbukia mtoni ____________
(a) chubwi!
(b) kacha!
(c) pruu!
(d) puu!

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(v) Rafiki yake Mayumba aliitwa Madeha. Neno lililopigiwa mstari lina maana sawa na neno lifuatalo.
  (a) Jirani
  (b) Ndugu
  (c) Adui
  (d) Mpendwa

(vi) Kazi ya fundi seremala ni kutengeneza:
  (a) viatu
  (b) mabomba
  (c) samani
  (d) umeme

(vii) Bwana Hekima kwa jina lingine unaweza kumwita:
  (a) Bwana maarifa
  (b) Bwana Amani
  (c) mwanamwali
  (d) mtu wa busara

(viii) Kibarua ni mtu anayefanya kazi ya ____________ .
  (a) kumsaidia fundi
  (b) kusimamia ujenzi
  (c) mwenye nyumba
  (d) kucheza na fundi

(ix) Kazi ya Madeha ilikuwa ni useremala. Kazi hiyo inamaanisha:
  (a) fundi wa ujenzi
  (b) fundi barabara
  (c) fundi wa samani
  (d) fundi wa rangi

(x) Mayumba alikosa kazi kwa sababu alikuwa na kiburi. Neno lililopigiwa mstari lina maana gani?
  (a) mpole
  (b) mkaidi
  (c) mkorofi
  (d) mvivu

(xi) Bwana Hekima alimkanya Mayumba kuacha ujeuri. Neno lililopigiwa mstari lina maana gani?
  (a) kusabahi
  (b) kukanya

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 36 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(c) kuonya
(d) kupongeza

(xii) Mayumba alipoonesha jeuri, mwenye nyumba alifanya nini? Swali hili lipo katika wakati gani?

(a) uliopita
(b) ujao
(c) uliopo
(d) wa sasa

## F. Malizia methali zifuatazo:

(i) Asiyesikia la mkuu, ..........................
(ii) Kutoa ni moyo, ..........................
(iii) Linalowezekana leo, ..........................
(iv) Mkataa wengi ni ..........................
(v) Damu ni nzito, ..........................
(vi) Hamadi ..........................
(vii) Mdharau mwiba, ..........................
(viii) Chema chajiuza, ..........................
(ix) Chelewa chelewa, ..........................
(x) La kuvunda, ..........................

## G. Andika methali zenye maana sawa na methali zifuatazo:

**Mfano:** Kula kutamu, kulima mavune.
*Kukopa harusi, kulipa matanga.*

(i) Hakuna msiba, usiokuwa na mwenzie.
(ii) Mwenda pole, hajikwai.
(iii) Ngoja ngoja, huumiza matumbo.
(iv) Mchelea mwana kulia, hulia yeye.
(v) Majuto ni mjukuu.
(vi) Baada ya dhiki, faraja.
(vii) Heri nusu shari, kuliko shari kamili.
(viii) Maji ukiyavulia nguo, huna budi kuyaoga.
(ix) Ng'ombe wa maskini hazai; akizaa, huzaa dume.
(x) Baada ya kisa mkasa.

## H. Andika neno moja linalojumuisha maneno yaliyo katika mabano.

**Mfano:** Hospitalini wanatibu (homa, kikohozi, kuhara na kaswende)

Hospitalini wanatibu magonjwa.

(i) Hapa dukani wanauza (sahani, masufuria, vikombe na mabirika)
Hapa dukani wanauza ________________________ .

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(ii) Dada alifua (shati, suruali, sketi, kanga na kitenge)
Dada alifua _____________________ .

(iii) Mama alipika (ndizi, wali, kande, biriani na ugali)
Mama alipika ____________________ .

(iv) Baba alileta (maembe, machungwa, mananasi na matikiti)
Baba alileta ___________ .

(v) Bibi amevuna (mahindi, uwele, mtama na mpunga)
Bibi amevuna _______________________ .

(vi) Wanakijiji walitengeneza (viti, meza, madawati na makabati)
Wanakijiji walitengeneza _____________________ .

(vii) Sungusungu walibeba (visu, mishale, mapanga na mikuki)
Sungusungu walibeba _____________________ .

(viii) Mgeni anapenda (chai, soda, juisi, maziwa na togwa)
Mgeni anapenda _____________________ .

(ix) Mimi (ninaipenda, ninailinda na ninaitumikia) nchi yangu.
Mimi ni ______________________ wa nchi yangu.

(x) Sikujua amebeba (sato, sangara, perege na changu)
Sikujua amebeba _____________________________ .

## Zoezi la 4: Utungaji

**Tunga hadithi yenye maneno kati ya mia moja hadi mia moja ishirini (100 – 120) yenye methali ndani yake.**

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 38 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tano

## Taswira za nahau

### Utangulizi

*Katika sura hii, utasoma hadithi inayohusu Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika. Pia, utaweza kusimulia hadithi na kujifunza taswira zilizomo katika nahau. Maarifa haya yatakusaidia kuzitumia vema nahau katika mawasiliano.*

### Fikiri



1. Je, umewahi kuhudhuria maadhimisho yoyote?
2. Maadhimisho hayo yalihusu nini?
3. Je, ulijisikiaje ulipohudhuria maadhimisho hayo? Kwa nini?

### Ufahamu

*Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

**Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika**

Mwalimu Sikujua anafundisha katika Shule ya Msingi Kahama. Siku moja, aliwatangazia wanafunzi wa shule yake kuwa kesho itakuwa siku ya ku**adhimisha** mtoto wa Afrika. Maadhimisho haya hufanyika tarehe 16 ya mwezi Juni kila mwaka.

Maganga ambaye ni mwanafunzi wa Darasa la Sita alifurahi sana. Alimuuliza mwalimu Sikujua, "Mwalimu, maadhimisho hayo yatafanyika wapi?" Mwalimu Sikujua alimjibu, "Maadhimisho hayo yatafanyika katika Shule ya Msingi Mahande." Chausiku ambaye ni mwanafunzi wa Darasa la Tano, alimuuliza mwalimu."Je, wanafunzi wote wanaruhusiwa kwenda kwenye maadhimisho hayo?" Mwalimu Sikujua alijibu, "Ndiyo." Mwalimu Sikujua alimteua Bahati ku**shika usukani** katika kuhamasisha wanafunzi wenzake. Mwalimu Sikujua aliwaomba wanafunzi kuwa **bega kwa bega** katika kufanikisha maadhimisho hayo.

Kesho yake, wanafunzi walifika shuleni tayari kwenda kwenye maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika. Wanafunzi walihamasika na kujitokeza kwa wingi. Kabla ya kwenda kwenye maadhimisho, Mwalimu Sikujua aliwasisitiza wanafunzi kuwa na **nidhamu**.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 39 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mwalimu Sikujua aliondoka na wanafunzi kwenda Shule ya Msingi Mahande kwenye Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika. Mwanafunzi aitwaye Luhumbika aliwa**piga chenga** wanafunzi wenzake na kurudi nyumbani. Mwalimu Sikujua na wanafunzi wengine waliwasili Shule ya Msingi Mahande na kukutana na wanafunzi wengine. Ratiba ya maadhimisho ilitangazwa. Vikundi mbalimbali vya ngoma viliitwa uwanjani ili ku**tumbuiza**. Kulikuwa na kikundi cha ngoma cha Mazinde, Mzalendo na Mkuki. Kati ya vikundi vyote vya ngoma, kikundi cha Mazinde kili**tia fora**.



Baada ya burudani ya ngoma, Nyangeta aliitwa ili aghani shairi. Alighani shairi vizuri sana. Shairi lilikuwa linahusu **haki** za watoto. Alipokuwa akighani shairi, wanafunzi wenzake walikuwa wakimshangilia. Baada ya kughani shairi, watu wote walimpigia makofi na mgeni rasmi alimpa zawadi. Mgeni rasmi wa maadhimisho hayo alikuwa Afisa Maendeleo wa Wilaya.

Baada ya kughani shairi, mshereheshaji alimwita msomaji wa risala aliyeandaliwa. Mwanafunzi aitwaye Bukehele alienda kusoma risala mbele ya mgeni rasmi. Risala hiyo ilieleza kuwa watoto wanatakiwa kupewa haki za msingi. Haki hizo ni elimu, kucheza, kupendwa na kulindwa.

Mara baada ya kusoma risala, Bukehele alimkabidhi mgeni rasmi risala hiyo. Mgeni rasmi alii**pokea kwa mikono miwili**. Zoezi la kusoma risala lilipokamilika, kikundi cha Mazinde kilikaribishwa tena uwanjani ili kutumbuiza. Kikundi hicho kilicheza ngoma kwa madaha, kisha kuanguka na kuinuka kwa haraka.



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 40 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kitendo hicho kilimfanya mgeni rasmi na wanafunzi wote ku**angua kicheko**. Mgeni rasmi alifurahi sana, kisha aliendа kuwapa **tuzo**. Alisimama na kuwapungia mkono, kisha alitangaza na kutoa zawadi ya fedha kwa watumbuizaji.

Mara baada ya kutoa zawadi, mgeni rasmi alitoa hotuba yake. Aliwaomba watoto wasimame **kidete** kudai haki zao zinapokiukwa. "Kamwe msiogope. Ninyi ni jeshi kubwa," mgeni rasmi alisema. Mwisho, aliwashukuru watu wote waliohudhuria maadhimisho hayo. Mwalimu Sikujua aliwakusanya wanafunzi wake na kuwaambia warejee shuleni.

Walipokuwa njiani wakirejea shuleni kwao, wali**tupa jicho** pembeni mwa barabara. Walimwona Upendo akiwa amebeba mtoto mdogo. Alionekana mwenye huzuni kubwa. Wanafunzi waliamua kumsogelea na kumuuliza, "Upendo, kwa nini tangu juzi hujaja shuleni?" Aliwajibu, "Mama yangu aitwaye Nyamate ameniachisha shule ili niwe **yaya** wakati anafanya kazi zake. Amenizuia kuja shuleni tangu juzi ndiyo maana nina huzuni kubwa."

Wanafunzi waliamua kumchukua Upendo mpaka kwa mama yake. Nyamate alipoangalia kundi kubwa la wanafunzi wakielekea nyumbani kwake, ali**shikwa na fadhaa.** Aliwauliza, "Kulikoni?" Wanafunzi walimweleza kuwa wamekuja kufuatilia kwa nini amemwachisha Upendo shule. Nyamate ali**hamaki** na kuwauliza wale wanafunzi, "Ninyi nani?" "Sisi ni wanafunzi wenzake Upendo. Tunatoka kwenye Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika," walijibu.

"Pia, tunatakiwa kusimama kidete kudai haki za watoto pale zinapokiukwa. Haki ya Upendo ya kupata elimu imekiukwa. Hivyo, huna budi kumruhusu aendelee na shule. Kumbuka kwamba elimu ni ufunguo wa maisha," waliongeza. Nyamate ali**kata shauri** na kuwaambia wale wanafunzi, "Kweli elimu ndiyo mkombozi wa mtoto wa kike. Kuanzia leo, ninamruhusu Upendo aendelee na masomo yake. Sitamwachisha tena." Wanafunzi walimshukuru Nyamate na kuondoka kuelekea shuleni.

Kesho yake asubuhi, Nyamate alimwamsha Upendo aende shuleni. Upendo aliamka na kujiandaa, kisha alikwenda shuleni. Alipofika shuleni, alipokelewa na wanafunzi wenzake. Wanafunzi walifurahi sana. Waliongozana naye hadi kwa mwalimu wa darasa aitwaye Lushinge aliyekuwa ofisini kwake aki**chapa kazi.** Alimpokea na kumpeleka darasani. Upendo aliwashukuru wanafunzi wenzake kwa kumsaidia kurudi shuleni. Upendo aliendelea na masomo yake vizuri.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 41 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Mwalimu Sikujua anafundisha shule gani?
2. Nani aliwatangazia wanafunzi Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika?
3. Maganga ni mwanafunzi wa darasa la ngapi?
4. Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika yalifanyika wapi?
5. Kikundi gani kilitia fora katika Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika?
6. Nani alisoma risala siku ya Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika?
7. Mama yake Upendo anaitwa nani?
8. Kwa nini mama yake alimwachisha Upendo shule?
9. Eleza haki nne za msingi za mtoto kama zilivyoelezwa katika habari uliyosoma.
10. Umejifunza nini kutokana na habari hii?

## Zoezi la pili: Msamiati

**Tunga sentensi mbili kwa kila neno.**

1. adhimisha
2. nidhamu
3. tumbuiza
4. haki
5. tuzo
6. kidete
7. yaya
8. hamaki

## Zoezi la 3: Nahau

**Oanisha nahau na taswira zake katika jedwali lifuatalo:**

**Mfano:** *pigwa chini – kuachishwa kitu au jambo fulani*

| Nahau | Taswira za nahau |
|---|---|
| (i) shika usukani | (a) kufanya kazi kwa bidii |
| (ii) tia fora | (b) kuwa na kiburi au jeuri |
| (iii) pokea kwa mikono miwili | (c) kuwa na wasiwasi au woga |
| (iv) angua kicheko | (d) fukuzwa kazi |
| (v) simama kidete | (e) kucheka kwa sauti kubwa |
| (vi) tupa jicho | (f) kukwepa au kumtoroka mtu |
| (vii) shikwa na fadhaa | (g) kufanya jambo kwa siri |
| (viii) kata shauri | (h) kuzunguka mahali fulani |
| (ix) chapa kazi | (i) kufanya jambo bila mafanikio |
| (x) kula njama | (j) kuamua au kutoa uamuzi kuhusu jambo fulani |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

| | |
|---|---|
| (xi) vimba kichwa | (k) kuangalia mbali kwa wepesi |
| (xii) gonga mwamba | (l) kunywa pombe |
| (xiii) kata kona | (m) kuongoza chombo au watu kufanya jambo fulani |
| (xiv) piga maji | (n) kupokea kitu kwa heshima bila kinyongo |
| (xv) piga chenga | (o) kushinda au kufanya jambo vizuri zaidi |
| | (p) simama madhubuti bila woga |

## Zoezi la 4: Miundo

**Tunga sentensi mbili kwa kila muundo.**

1. …………. ndani ya ……………….
   **Mfano:** Mdudu ameingia ndani ya shimo refu.
2. …………………. juu ya ……………
   **Mfano:** Juma ameweka kitabu juu ya meza.
3. ………………… chini ya ……………
   **Mfano:** Mwadawaameficha kikombe chini ya kitanda.
4. ……………….. katikati ya ……………….
   **Mfano:** Ng'ombe amesimama katikati ya mbuzi na mbwa.
5. …………………. mbele ya ………………..
   **Mfano:** Kulwa anaigiza mbele ya wanafunzi wenzake.

## Zoezi la 5: Mazoezi ya lugha

**A. Andika umoja au wingi wa maneno yafuatayo:**

| Na. | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| (i) | mgeni | ______________ |
| (ii) | kicheko | ______________ |
| (iii) | risala | ______________ |
| (iv) | ______________ | viwanda |
| (v) | shairi | ______________ |
| (vi) | ______________ | vyandarua |
| (vii) | somo | ______________ |
| (viii) | ______________ | shule |
| (ix) | ______________ | mazingira |
| (x) | ______________ | vikundi |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**B. Andika kinyume cha maneno yafuatayo:**

**Mfano:** mwanafunzi - *mwalimu*

(i) mgeni ______________
(ii) ghali ______________
(iii) haki ______________
(iv) zuia ______________
(v) chelewa ______________
(vi) halali ______________
(vii) kijana ______________
(viii) mjinga ______________
(ix) kiangazi ______________
(x) kale ______________

**C. Andika sentensi zifuatazo katika wakati ujao.**

**Mfano:** Mwalimu Sikujua anafundisha Shule ya Msingi Kahama.
*Mwalimu Sikujua atafundisha Shule ya Msingi Kahama.*

(i) Tuko tayari kupigania haki zetu.
(ii) Afisa Maendeleo wa Wilaya aliwapa wanafunzi zawadi.
(iii) Wanafunzi wote waliangua kicheko.
(iv) Chausiku anauliza swali darasani.
(v) Mwalimu amewatangazia wanafunzi Siku ya Mtoto wa Afrika.
(vi) Vikundi vya ngoma vinaburudisha wanafunzi.
(vii) Nyamate alimwamsha Upendo ili aende shuleni.
(viii) Mgeni rasmi alitangaza kutoa zawadi.
(ix) Mkulima amekwenda shambani.
(x) Watoto waliimba nyimbo nzuri sana.

**D. Kanusha sentensi zifuatazo:**

**Mfano:** Magesa atakuwa mwanafunzi mtoro.
*Magesa hatakuwa mwanafunzi mtoro.*

(i) Mwalimu Sikujua alikwenda mjini kutembea.
(ii) Lushinge alimfukuza Upendo darasani.
(iii) Walimu waliwagawia wanafunzi vitabu vya kujisomea.
(iv) Upendo alikubali kwenda kuchunga ng'ombe.
(v) Maktaba ni sehemu ya kutibia wagonjwa.
(vi) Luhumbika ameimba shairi.
(vii) Mgeni rasmi atafika kesho asubuhi.
(viii) Wanafunzi watashiriki katika Maadhimisho ya Sikukuu ya Uhuru.
(ix) Mimi ninasoma kitabu cha hadithi.
(x) Mwalimu wetu ni mgonjwa.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 44 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**E. Tunga sentensi sahihi kumi (10) kutokana na jedwali lifuatalo:**

**Mfano:** *Mwalimu wetu alikuwa anahutubia.*

| | | |
|---|---|---|
| Wazazi<br>Mwalimu wetu<br>Wacheza ngoma<br>Mwanafunzi | alikuwa<br>walikuwa | anahutubia<br>anafundisha kusoma<br>wanasoma vitabu<br>wanawatumbuiza wanafunzi<br>wanacheza mpira<br>anaimba shairi<br>anampongeza mwanafunzi<br>anasoma gazeti<br>analima shambani<br>anatoa huduma ya kwanza<br>wanakula chakula |

**F. Badili sentensi zifuatazo ziwe katika kauli ya kutendwa.**

**Mfano:** Mama amepika chakula**.**
*Chakula kimepikwa na mama.*

(i) Mwalimu anafundisha wanafunzi.
(ii) Baba yangu anasoma kitabu.
(iii) Dada alifungua mlango.
(iv) Manyama amechana kitabu changu.
(v) Dereva ataendesha basi la shule.
(vi) Mzee Salimu aliwasalimia wageni.
(vii) Mafuru alikuwa anapalilia bustani.
(viii) Babu yetu anauza mayai mengi.
(ix) Zawadi amesoma vitabu vichache.
(x) Fundi ametengeneza mlango wa nyumba yetu.

## Zoezi la 6: Kazi ya kufanya

**Andika nahau kumi (10) unazozifahamu, kisha eleza taswira zilizomo katika nahau hizo.**

## Zoezi la 7: Utungaji

**Malizia hadithi hii kwa maneno yasiyopungua tisini (90). Tumia nahau zifuatazo: piga mbio, gonga mwamba na kubali kwa shingo upande.**

Chui alikuwa anamdai Tembo chakula chake alichomkopesha. Tembo alikuwa anampiga kalenda Chui. Siku moja, uliitishwa mkutano wa wanyama. Wanyama wote walialikwa wakiwamo Tembo na Chui. Tembo alipomwona chui anakaribia mkutanoni …



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 45 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Sita

## Ziara

### Utangulizi

*Katika sura hii, utasoma habari inayohusu ziara ya kitaaluma katika Shule ya Msingi Matomondo. Pia, utaweza kusimulia mambo uliyoyaona katika ziara hiyo. Maarifa utakayoyapata yatakusaidia kujifunza mambo mbalimbali.*

### Fikiri



1. Je, umewahi kutembelea mahali popote?
2. Mambo gani uliyoyaona huko?
3. Je, ulijisikiaje wakati wa matembezi hayo? Kwa nini?

### Ufahamu

*Soma habari ifuatayo kisha, jibu maswali yanayofuata.*

**Ziara ya kitaaluma katika Shule ya Msingi Matomondo**

Mwalimu Matokeo ni mwalimu wetu wa somo la Kiswahili katika Shule ya Msingi Miti Mirefu. Anafundisha somo hili Darasa la Sita. Pia, ni mtaalamu wa somo la Kiingereza pamoja na Stadi za Kazi. Alihamia katika shule yetu mwaka jana. Mwalimu wetu anatupenda sana na ni mkarimu.

Mwalimu Matokeo alipohamia katika shule yetu, alikuta shule inafanya vibaya katika matokeo ya mitihani ya Darasa la Saba. Siku moja, Mwalimu Matokeo alimuuliza Mwalimu Mkuu, "Kwa nini matokeo ya Darasa la Saba si mazuri katika shule hii?" Mwalimu Mkuu alimweleza Mwalimu Matokeo mambo kadhaa yanayosababisha ufaulu kuwa mbaya. Hivyo, walishauriana waandae ziara kwa wanafunzi wa Darasa la Sita ili kuwajenga zaidi kitaaluma. Ndipo Mwalimu Matokeo alipotuandalia ziara ya kitaaluma katika Shule ya Msingi Matomondo. Lengo lilikuwa kutaka kujifunza kwa nini ufaulu wa shule hiyo uko juu kila mwaka. Kwa hiyo, Mwalimu Matokeo aliandika barua kwenda Shule ya Msingi Matomondo. Hatimaye, alikubaliwa twende kufanya ziara siku ya Ijumaa. Walimu na wanafunzi, kwa pamoja, wali**ahidi** kutupatia **ushirikiano.** Tulifurahi sana. Mwalimu Matokeo alitu**kumbusha** kufua na kupiga pasi nguo zetu ili siku ya ziara tuwe **nadhifu**.




KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 46 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kesho yake, Mwalimu Matokeo alituambia tuandae maswali ya kuuliza siku ya ziara. Mimi nilitaka kujua sababu za ufaulu wa mitihani ya Darasa la Saba kuwa juu kila mwaka katika shule hiyo. Wanafunzi wengine waliandaa maswali mengine pia.

Siku ya ziara, wanafunzi wote wa Darasa la Sita tuliwahi kufika shuleni. Mwalimu Matokeo alitupatia maelekezo kabla ya ku**zuru** Shule ya Msingi Matomondo.
Mwalimu Matokeo alituongoza kuelekea Shule ya Msingi Matomondo. Tulitembea kwa miguu tukiwa na mwalimu wetu. Punde si punde, tulifika Shule ya Msingi Matomondo. Tulikaribishwa na kupokelewa na wanafunzi na walimu. Walituonesha **ukarimu** wa hali ya juu. Kengele iligongwa na wanafunzi walikusanyika mstarini. Tulitambulishwa kwa walimu na wanafunzi. Mwalimu Mkuu aliwaeleza wanafunzi kuwa ziara yetu ilikuwa ya kitaaluma.

Baada ya hapo, mwalimu wa taaluma aitwaye Mangala alitupeleka mahali palipokuwa na takwimu za ufaulu. Alituonesha takwimu za ufaulu wa mitihani ya Darasa la Saba kwa miaka mitano mfululizo. Ufaulu ulikuwa wa juu sana.  Kila mwaka wanafunzi wengi walifaulu mitihani yao na kwenda kujiunga na elimu ya sekondari.






KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 47 26/07/2021 16:26
FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Nilimuuliza mwalimu wa taaluma, "Kwa nini katika shule yenu ufaulu wa mitihani ya Darasa la Saba uko juu kila mwaka?" Alijibu, "Sisi tuna vitabu vingi sana. Pia, walimu tunafundisha kwa bidii na wanafunzi wetu wanasoma kwa bidii." Aliongezea, "**Nidhamu** ni msingi wa **maendeleo** ya kitaaluma kwa mwanafunzi." Wanafunzi wetu wana nidhamu ya hali ya juu." Wanafunzi wengine waliuliza maswali mbalimbali na kujibiwa.

Baada ya maswali, mwalimu wa taaluma alitupeleka **maktaba**. Tulifika maktaba na kuona vitabu vingi sana. Maktaba hiyo ilikuwa na vitabu vingi vya masomo mbalimbali na hadithi. Alisema, "Wanafunzi wetu wana ratiba ya kuja maktaba kujisomea. Maktaba ni hazina ya **maarifa**." Tulipata nafasi ya kumuuliza maswali na kuangalia baadhi ya vitabu. Tulimshukuru mwalimu wa maktaba kwa majibu  na maelezo mazuri.

Ilipofika saa saba mchana, mwalimu wa maktaba alitupeleka kwenye **bwalo** la chakula. Tulikula pamoja na wanafunzi wa Shule ya Msingi Matomondo. Tulipomaliza kula, mwalimu wetu alienda katika Ofisi ya Mwalimu Mkuu kushukuru na kuaga. Kengele iligongwa tena na wanafunzi walikusanyika mstarini. Nasi tulijongea mpaka eneo walilokusanyika wanafunzi wenyeji ili tushukuru na kuaga. Tuliwashukuru walimu na wanafunzi kwa ukarimu wao na ushirikiano waliouonesha kwetu. Tuliagana na wenyeji wetu na kurudi shuleni. Tulifika shuleni salama tukiwa tumejifunza mambo mengi katika ziara hiyo.

Kesho yake asubuhi, Mwalimu Matokeo alipokuja darasani, alituuliza maswali kuhusu ziara yetu. Tuliyajibu vizuri maswali hayo. Mwalimu wetu alifurahi sana. Aliahidi kushirikiana na uongozi wa shule kututengenezea maktaba. Nasi tuliahidi kusoma kwa bidii ili tufaulu.

## Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Mwalimu Matokeo anafundisha somo gani?
2. Lengo la Mwalimu Matokeo kuandika barua lilikuwa nini?
3. Wanafunzi walifurahia nini?
4. Mwalimu wa taaluma wa Shule ya Msingi Matomondo anaitwa nani?
5. Kwa nini ufaulu wa mitihani ya Darasa la Saba uko juu katika Shule ya Msingi Matomondo?
6. Wanafunzi waliona nini kwenye maktaba ya Shule ya Msingi Matomondo?

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 48 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

7. Wanafunzi walipelekwa wapi ili kula chakula?
8. Kwa nini wanafunzi waliwashukuru walimu na wanafunzi wenyeji?
9. Habari hii inahusu nini?
10. Eleza mambo muhimu ya kuzingatia unapofanya ziara.

## Zoezi la pili: Msamiati

### Oanisha maneno ya safu A na maana zake katika safu B

**Mfano:** *(ii) ushirikiano – (d) hali ya kuungana na kusaidiana katika jambo*

| Safu A | Safu B |
|---|---|
| (i) ahidi | (a) ukumbi maalumu wa kulia chakula |
| (ii) ushirikiano | (b) enye kupendeza au kuwa safi |
| (iii) kumbusha | (c) weka dhamira ya kutekeleza jambo fulani |
| (iv) nadhifu | (d) hali ya kuungana na kusaidiana katika jambo |
| (v) zuru | (e) hali ya mtu kuwa mwema |
| (vi) ukarimu | (f) elimu au ujuzi aupatao mtu kutokana na kusoma, kusikia au kutenda |
| (vii) nidhamu | (g) fanya mtu afanye jambo fulani alilolisahau |
| (viii) maendeleo | (h) kupiga hatua kutoka hali duni kwenda hali bora zaidi katika nyanja za kiuchumi, kisiasa na kijamii |
| (ix) maktaba | (i) tabia njema aliyo nayo mtu katika jamii anayoishi |
| (x) maarifa | (j) nyumba au chumba mnamohifadhiwa machapisho ambayo watu huruhusiwa kuyatumia au kuyaazima kwa muda |
| (xi) bwalo | (k) enda mahali fulani kwa madhumuni ya kutembea na kujifunza jambo au kuonana na mtu |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 3: Vitendawili

**Tegua vitendawili vifuatavyo kwa kuandika jibu lako kwenye nafasi zilizoachwa wazi.**

1. Ziwa kubwa, lakini naogelea ukingoni tu ……………..
2. Ninapompiga mwanangu, watu hucheza ……………..
3. Ajenga nyumba ingawa hana mikono ……………..
4. Nina mtoto wangu, nikimpa chakula analia, nikimnyima chakula halii ……………..
5. Nikicheka, kinacheka, nikinuna, kinanuna ……………..
6. Mvua hema na jua hema ……………..
7. Nikienda kwenye ndege wanifukuza nikienda kwenye wanyama hawanitaki ……………..
8. Mdogo, lakini humaliza gogo ……………..
9. Namlalia, lakini halii ……………..
10. Nanywa supu na nyama naitupa ……………..

## Zoezi la 4: Methali

**Kamilisha methali zifuatazo:**

**Mfano:** Mpanda ngazi, hushuka.

1. ……………………….., furaha ya kunguru.
2. Usimwage mtama, ……………………….
3. Ukitaka kuruka, …………………………….
4. ………………………..., yakuwashia nini?
5. Mpiga ngumi ukuta, ………………………..
6. ……………………., mpaka siku ya Idi.
7. …………………….., lisingoje kesho.

## Zoezi la 5: Miundo

**Tunga sentensi mbili kwa kila muundo.**

1. ……………….. tangu ………………..
   **Mfano:** Magembe ni mgonjwa tangu mwaka jana.
2. ………………….. muda si mrefu.
   **Mfano:** Mgeni amefika muda si mrefu.
3. ………………….. mpaka sasa.
   **Mfano:** Doto ni mkulima mpaka sasa.



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

4. ………………… kuliko ……………..
**Mfano:** Tembo ni mkubwa kuliko sungura.

## Zoezi la 6: Mazoezi ya lugha

**A. Pigia mstari neno ambalo ni tofauti na mengine katika orodha ifuatayo:**

**Mfano:** kiti, meza, chakula, dawati, sofa

(i) ghasia, fujo, vurugu, vurumai, muziki
(ii) kuona, kusikia, kunusa, kuonja, kupima
(iii) gari, treni, basi, pikipiki, ndege
(iv) chaki, kitabu, mwanafunzi, kalamu, daftari
(v) ndizi, papai, fenesi, nazi, embe
(vi) papa, kambare, sangara, perege
(vii) simba, tembo, pundamilia, faru, ng'ombe
(viii) piga, cheza, cheka, lima, somo
(ix) simu, gazeti, kikokotozi, televisheni, redio
(x) bangili, soksi, hereni, mkufu

**B. Andika wingi wa sentensi zifuatazo:**

**Mfano:** Mwalimu wangu anafuata ratiba.
*Walimu wetu wanafuata ratiba.*

(i) Mpishi anapika chakula cha mgeni.
(ii) Nimeandika barua ya kirafiki.
(iii) Mwanafunzi alisoma kitabu cha hadithi.
(iv) Mwanakijiji amejenga darasa la kusomea.
(v) Daktari atakuwa anamtibu mgonjwa.
(vi) Mfanyakazi alikuwa anadai mshahara wake.
(vii) Nilimuuliza mwalimu kuhusu ufaulu.
(viii) Mwalimu aliniandalia ziara.
(ix) Shule itafunguliwa kesho asubuhi.
(x) Mimi ninapenda kusoma gazeti.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 51 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**C. Jaza chemshabongo ifuatayo kwa kuandika herufi moja tu kwa kila kisanduku. Zingatia maelezo ya kwenda chini na kulia.**

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 F | 2 U | 3 J | 4 O | | | | | 5 |
| 6 | | | | | | 7 | 8 | |
| 9 | | | | | | 10 | | |
| | | | | | 11 | | | |
| | | 12 | 13 | | | | | |
| 14 | 15 | | | | | | | |
| | 16 | | | | | | | |
| | | | | | | | | |

**Kwenda kulia**

**Mfano:** 1. Hali ya kuwa na ghasia. (herufi 4) – *FUJO*

6. Changanya unga maji na vitu vyenye uchachu ili ufure. (herufi 4)
7. Agizo la mdomo au la kuandika kutaka vitu au huduma fulani kwa malipo. (herufi 3)
9. Ugonjwa wa ngozi uwekao mabaka yawashayo mwilini. (herufi 3)
10. Safisha nguo kwa mashine au mikono ukitumia maji na sabuni. (herufi 3)
11. Keti mahali fulani. (herufi 3)
12. Pasha mwili joto, chipuka kutoka ardhini au mwilini na ona mambo usingizini. (herufi 3)
14. Kufanya jambo kwa mara ya kwanza. (herufi 4)
16. Kujifungua au kupata mtoto. (herufi 3)

**Kwenda chini**

1. Tegua au weka wazi fumbo fulani. (herufi 6)
2. Tengeneza kitu kwa kufinyanga. (herufi 4)
3. Elewa au kuwa na maarifa ya jambo fulani au nyota kubwa inayotoa mwanga na joto. (herufi 3)
4. Fanya harusi. (herufi 2)

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

5. Chombo tunachotumia kuangalia muda. (herufi 3)
7. Punguzo la gharama au bei ya bidhaa au huduma, ulipaji wa vyakula au vinywaji wanavyokunywa wengine. (Herufi 3)
8. Maombi maalumu ambayo huelekezwa kwa Mwenyezi Mungu. (herufi 3)
12. Haribika na kutoa harufu mbaya. (herufi 3)
13. Chombo kinachowashwa na kutoa mwangaza ili kumulika. (herufi 3)
15. Mdudu anayepatikana mahali penye uchafu au kinyesi na kueneza magonjwa. (herufi 3)

### D. Oanisha maneno yanayokaribiana kimaana kutoka safu A na safu B.

**Mfano:** (i) abiria (f) *msafiri*

| Safu A | Safu B |
|---|---|
| (i) abiria | (a) mateso |
| (ii) siha | (b) aibu |
| (iii) adhabu | (c) nafuu |
| (iv) bakora | (d) shukurani |
| (v) asante | (e) afya |
| (vi) fedheha | (f) msafiri |
| (vii) dhiki | (g) maradhi |
| (viii) maringo | (h) dhahiri |
| (ix) magonjwa | (i) fimbo |
| (x) uzembe | (j) uvivu |
| (xi) bayana | (k) madaha |
| (xii) faragha | (l) katili |
| (xiii) jela | (m) siri |
| (xiv) ahueni | (n) gereza |
| (xv) ajuza | (o) kikongwe |
| (xvi) dhalimu | (p) shida |

### E. Andika kinyume cha maneno yafuatayo:

**Mfano:** kumbuka – *sahau*

(i) ezeka
(ii) kusanya
(iii) chomeka
(iv) injika
(v) msichana
(vi) vita
(vii) shibe
(viii) chungu
(ix) funika
(x) anika

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**F. Kanusha sentensi zifuatazo:**

**Mfano:** Walimu wetu ni wakali sana.
*Walimu wetu si wakali sana.*

(i) Sisi tulifanya ziara shule ya jirani.
(ii) Shule yetu ina maktaba kubwa.
(iii) Wanafunzi wanasoma vitabu.
(iv) Magafu na Minza wanajadiliana kuhusu umuhimu wa maktaba.
(v) Mwanafunzi ataandika barua ya kuomba ruhusa.
(vi) Shule ya Msingi Miti Mirefu ina matokeo mazuri.
(vii) Ameuliza swali darasani.
(viii) Mama amenikumbusha kufua nguo zangu.
(ix) Wamesoma vitabu vya hadithi.
(x) Mwalimu amefundisha Kiswahili.

## Zoezi la 7: Kazi ya kufanya

**(i) Fanya ziara shule ya jirani. Andika kwa kifupi mambo uliyojifunza katika ziara hiyo.**

**(ii) Jadiliana na wanafunzi wenzako kuhusu mambo uliyojifunza katika ziara hiyo. Andika kwa kifupi mambo mliyojadiliana.**

## Zoezi la 8: Utungaji

**Tunga habari yenye maneno themanini (80) hadi mia moja (100) kuhusu ziara yoyote ambayo umewahi kuifanya. Habari hiyo ioneshe ziara ilihusu nini.**

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 54 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Saba

## Mawasiliano ya simu

### Utangulizi

*Katika sura hii, utajifunza umuhimu wa simu katika mawasiliano. Pia, utajifunza maadili bora katika kufanya mawasiliano kwa njia ya simu. Maarifa haya yatakusaidia kuandika ujumbe mfupi wa simu na kuutuma kwa jamaa au rafiki zako.*

### Fikiri



1. Je, umewahi kuona simu?
2. Je, umewahi kuwasiliana kwa njia ya simu?

### Ufahamu

*Soma mdahalo ufuatao, kisha jibu maswali yanayofuata.*

**Mada: Umuhimu wa matumizi ya simu katika jamii**

**Mwenyekiti:** Karibuni katika mdahalo wetu wa leo wenye mada inayosema, "Umuhimu wa matumizi ya **simu** katika jamii." **Mdahalo** huu utakuwa na wachangiaji wa pande mbili zinazokinzana. Wapo wanaosema kuwa matumizi ya simu ni muhimu. Hao wataeleza sababu za madai yao. Wengine wanasema, matumizi ya simu si muhimu. Hao nao wataeleza hasara za matumizi ya simu. Upande unaokubali ninaupa jina la *ndiyo* na upande unaopinga utaitwa *hapana*. Karibuni tusikilize **hoja** mbalimbali kutoka pande hizo mbili na tujifunze faida na hasara za matumizi ya simu.


Kwa kuanza, ninawakaribisha upande wa *ndiyo* tusikilize mawazo yao. Karibuni!

**Ndiyo:** Asante mwenyekiti. Mimi ninakubali kuwa matumizi ya simu ni muhimu sana kwani hurahisisha mawasiliano. Simu husaidia watu wa sehemu mbalimbali kuwasiliana ndani ya muda mfupi sana. Ni tofauti kabisa na zamani, ambapo ilikuwa vigumu sana kuwasiliana na watu, hasa walio mbali. Kwa kutumia simu, **mawasiliano** yamekuwa rahisi na watu wanaweza kutumiana ujumbe kwa muda mfupi na ukasambaa sehemu nyingi duniani.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Pia, matumizi ya simu hukuza uhusiano miongoni mwa watumiaji. Uhusiano huo huweza kuwa baina ya mtu na mtu, kikundi na kikundi, jamii na jamii. Vilevile, simu hukuza uhusiano wa kimataifa kupitia kupashana habari za kimataifa.



**Mwenyekiti:** Asante sana upande wa *ndiyo*! Wao wanasema kwamba simu ni muhimu kwa sababu hurahisisha mawasiliano na kukuza uhusiano baina ya watumiaji. Karibuni upande wa *hapana*.

**Hapana:** Asante mwenyekiti, matumizi ya simu yana hasara nyingi ikiwemo, kupoteza muda wa kufanya kazi. Hii hutokea, hasa maofisini pale wafanyakazi wanapotumia muda mwingi kusogoa na kuangalia video katika simu, na hivyo, kusahau kazi zao. Pia, nyumbani watu hupoteza muda mwingi kutumia simu badala ya kufanya kazi. Hali hii husababisha utendaji kazi mbovu.

Pia, matumizi mabaya ya simu husababisha mmomonyoko wa maadili hasa kwa watoto na vijana. Watoto na vijana wanaharibika kitabia



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 56 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kupitia matumizi ya simu, hasa kwa kuangalia **programu** hatarishi zilizowekwa au zinazotumwa **mitandao**ni. Programu hizo ni kama vile picha na video mbaya. Vijana na watoto hutumia simu kuangalia programu hizo ambazo ni kinyume cha maadili. Hivyo, huiga wanachokiona ikiwa ni pamoja na uvaaji na matendo mengine mabaya. Kwa kufanya hivyo, maadili ya watoto na vijana humomonyoka.

**Mwenyekiti:** Asante sana upande wa *hapana*! Karibuni tena upande wa *ndiyo*.

**Ndiyo:** Asante sana mwenyekiti. Mimi ninapenda kusisitiza kuwa matumizi ya simu bado ni muhimu sana kwani simu husaidia katika kujipatia elimu na kukuza ujuzi. Kupitia programu za simu, video, ujumbe, makala, na vitabu vinavyoweza kupakuliwa mitandaoni, wanafunzi na wanazuoni, hujipatia elimu, na hivyo, kukuza ujuzi na uelewa wao. Watoto pia huweza kujifunza kusoma na kuandika kupitia simu kwa kutumia programu hizo.

Pia, kibiashara, simu husaidia kutangaza na kufanya biashara mitandaoni. Wafanyabiashara hutangaza biashara zao ili kukuza soko la bidhaa zao kupitia mitandao ya kijamii.

**Mwenyekiti:** Asante sana upande wa *ndiyo*! Karibuni tena upande wa *hapana*.

**Hapana**: Ndugu mwenyekiti, nasi tunaendelea kusisitiza kuwa simu zina hasara nyingi. Matumizi ya simu yaliyokithiri, huweza kusababisha magonjwa katika miili ya binadamu kama vile maumivu na kuharibika kwa macho kutokana na miale ya umeme inayotokana na mwanga wa simu. Aidha, kuongea na simu kwa muda mrefu kunaweza kusababisha maumivu na kuharibika kwa uwezo wa masikio kusikia vema. Pia, matumizi ya simu huweza kusababisha ajali. Hii hutokea pale madereva wanapotumia simu za mikononi wakiwa wanaendesha vyombo vya usafiri kama vile magari na pikipiki. Vilevile, watembea kwa miguu huweza kupata au kusababisha ajali barabarani wakiwa wanatumia simu njiani pasi na kuangalia nini kinakuja mbele yao.

Matumizi ya simu pia ni ghali sana. Kwanza kabisa, ni gharama kununua simu yenyewe kwani baadhi ya simu hasa simumtelezo ni ghali sana. Pia, simu inahitaji kuwekwa fedha kila mtumiaji anapotaka kuwasiliana au kupakua taarifa fulani mtandaoni.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 57 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Mwenyekiti:** Asante sana upande wa *hapana*! Tunazidi kupata hoja nyingi zinazotuelimisha kuhusu hasara za matumizi ya simu. Kwa sasa, ninakaribisha upande wa *ndiyo*. Karibuni!

**Ndiyo:** Mwenyekiti, faida za matumizi ya simu zipo nyingi! Labda niwaambie tu wasiojua, kwamba matumizi ya simu husaidia katika utunzaji wa kumbukumbu. Simu hutunza kumbukumbu za mambo au matukio mbalimbali kama vile ya kibiashara, kisiasa, na hata kielimu. Vilevile, wasomi, wanafunzi na wanazuoni huweza kutunza makala na vitabu vyao kwenye simu.

Matumizi ya simu huburudisha na kutuliza akili pale mtu anapokuwa amechoka. Kupitia programu zilizopo kwenye simu kama vile muziki, video na michezo, picha na hata ujumbe wa kuchekesha unaosambazwa kupitia simu, mtu anaweza pata faraja za maisha.

**Mwenyekiti:** Asante upande wa *ndiyo*! Karibu upande wa *hapana* mwendelee kutoa hoja.

**Hapana:** Asante mwenyekiti! Matumizi ya simu hupunguza uwezo wa kufikiri. Mazoea yaliyokithiri ya kutumia simu hupunguza uwezo wa kufikiri wa watumiaji, hasa wanafunzi. Hali hii inadhihirika pale ambapo wanafunzi hutumia simu zao kutafuta majibu ya maswali rahisi ambayo wangeweza kuyajibu pasipo kutumia simu.

**Mwenyekiti:** Shukurani sana upande wa *hapana* kwa kuzidi kutuelimisha juu ya hasara za matumizi ya simu. Sasa mnakaribishwa upande wa *ndiyo*, mzidi kutuelimisha juu ya umuhimu wa matumizi ya simu.

**Ndiyo:** Matumizi ya simu, ndugu mwenyekiti, kwanza, huleta ajira kwa wauzaji wa simu, vocha na vifaa vingine vinavyohusiana na simu. Pili, watu wanaajiriwa katika maduka ya kuuza simu na **laini** za simu. Tatu, vijana wanajiajiri kama mafundi wa simu.

Pia, matumizi ya simu hurahisisha huduma za kibenki, yaani watu huweza kutuma, kutoa na kuhifadhi pesa kwenye simu. Matumizi ya simu pia husaidia sana kukuza pato la nchi yetu kupitia ulipaji kodi. Watoa huduma mbalimbali zinazohusiana na matumizi ya simu kama wauzaji wa simu, wauzaji wa **vocha** na biashara zote zinazohusiana na simu, wanalipa kodi kwa nchi yetu.

**Mwenyekiti:** Asante sana kwa mawazo mazuri kutoka upande wa *ndiyo*. Karibu upande wa *hapana* tumalize nanyi.

**Hapana:** Matumizi ya simu yanaharibu **utamaduni** wa watu katika mataifa mbalimbali kupitia kuiga tamaduni za mataifa mengine



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 58 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

zinazosambazwa kupitia mtandao wa intaneti. Hivyo, tamaduni za nchi nyingi zimeharibiwa kwa kuiga tamaduni za kigeni kupitia matumizi ya simu.

Pia, matumizi ya simu husababisha kusambaa kwa uzushi ambao husababisha ugomvi na kuvunjika kwa mahusiano katika ngazi ya familia, jamii na taifa kwa ujumla.

Kupitia matumizi ya simu, watu huweza kupanga matukio ya uhalifu. Hivyo, simu huleta hasara na kuondoa amani katika eneo fulani au nchi fulani.

Zaidi ya hayo, matumizi ya simu pia yanaua uhai wa mahusiano na ushirikiano baina ya watu. Kwa mfano, zamani watu walitembeleana ili kufikishiana **habari**, kujuliana hali na kushirikiana vizuri, lakini sasa watu wamepunguza kutembeleana ila wanawasiliana na kuonana kupitia picha tu kwenye simu. Pia, baadhi ya wazazi wanakosa muda wa kuonesha upendo kwa familia wanapokuwa nyumbani na kujikuta muda mwingi wanatumia simu. Hivyo, matumizi ya simu yana hasara zaidi kuliko faida zake.

**Mwenyekiti:** Asanteni sana nyote kwa mawazo yenu mazuri juu ya matumizi ya simu. Kupitia mawazo hayo tumejifunza kuwa, matumizi ya simu ni muhimu sana hasa katika zama hizi za sayansi na **teknolojia**. Hata hivyo, matumizi mabaya ya simu husababisha hasara nyingi kama tulivyosikia kutoka upande wa *hapana.* Hivyo, tuzingatie matumizi sahihi ya simu ili kuepuka hasara hizo. Asanteni nyote.

## Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Mdahalo uliosoma unahusu nini?
2. Mdahalo huo ulikuwa na pande ngapi? Zitaje.
3. Taja faida za simu kama zilivyotajwa kwenye mdahalo uliousoma.
4. Taja kiongozi wa mdahalo.
5. Taja hasara za simu kama zilivyotajwa kwenye mdahalo uliousoma.
6. Upande gani ulioeleza madhara ya matumizi ya simu?
7. Kama ungepata nafasi ya kushiriki katika mdahalo huo, ungechangia upande gani? Kwa nini?
8. Umejifunza nini kutokana na mdahalo uliousoma?

## Zoezi la pili: Msamiati

**Tunga sentensi mbili kwa kila neno kwa kutumia msamiati ufuatao:**

1. simu
2. mdahalo



FOR ONLINE USE ONLY

KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 59 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. hoja
4. mawasiliano
5. programu
6. mtandao
7. laini
8. vocha
9. utamaduni
10. habari
11. teknolojia

## Zoezi la 3: Miundo

**Soma miundo ifuatayo, kisha tunga sentensi tatu kwa kila muundo.**

1. …………………. ilimradi …………………..

   **Mfano:** *Mushi alikula chakula **ilimradi** tu amfurahishe baba yake.*
2. Vivyo hivyo, …………………………….

   **Mfano:** ***Vivyo hivyo,*** *kila atakayefika kwenye sherehe atakula na kunywa hadi atosheke.*
3. …………………… kimoyomoyo …………………..

   **Mfano:** *Mama alijisemea **kimoyomoyo** kuhusu matarajio ya mwanawe.*
4. ………………….. kimyakimya ……………………

   **Mfano:** *Wanafunzi wote walifanya mazoezi **kimyakimya** bila kelele.*
5. ……………………….. kinagaubaga ………………………

   **Mfano:** *Doni aliongea na Kulwa **kinagaubaga** kuhusu matumizi sahihi ya simu.*

## Zoezi la 4: Methali

**Malizia methali zifuatazo:**

1. Siku njema, ………………..
2. Hakuna msiba, …………………………
3. Kila ngoma, ……………………………..
4. Tabia hupamba, …………………
5. Cha mwerevu, ………………………………
6. …………………….. ni kichwa.
7. ……………………., mbele kina sumbuko.
8. Kijengacho mtu si jina, ……………………
9. ……………………, upate heshima.
10. Bora nusu yai, ……………………

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 5: Mazoezi ya lugha

**A. Pigia mstari neno lenye maana tofauti na mengine.**

(i) maharage, mtama, kunde, mbaazi
(ii) salio, shule, vocha, pesa
(iii) babaika, wasiwasi, dukuduku, kizunguzungu
(iv) juzi, jana, leo, mchana
(v) chumba, stoo, kitanda, sebule
(vi) wali, ubwabwa, pilau, mchele
(vii) kimyakimya, harakaharaka, kimoyomoyo, kisirisiri
(viii) mawimbi, upepo, kimbunga, giza
(ix) choma, bofya, gusa, bonyeza
(x) rukono, simujanja, nukushi, simutamba

**B. Andika neno moja linalojumuisha maneno uliyopewa.**

(i) ongea, zungumza, ujumbe, taarifa ______________
(ii) Ijumaa, Jumamosi, Jumapili, Jumatatu _____________
(iii) malaria, surua, kipindupindu, UKIMWI _______________
(iv) fundisha, somesha, elekeza, endesha __________________
(v) rukono, simujanja, simutamba, simumtelezo ________________
(vi) Hisabati, Kiswahili, Sayansi, Uraia _________________
(vii) punda, mbwa, ng'ombe, paka __________________
(viii) mchele, ngano, mtama, mahindi ______________
(ix) nanasi, papai, parachichi, chungwa ____________
(x) bata, njiwa, kunguru, kuku ________________

**C. Andika KWELI au SI KWELI.**

(i) Simu ni njia pekee ya mawasiliano. _________
(ii) Mzungumzaji na msikilizaji ni watu muhimu katika mawasiliano ya simu. _________
(iii) Simu hazina umuhimu wowote katika jamii. _________
(iv) Ujumbe wa maneno kwenye simu unapaswa kuwa mrefu sana. _________
(v) Simu inafanya mazungumzo kwa mtu aliye karibu tu. _________
(vi) Matumizi ya simu yana faida na hasara. _________
(vii) Simu inaweza kutumika kurekodi sauti. _________
(viii) Mwanafunzi mwema hufanya kazi bila kusimamiwa. _________
(ix) Simumtelezo kwa jina jingine huitwa simujanja. _________
(x) Simu ikitumika vibaya inaweza kusababisha migogoro. _________

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 61 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## D. Tunga sentensi sahihi kumi (10) kwa kutumia jedwali lifuatalo:

**Mfano:** *Baba yangu anamiliki simu ya mkononi.*

*Mjomba anauza kiwanja kilichoko kijijini.*

| | | |
|---|---|---|
| Baba yangu<br>Mjomba<br>Shangazi | anamiliki<br>anauza | simu ya mkononi<br>kiwanja kilichoko kijijini<br>baiskeli mbili nzuri<br>nyumba iliyojengwa kwa miti<br>duka la nguo lililosheheni vitambaa |

## E. Kanusha sentensi zifuatazo:

**Mfano: Tu**tatoka hapa saa sita - ***Ha**tutatoka hapa saa sita.*

(i) Sisi tuliimba wimbo wa shule …………………..
(ii) Ninakwenda kucheza …………………..
(iii) Jua lina faida moja tu kwa viumbe hai …………………..
(iv) Baba ana duka la simu …………………..
(v) Mdogo wangu ni mwanafunzi wa Darasa la Pili …………………..
(vi) Bahati atanunua simu …………………..
(vii) Watu walimiminika kwenye sherehe …………………..
(viii) Mwalimu wetu ana simu ndogo …………………..
(ix) Kaka anaitwa Bahati …………………..
(x) Kulwa anajua kupiga simu …………………..

## F. Andika sentensi zifuatazo katika wingi:

**Mfano:** Mwanafunzi anapenda kusoma kitabu chenye hadithi ya kuvutia na kusisimua.

*Wanafunzi wanapenda kusoma vitabu vyenye hadithi za kuvutia na kusisimua.*

(i) Ninasoma Shule ya Msingi Tumaini.
(ii) Mimi ni mzalendo kwelikweli.
(iii) Simu yangu imepotea leo asubuhi wakati ninachota maji.
(iv) Mwalimu ana simu kubwa yenye rangi nyeusi na nyeupe.
(v) Anaandika ujumbe mfupi wa simu.
(vi) Kaka yangu amenipigia simu.
(vii) Mtoto anajua kucheza mpira.
(viii) Kakakuona ni mnyama wa ajabu.
(ix) Ng'ombe amekamuliwa maziwa.
(x) Yeye atanunua tunda.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**G. Chagua neno sahihi kutoka kwenye mabano, kisha uliandike ili kujaza nafasi zilizoachwa wazi.**

**Mfano:** Mama anapenda ugali.
(anapenda, atapendwa, alipendwa)

(i) Mariamu __________ Kiswahili fasaha
(kanazungumza, kinazungumza, anazungumza).

(ii) Alipokuwa __________simu, alikutana na mjomba wake
(akiwaletea, atamletea, atawaletea).

(iii) Mke wake Rajabu_________ kupiga simu.
(kanajua, anajua, watajua)

(iv) Maharage _______chakula kitamu.
(ni, kama, ndimi)

(v) Ufupi ________ ugonjwa.
(kama, si, ndiyo)

(vi) Kaka __________ keshokutwa.
(alikuja, amekuja, atakuja)

(vii) Mwalimu wetu _________ vizuri sana.
(tunafundisha, anafundisha, wanafundisha)

(viii) Shambani __________ ngano.
(kumepanda, kumepandwa, pamepandia)

(ix) Doni _____ aliyepiga simu kwa shangazi yake.
(ndicho, ni, ndiye)

(x) Jana mwalimu _________ jinsi ya kupiga simu.
(alitufundisha, anajifundisha, amelifundisha)

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 63 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**H. Oanisha maneno ya safu A na safu B kwa kuandika maelezo ya safu B kwenye nafasi zilizoachwa wazi.**

**Mfano:** *Kimoyomoyo – kuongea na nafsi yako bila kutoa sauti.*

| Na. | Safu A | Safu B |
|---|---|---|
| (i) | Lugha ……… | Kifaa maalumu kitumikacho kuchapa na kuhifadhi kumbukumbu mbalimbali kwenye nakala laini. |
| (ii) | Taasisi ……. | Ujuzi mkubwa wa kufanya jambo fulani. |
| (iii) | Simu …….. | Chumba maalumu cha kupumzikia ndani ya nyumba. |
| (iv) | Mawaidha ……. | Sauti za kubuni na zenye maana zitumiwazo na binadamu katika mawasiliano. |
| (v) | Simujanja …………… | Kituo maalumu na rasmi kinachojihusisha na shughuli za kijamii au kiserikali. |
| (vi) | Teknolojia …………. | Kwa kuongea na nafsi yako bila kutoa sauti. |
| (vii) | Kompyuta …………… | Nasaha au mafunzo anayopewa mtu. |
| (viii) | Sebule ……………… | Simumtelezo. |
| (ix) | Umahiri ………… | Kiwango cha juu cha uvumbuzi wa kisayansi. |
| (x) | Kimoyomoyo ……… | Kifaa kitumiwacho na watu walioko kwenye maeneo tofauti kupashana habari papo kwa papo. |

## Zoezi la 6: Utungaji

**A. Andika ujumbe mfupi wa simu wenye maneno yasiyozidi kumi na matano (15) kuhusu mada ulizopewa.**

**Mfano:** Salamu kwa Baba

*Shikamoo Baba. Mimi mzima. Nimekuwa wa kwanza darasani. Bakari.*

(i) Kuomba ada ya shule kwa mzazi.

(ii) Kujua matokeo ya mechi kutoka kwa rafiki yako.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**B. Wewe umeandikiwa barua ifuatayo. Isome, kisha andika ujumbe mfupi wa simu kumshukuru mwalimu mkuu. Maneno yasizidi kumi na matano (15).**

Shule ya Msingi Tumaini,
S.L.P. 60,
Masasi,
Mtwara.

10/07/2018.

Kumb. Na. HWM/SMT/2018/021
Kabonza Digo,
Kijiji cha Kashule,
S.L.P. 60,
Masasi,
Mtwara.

Ndugu,

**YAH: KIBALI CHA RUHUSA YA KUUGUZA**

Kichwa cha habari chahusika.

Rejea barua yako ya tarehe 08/07/2018 inayohusu ombi la ruhusa ya kumuuguza mama yako. Ombi lako limekubaliwa. Umeruhusiwa kwa muda wa siku kumi na nne (14) kama ulivyoomba, kuanzia tarehe 09/07/2018 hadi 22/07/ 2018.

Ninakutakia kila la heri.

*A. Kaboko*
Amani Kaboko
Mwalimu Mkuu

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Nane

## Aina za maneno

### Utangulizi

*Katika sura hii, utajifunza aina nane za maneno ambazo ni nomino (N), kivumishi (V), kitenzi (T), kielezi (E), kiwakilishi (W), kiunganishi (U), kihusishi (H) na kihisishi (Hs) au kiingizi (I). Maarifa haya yatakuwezesha kutumia aina hizo za maneno ya lugha ya Kiswahili kwa ufasaha katika miktadha mbalimbali. Pia, utatumia vifupi vya aina hizo za maneno kubainisha maneno yanayounda sentensi mbalimbali.*

### Fikiri




Aina gani ya neno hujumuisha maneno yafuatayo?
1. Asha, Juma, Kigoma, Omari
2. kimbia, simama, tembea, rukaruka
3. mzuri, mbaya, mrefu, mfupi

### Ufahamu

*Tamba ngonjera ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

**Aina za maneno**



**Kaka:** Nauliza da' Aziza,
Mawazo yaniumiza,
Naomba kunieleza,
**Nomino** ni kitu gani?

**Dada:** Hebu kaka sikiliza,
Maneno ya kupendeza,
Majina ya kupendeza,
Ya viumbe na mahali.

**Kaka:** Siku nyingi nimewaza,
Sauti ninaipaza,
Majina ninayowaza,
Ndiyo yaitwa nomino?




KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 66 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Dada:** Sikiliza kaka Mesha,
Nataka kukukumbusha,
Kila jina nakupasha,
Ndilo huitwa nomino.




**Kaka:** Majina unayotaja,
Sijui yanavyokuja,
Kutambua nina haja,
Nomino ni kitu gani?

**Dada:** Majina ya kila kitu,
Mimea na hata vitu,
Wanyama hata misitu,
Majinaye ni nomino.

**Kaka:** Sasa nuru naiona,
Macho yangu yanaona,
Bado niulize tena,
**Kivumishi** ndicho nini?

**Dada:** Ni maneno yenye sifa,
Huzipa nomino sifa,
Ni wasifu wenye sifa,
Nomino kufafanua.

**Kaka:** Sifaze unazosema,
Ndizo zipi unasema,
Kuuliza sitakoma,
Kivumishi ndicho nini?




**Dada:** Kuna sifa za uzuri,
Hata pia uhodari,
Urefu hata kiburi,
Sifaze ni vivumishi.

**Kaka:** Dada yangu wanikuna,
Kwa maarifa ya kina,
Naomba nipe maana,
**Kitenzi** nacho ni nini?

**Dada:** Kila utendalo tendo,
Limefumbata kitendo,
Penda upate upendo,
Kitenzi hapo ni *penda.*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Kaka:** Dada yangu wanijuza,
Maarifa wanijaza,
Tena swali nauliza,
**Kielezi** nacho nini?

**Dada:** Tendo kinaliabiri,
Mfanowe tafakari,
Umeelewa vizuri,
Kielezi ni *vizuri.*


**Kaka:** Kiu bado yanikaba,
Haba hujaza kibaba,
Maarifa siyo haba,
**Kiwakilishi** ni nini?

**Dada:** Hicho ndicho kibadala,
Kwa nomino ni wakala,
Yeye huwa analala,
Kiwakilishi ni *yeye.*

**Kaka:** Aa! Aa! Nimecheka,
Maarifa nayataka,
Kujua bado nataka,
**Kihisishi** kitu gani?

**Dada:** Tehe! Tehe! Kaka yangu,
Watekenya roho yangu,
Natoa hisia zangu,
Kutumia kihisishi.

**Kaka:** Lo! Lo! Lo! Lo! Nauliza,
Mifano hujaeleza,
Hebu! Njoo na eleza,
Kihisishi ndio nini?



**Dada:** Vicheko tunavyotoa,
Mshangao ulotoa,
Hisia vinazitoa,
Vihisishi, viingizi.


**Kaka:** Dada umenipa nuru,
**Kihusishi** sasa zuru,
Nieleze naamuru,
Kihusishi ndiyo nini?

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 68 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Dada:** Kinahusisha maneno,
Hujalizwa na nomino,
Ninakula kwa mkono,
Neno *kwa* kihusishi.

**Kaka:** Hapa mwisho nimefika,
**Kiunganishi** nafika*,*
Hicho nini kinashika,
Kiunganishi ni nini?

**Dada:** Huunga neno kwa neno,
Kuleta mshikamano,
Baba na mama ni pendo,
Kiunganishi ndicho *na.*

**Kaka:** Aina zina vifupi?
Nieleze viko wapi?
Utaratibu ni upi?
Tena kwa maneno yapi?

**Dada:** **U** ni kwa kiunganishi,
**H** ndiyo kwa kihusishi,
**V** nayo kwa kivumishi,
Pia **W** kiwakilishi.

**N** nomino hueleza,
**T** tendo linadokeza,
**E** nayo kwa kielezi,
**Hs** ni kwa kihisishi.

**Wote:** Somo sasa limekwisha,
Kusoma siyo kukesha,
Wenzetu tutawapasha,
Maneno na ainaze.



FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 69 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Taja wahusika wawili wa ngonjera uliyoisoma?
2. Katika ngonjera uliyoisoma, nani alikuwa anauliza maswali?
3. Nani alikuwa anajibu maswali yote yaliyokuwa yanaulizwa?
4. Taja majina ya watambaji wa ngonjera hii.
5. V inasimama badala ya aina gani ya neno?
6. Umejifunza kuwa kiunganishi ni nini?
7. Kaka anasema majina anayowaza yanaitwaje?
8. Taja aina nane za maneno zilizofafanuliwa katika ngonjera hii.
9. Umejifunza nini kutokana na ngonjera uliyoisoma?

## Zoezi la pili: Msamiati

**Tunga sentensi moja kwa kutumia maneno yaliyomo katika aina za maneno zifuatazo:**

nomino, kivumishi, kielezi, kitenzi, kiwakilishi, kihisishi, kihusishi na kiunganishi

## Zoezi la 3: Mazoezi ya lugha

**A. Oanisha sehemu A na sehemu B ili kuleta maana.**

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| (i) nomino | (a) kisifa |
| (ii) kiwakilishi | (b) jina |
| (iii) kivumishi | (c) kiungo |
| (iv) kitenzi | (d) hufafanua kitenzi na kivumishi |
| (v) kielezi | (e) huonesha hisia |
| (vi) kihisishi | (f) mbadala wa nomino |
| (vii) kiunganishi | (g) huonesha uhusiano baina ya neno moja na neno au maneno mengine |
| (viii) kihusishi | (h) kitendo |

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 70 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**B. Jaza chemshabongo ifuatayo kwa kutumia maelekezo ya kwenda chini na kulia.**

| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | 2 | | 3 | | | 4 | | |
| | | | | | | | | | | | |
| 5 | | | | | | | | | | | |
| | | | 6 | | | | 7 | | | | 8 |
| | | | | | | | | | | | |
| | | 9 | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | |
| | | 10 | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | |
| | 11 | | | | | | | | | | |

**Kwenda kulia**

1. Kitendo (Herufi 7)
5. Toa samaki baharini, ziwani au mtoni (Herufi 3)
6. Panga katika aina mbalimbali (Herufi 7)
9. Kifaa kinachotumika kwa kujitazamia au kutengeneza gilasi au kitu kigumu kilicho angavu na hupitisha mwanga kilichotengenezwa na madini ya ulanga (Herufi 4)
10. Wasilisha au fikisha kitu mahali alipo anayehitaji (Herufi 4)
11. Neno linalokaa badala ya nomino (Herufi 11)

**Kwenda chini**

1. Hueleza nomino (Herufi 9)
2. Majina (Herufi 6)
3. Kuwa na uhai (Herufi 4)
4. Weka vitu kwa pamoja (Herufi 9)
7. Uzuri au ubaya wa kitu au mtu (Herufi 4)
8. Huonesha hisia (Herufi 9)
9. Hufafanua kitenzi (Herufi 7)

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**C. Bainisha nomino zilizotumika katika sentensi zifuatazo kwa kuzipigia mstari.**

**Mfano:** Ngoma ilipigwa usiku kucha.
Shangazi alinunua machungwa, mananasi na matango.

(i) Darasa lina wanafunzi wengi.
(ii) Asante sana Vumilia.
(iii) Bustani ina matunda mengi sana.
(iv) Dada anasoma kitabu chake.
(v) Maendeleo ni muhimu kijijini kwetu.
(vi) Alikula kwa sababu alikuwa na njaa.
(vii) Fundi amekuja na msumeno.
(viii) Amepoteza kalamu na rula.
(ix) Jeshi lao limeshinda vita.
(x) Babu yake ana huruma sana.

**D. Pigia mstari viwakilishi katika sentensi zifuatazo:**

**Mfano:** Mimi nitakwenda kumsaidia bibi kuvuna mtama.
Wote tulipiga makofi kumshangilia mgeni.

(i) Sisi hatuwajui wao.
(ii) Pale panafahamika sana.
(iii) Ninyi mnafanya nini hapa?
(iv) Wao walihudhuria mkutano ule.
(v) Yupi ameondoka?
(vi) Wawili waende wakachote maji.
(vii) Ambaye amemaliza aje.
(viii) Yale yameharibika sana.
(ix) Chake kimepotea.
(x) Wengine wakae hapa.

**E. Pigia mstari vivumishi katika sentensi zifuatazo:**

**Mfano:** Ndege mzuri alituburudisha kwa nyimbo zake.
Embe kubwa limeiva mtini.

(i) Vijana wengi wana tabia nzuri.
(ii) Panya mkubwa ameingia shimoni.
(iii) Kijiji chetu kina zahanati nzuri.
(iv) Amekula chakula chote.
(v) Yeye mwenyewe amefika.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 72 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(vi) Wanafunzi wengine watoke nje.
(vii) Mwanafunzi hodari amepata zawadi.
(viii) Maendeleo yetu yanakua kwa kasi.
(ix) Kanga wawili wameatamia.
(x) Mkutano huu umeitishwa na kiongozi wetu.

## F. Bainisha vitenzi katika sentensi zifuatazo kwa kuvipigia mstari.

**Mfano:** Dereva alimkwepa mlevi barabarani.
Tausi ni ndege mwenye maringo.

(i) Dada na kaka wanatamba ngonjera.
(ii) Kaka anamuuliza dada maswali.
(iii) Dada anamjibu kaka maswali.
(iv) Wezi walivunja duka letu.
(v) Popo si ndege.
(vi) Vijana wamebomoa ukuta wote.
(vii) Fundi alitaka kujenga ukuta huo.
(viii) Mvua ilinyesha usiku mzima.
(ix) Hii ndiyo nyumba yangu.
(x) Alicheza na kuimba vizuri.

## G. Pigia mstari vielezi katika sentensi zifuatazo:

**Mfano:** Mamba ameonekana mtoni.
Takataka zinatupwa jalalani.

(i) Maji yamejaa pomoni.
(ii) Kaa anakwenda upandeupande.
(iii) Pikipiki ilitumbukia bwawani taratibu.
(iv) Daktari atafika keshokutwa.
(v) Ataondoka mapema ili kuwahi usafiri.
(vi) Mwanafunzi anatembea polepole.
(vii) Walimpiga sana.
(viii) Alihesabu vizuri ili kupata jibu.
(ix) Humtembelea kila siku.
(x) Simba ananguruma sana.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 73 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**H. Jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kutumia vihisishi vifuatavyo:**

| La! Hasha! Lo! Ahaa! Aa! Aisee! Kumbe! Ebo! Uwii! |
|---|

**Mfano:** Uwii! Nimechelewa kuamka.
Aa! Hivi naye alikuwapo?

(i) ______ Sipendi uji.
(ii) ______ Nimejua faida zake.
(iii) ______ Ona mwizi yule.
(iv) ______ Wamefungwa jamani.
(v) ______ Ameumia mguu.

**I. Tumia vifupi kubainisha maneno katika sentensi zifuatazo:**

**Mfano:** Madawati yetu yametengenezwa vizuri.
N V T E

(i) Juma alinunua sabuni yake.
(ii) Katundu alijipaka mafuta mazuri.
(iii) Sote tunatunga sentensi sahihi.
(iv) Mmoja atakuja mapema.
(v) Aa! Wewe angalia usinase.
(vi) Sisi tulisikitika goli lile lilipoingia wavuni.
(vii) Mahakama yetu inatoa huduma bora.
(viii) Paka shume aliingia bandani kukamata kuku.
(ix) Aisee! Twende tukalale nimechoka.
(x) Uji ulimwagika mwaa!
(xi) Baba ndiye mwalimu mkuu.

## Zoezi la 4: Utungaji

**Tunga hadithi yoyote unayoipenda yenye maneno yasiyozidi mia moja ishirini (120), kisha pigia mstari nomino na vitenzi.**

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tisa

## Risala

### Utangulizi

*Katika sura hii, utajifunza kusoma na kuandika risala kwa kuzingatia muundo wake. Maarifa utakayoyapata, yatakusaidia kuandika na kusoma risala katika hafla mbalimbali.*

### Fikiri



1. Je, umewahi kusoma risala?
2. Risala hiyo ilihusu nini?
3. Nani aliandika risala hiyo?

### Ufahamu

*Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

**Mwenge wa Uhuru**

Hatimaye siku niliyokuwa nikiisubiri kwa hamu kubwa ili**wadia**! Hauchi hauchi, sasa umekucha! Siku hiyo niliamka asubuhi na mapema ili nijiandae kwenda shuleni. Ingawa nilipika **kifunguakinywa**, sikuweza hata kukila. Mawazo yangu yote yalikuwa kwenye ugeni mkubwa ambao unakuja shuleni kwetu, Shule ya Msingi Changanyikeni.

Ugeni wenyewe ulikuwa Mwenge wa Uhuru. Mwalimu Mkuu alitutangazia kuwa Mwenge wa Uhuru utafika na kusimama kwa muda shuleni kwetu. Pia, mgeni rasmi ataweka **jiwe la msingi** kwenye jengo la madarasa mapya. Mgeni Rasmi alikuwa kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa.

Nyumbani kwetu ni mbali na shuleni. Kwa hiyo, nilianza safari ya kuelekea shuleni mapema ili nisichelewe. Njiani kulikuwa na **shamrashamra** nyingi. Watu wengi walianza kujipanga **kandokando** ya barabara ili kuupokea Mwenge. Wote walikuwa na nyuso za furaha. Mikononi, walikuwa wameshika matawi ya miti na nguo zao wakizi**punga** hewani kuonesha furaha yao.

Nilikuwa na **shauku** kubwa ya kuuona Mwenge wa Uhuru. Maishani mwangu, sikuwahi kuuona. Nilikuwa nikisikia tu habari zake kwa watu mitaani au

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kuzisoma vitabuni. Mwalimu wetu alitufundisha kuwa Mwenge wa Uhuru hutangaza uhuru wetu, amani, uzalendo na kuhimiza watu kufanya shughuli za maendeleo katika nchi yetu. Leo nitapata **fursa** ya kuu**shuhudia** Mwenge wa Uhuru kwa macho yangu mwenyewe!

Nikiwa njiani, nilikutana na wanafunzi wenzangu nao wakienda shuleni. Nyuso zao zilikuwa za **bashasha**. Nao walikuwa na hamu ya kuuona mwenge kama mimi. Tuliongeza mwendo ili tufike shuleni mapema.

Tulipowasili shuleni, kengele iligongwa, tukaenda kujipanga mstarini. Walimu wote walikuwapo. Mwalimu Mkuu alituagiza tusafishe mazingira kama ilivyo ada. Pia, aliwaelekeza walimu na viranja kusimamia vizuri shughuli zote.

Tulipomaliza kufanya usafi, kengele iligongwa tena tukarejea mstarini. Mara hii, Mwalimu Mkuu alituarifu kuwa ule **wasaa** tuliousubiri kwa hamu, ulikuwa umekaribia. Alisema kuwa **msafara** wa Mwenge wa Uhuru ulikuwa karibu kufika shuleni kwetu. Tuliposikia hivyo, tulilipuka kwa shangwe!

Tuliambiwa tupange mstari pembezoni mwa barabara kuu inayoingia shuleni ili kuupokea ugeni huo mkubwa. Tulitawanyika chapuchapu na kwenda kujipanga kwa umaridadi. Hayawi hayawi, sasa yamekuwa! Tulianza kusikia kwa mbali mlio wa king'ora kilichoongoza msafara wa Mwenge. Loo! Kufumba na kufumbua, tukaona msururu mrefu wa magari ukija shuleni kwetu. Gari mojawapo la wazi lilikuwa limebeba Mwenge wa Uhuru. Mwenge ulikuwa unawaka. Rangi yake ilivutia sana machoni. Askari shupavu walikuwa kwenye gari hilo wakiulinda. Watu wengi tayari walikuwa wamejaa shuleni kwetu. Shangwe, nderemo, hoihoi na vifijo vilisikika kila kona vikiushangilia Mwenge. Wakati Mwenge unapita, sote tulipiga makofi na kuimba kwa sauti kuu:


*Mwenge wetu! Mwenge wetu! Tunakupongeza! x2*
*Utuletee amani, utuletee upendo!*
*Tuletee matumaini na maendeleo ya kweli x2*
*Mwenge! Mwenge wetu!*
*Palipo na dharau x6*
*Mwenge! Mwenge mama!*
*Kamulike wala rushwa,*
*Kamulike mafisadi,*
*Kamulike maadui,*
*Mulika mipaka yetu.*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Msafara ulipofika shuleni, ulisimama. Wakimbiza mwenge wakashuka kwenye magari. Walitupungia mikono na kusalimiana na watu mbalimbali. Walimu, askari na viongozi wengine walituelekeza kukusanyika chini ya mti mkubwa wa mkuyu uliopo shuleni.

Watu wote walipokusanyika, Mwalimu Mkuu alichukua kipazasauti, akawakaribisha wageni wote shuleni kwetu. Alisoma **risala** kwa Mgeni Rasmi aliyeitwa Bi. Matandika.



FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

***RISALA YA WALIMU NA WANAFUNZI WA SHULE YA MSINGI CHANGANYIKENI KWA MGENI RASMI, KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU***

*Ndugu Mgeni Rasmi, awali ya yote, tunatoa shukurani zetu kwako na kwa kamati nzima ya mbio za Mwenge, kwa kukubali kuja katika shule yetu. Tunayo furaha kwa shule yetu kuchaguliwa kuwa miongoni mwa vituo vinavyoupokea Mwenge wa Uhuru mwaka huu.*

*Ndugu Mgeni Rasmi, shule hii ilianzishwa mwaka 1985 ikiwa na jumla ya wanafunzi 100 na walimu wawili. Kati ya wanafunzi hao, wavulana walikuwa 45 na wasichana 55. Shule ilikuwa na vyumba viwili tu vya madarasa.*

*Ndugu Mgeni Rasmi, mpaka sasa shule hii ina jumla ya wanafunzi 870 wa Darasa la Kwanza hadi la Saba. Kati yao, wanafunzi 420 ni wavulana na 450 ni wasichana. Kwa sasa, shule hii ina walimu 15. Walimu 10 ni wa kike na 5 ni wa kiume.*

*Ndugu Mgeni Rasmi, shule hii imekuwa ikitoa wastani wa wanafunzi 20 kila mwaka kujiunga na kidato cha kwanza. Haya ni mafanikio makubwa ambayo shule yetu inajivunia. Vilevile, idadi ya vyumba vya madarasa imeongezeka kutoka viwili hadi kumi na viwili.*

*Ndugu Mgeni Rasmi, mafanikio haya yametokana na juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali yetu ikishirikiana na wazazi, walezi, walimu na wanafunzi wa Shule ya Msingi Changanyikeni. Wote wamekuwa mstari wa mbele kuona shule inasonga mbele kitaaluma.*

*Ndugu Mgeni Rasmi, pamoja na mafanikio hayo, shule hii inakabiliwa na changamoto mbalimbali. Changamoto hizo ni uchakavu na upungufu wa baadhi ya* ***miundombinu****. Changamoto kubwa ni upungufu wa vyumba vya madarasa. Hali hii inasababishwa na ongezeko kubwa la wanafunzi.*

*Ndugu Mgeni Rasmi, sanjari na hilo, kuna vyumba vingine vya madarasa vimechakaa. Vyumba hivyo vina nyufa katika kuta, sakafu zimeharibika na mapaa yanavuja. Hivyo, hali hii huleta adha kwa wanafunzi na walimu pindi mvua inaponyesha. Vilevile, ofisi ya walimu ni ndogo ikilinganishwa na idadi ya walimu waliopo sasa.*

*Ndugu Mgeni Rasmi, changamoto nyingine ni upungufu wa matundu ya vyoo. Shule ina matundu saba ya vyoo. Wavulana wanatumia matundu matatu na wasichana vivyo hivyo. Walimu wanatumia tundu moja.*

*Ndugu Mgeni Rasmi, changamoto nyingine ni upungufu wa samani. Madawati yaliyopo hayatoshelezi kulingana na idadi ya wanafunzi waliopo. Hali hii husababisha wanafunzi wengine kukaa chini wanapokuwa darasani. Pia, meza na viti havitoshelezi idadi ya walimu waliopo. Hivyo, walimu wengine hulazimika kukaa kwenye madawati ambayo pia ni machache na hayawatoshi wanafunzi wenyewe.*

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 78 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Ndugu Mgeni Rasmi, wanafunzi, walimu na wazazi, kwa kushirikiana na Serikali, hutatua changamoto hizo ili kuendelea kulisukuma gurudumu la maendeleo ya shule yetu. Mathalani, tumefanikiwa kuanza ujenzi wa jengo lenye vyumba vitano vya madarasa.*

*Ndugu Mgeni Rasmi, mwisho, kwa heshima na taadhima, tunaomba utuwekee jiwe la msingi kwenye jengo jipya litakalokuwa na vyumba vitano vya madarasa. Jengo hili linajengwa kwa nguvu za wananchi kwa kushirikiana na Serikali.*

Mwalimu Mkuu alimaliza kusoma risala, akaenda kumkabidhi Mgeni Rasmi nakala ya risala hiyo. Mgeni Rasmi alisimama na kuipokea. Wageni na watu wengine wote tulisimama pia. Mgeni Rasmi na viongozi mbalimbali walitembea kuelekea panapojengwa vyumba vipya vya madarasa ili kuweka jiwe la msingi.

Baada ya kuweka jiwe la msingi, Mgeni Rasmi alikaribishwa kuzungumza kwa niaba ya wenzake wote. Aliwashukuru walimu, wanafunzi na uongozi wa shule yetu kwa mapokezi mazuri. Pia, aliwapongeza wazazi na viongozi wa shule kwa juhudi kubwa ya kuboresha miundombinu ya shule.

Alitutangazia kuwa mwaka huo, mbio za Mwenge wa Uhuru zilikuwa zinaeneza ujumbe usemao, **"Tufanye kazi kwa bidii na maarifa, tuijenge nchi yetu."** Aliwapongeza watu wote wanaofanya kazi kwa bidii na maarifa ili kujiletea maendeleo na kujenga nchi. Vilevile, alituhimiza sisi wanafunzi kujifunza kwa bidii ili tupate maarifa yatakayotusaidia maishani.

Baada ya hapo, wageni waliingia kwenye magari na kuendelea na safari yao ya kukimbiza Mwenge wa Uhuru. Sitaisahau siku hiyo katika maisha yangu.

## Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Je, Mwenge wa Uhuru ulisimama katika shule gani?
2. Wakati wa kuupokea Mwenge wa Uhuru, watu wengi walijipanga wapi?
3. Watu walikusanyika chini ya mti gani?
4. Je, watu hao walikuwa na nyuso zilizoonesha nini?
5. Kiongozi wa mbio za Mwenge aliitwa nani?
6. Je, risala ilisomwa na nani kwa mgeni rasmi?
7. Taja mafanikio ya Shule ya Msingi Changanyikeni.
8. Je, changamoto zipi zinaikabili Shule ya Msingi Changanyikeni?
9. Je, kiongozi wa mbio za Mwenge alifanya shughuli zipi katika Shule ya Msingi Changanyikeni?
10. Je, ujumbe wa mbio za Mwenge mwaka huo ulikuwa upi?



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 79 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la pili: Msamiati

**Eleza maana ya maneno yafuatayo, kisha tunga sentensi moja kwa kila neno.**

1. wadia
2. kifunguakinywa
3. jiwe la msingi
4. shamrashamra
5. kandokando
6. punga
7. shauku
8. fursa
9. shuhudia
10. bashasha
11. wasaa
12. msafara
13. risala
14. miundombinu

## Zoezi la 3: Mazoezi ya lugha

**A. Badili sentensi zifuatazo kuwa katika wakati uliopita.**

**Mfano:** Mama anakwenda sokoni.
*Mama alikwenda sokoni.*
Watu wengi watajipanga kandokando ya barabara kuupokea Mwenge wa Uhuru.
*Watu wengi walijipanga kandokando ya barabara kuupokea Mwenge wa Uhuru.*

(i) Mwenge wa Uhuru utapita Shule ya Msingi Changanyikeni.
(ii) Kiongozi wa mbio za Mwenge anatusalimu.
(iii) Risala inasomwa mbele ya mgeni rasmi.
(iv) Changamoto zitatajwa kwenye risala.
(v) Shule ya Msingi Changanyikeni itaandikisha wanafunzi wengi.
(vi) Wanafunzi wanaimba wimbo wa kuusifu Mwenge.
(vii) Walimu wanaishi mbali na shule.
(viii) Watu watashikilia matawi ya miti kushangilia Mwenge wa Uhuru.
(ix) Wanafunzi wataketi chini ya mkuyu.
(x) Jiwe la msingi litawekwa na kiongozi wa mbio za Mwenge.

**B. Andika kinyume cha maneno yafuatayo:**

**Mfano:** tema - *meza*
kataza - *ruhusu*

(i) furaha
(ii) raha
(iii) baraka
(iv) mwalimu
(v) nuru
(vi) ukali
(vii) upendo
(viii) mlima
(ix) faida
(x) mwadilifu

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 80 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**C. Andika neno moja lenye maana sawa na tungo zifuatazo, kisha tunga sentensi moja kwa kila neno.**

**Mfano:** Kitu anachopewa mtu baada ya kuhitimu elimu au mafunzo fulani na kufaulu - *cheti*
*Joni alipohitimu Darasa la Saba na kufaulu vizuri, alipewa cheti.*

(i) Tendo la kunyang'anya mtu haki au mali yake. _____
(ii) Eleza au toa habari ya mambo yatakayotokea baadaye. _____
(iii) Nenda kutoka mahali fulani hadi pengine kwa miguu au kwa chombo cha usafiri. _____
(iv) Mahali ambapo sheria za nchi hutungwa. _____
(v) Ondoa ngozi ya mnyama aliyekufa. _____
(vi) Leta akilini fikira ya jambo lililotokea au lililopita. _____
(vii) Kitu anachopewa mtu kama ishara ya wema, upendo au ushindi. _____
(viii) Kuwa na hali ya kustaajabu baada ya kuona au kusikia jambo fulani. _____

**D. Tunga maswali sahihi kumi (10) kutokana na jedwali lifuatalo:**

| | | |
|---|---|---|
| Je, | Mwenge wa Uhuru<br>Mwalimu Mkuu<br>wanafunzi<br>jiwe la msingi<br>wananchi | liliwekwa na kiongozi wa mbio za Mwenge?<br>alisoma risala kwa mgeni rasmi?<br>walipunga mikono?<br>ulipita Shule ya Msingi Changanyikeni?<br>walijipanga katika msururu?<br>walikaa chini ya mkuyu?<br>walishikilia matawi ya miti?<br>waliimba wimbo unaohusu Mwenge?<br>alitaja mafanikio ya shule?<br>ni alama ya taifa letu?<br>liliwekwa katika jengo la madarasa mapya? |

**E. Panga sentensi zifuatazo ili zilete mtiririko sahihi.**

(i) Wanafunzi walipofika shuleni, walisafisha mazingira ya shule.
(ii) Baada ya muda mfupi, wanafunzi wakasikia mlio wa king'ora kilichoongoza msafara wa Mwenge.
(iii) Wanafunzi walipokuwa njiani kwenda shuleni, walikutana na watu wengine wakienda kuupokea Mwenge.
(iv) Mwalimu Mkuu aliwakaribisha wageni, kisha akasoma risala.
(v) Wanafunzi walipomaliza kusafisha mazingira, walijipanga kandokando ya barabara ili kuupokea Mwenge.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 81 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(vi) Baada ya kusomewa risala, mgeni rasmi aliweka jiwe la msingi.
(vii) Mwishowe, mgeni rasmi aliwashukuru watu wote, akawatangazia ujumbe wa mbio za Mwenge, msafara ukaondoka.
(viii) Mara, waliona msafara wa magari yaliyokimbiza Mwenge ukiingia shuleni.
(ix) Wanafunzi waliamka asubuhi na mapema ili kwenda shuleni kuupokea Mwenge wa Uhuru.
(x) Watu wote waliupokea Mwenge kwa wimbo, nderemo na vifijo, kisha wakakusanyika chini ya mkuyu.

**F. Andika maneno mengine yenye maana zinazofanana na za maneno haya:**

**Mfano:** *azma - kusudio*
*bure - bwerere*
*geza - iga*

(i) chumvi ____________
(ii) mvinyo ____________
(iii) asubuhi ____________
(iv) mno ____________
(v) huzuni ____________
(vi) barua ____________
(vii) siri ____________
(viii) gilasi ____________
(ix) msichana ____________
(x) mvulana ____________
(xi) jabali ____________
(xii) mwangaza ____________

**G. Andika KWELI kwa maelezo yaliyo sahihi au SI KWELI kwa maelezo yasiyo sahihi.**

(i) Risala haiandikwi anuani ya mgeni rasmi. ____________
(ii) Siyo lazima kuanza na ndugu mgeni rasmi kwa kila aya. ____________
(iii) Kichwa cha habari ni jambo la muhimu kwenye risala yoyote. ____________
(iv) Inatakiwa kuweka saini ya mhusika aliyeandika risala mwisho wa risala. ____________

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 82 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(v) Risala inaweza kusomwa na mtu mwingine kwa niaba ya mgeni rasmi. _______________

(vi) Risala hueleza mafanikio na changamoto juu ya jambo fulani. _________________

(vii) Baada ya risala kusomwa hukabidhiwa kwa mgeni rasmi._________________

(viii) Uandishi wa risala hufuata hatua zote za uandishi. _________

(ix) Risala inaweza kusomwa kimya. ___________________

(x) Risala husomwa na mtu yeyote aliyechaguliwa kufanya hivyo. ________________

**H. Pigia mstari neno lisiloendana na maneno mengine katika kila kifungu cha maneno.**

**Mfano:** *embe, ndizi, <u>mahindi</u>, tikiti*
*gari, pikipiki, baiskeli, <u>ndege</u>*

(i) risala, hotuba, barua, shule
(ii) kibarua, kazi, shughuli, rambirambi
(iii) furaha, bashasha, fadhaa, tabasamu
(iv) msururu, duara, mstari, foleni
(v) waridi, mkuyu, msonobari, mkaratusi, mninga
(vi) mwalimu, mwenge, shule, mwanafunzi, kitabu
(vii) redio, nyumba, gazeti, runinga, simu, barua
(viii) meza, kiti, ndoo, dawati, kabati
(ix) dawa, posta, tabibu, hospitali, mkunga

## Zoezi la 4: Utungaji

**Fikiria kuwa wewe ni kiranja mkuu wa shule. Andika risala ya wanafunzi itakayosomwa kwa mgeni rasmi siku ya mahafali ya Darasa la Saba.**

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 83 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi

## Kutumia kamusi

### Utangulizi

*Katika sura hii, utajifunza maana ya kamusi na jinsi ya kuitumia. Vilevile, utajifunza jinsi ya kuandika maneno na maana zake katika kamusi. Maarifa haya yatakusaidia kutambua, kutumia na kutamka maneno ya lugha kwa usahihi katika mawasiliano.*

### Fikiri



1. Je, umewahi kusikia au kusoma maneno usiyoyajua maana zake?
2. Je, ulitafuta maana zake wapi?
3. Je, uliweza kutumia maneno hayo katika mawasiliano?

### Ufahamu

*Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

**Ugonjwa wa maana**

Bwana **Kidahizo** na mke wake Bi **Maarifa** walibahatika kuzaa mtoto mmoja tu wa kike katika umri wao wa utu uzima. Wazazi hawa walimpenda sana binti yao huyo wa pekee aliyekuwa akiitwa **Kitomeo**. Kitomeo alikuwa msichana mwenye akili nyingi, mdadisi na mwenye maadili. Alipendwa sana na wazazi wake pamoja na jamii nzima ya kijiji chao kwa ujumla.

Siku moja, Kitomeo alipatwa na homa kali. Alitibiwa na matabibu wa kila aina, lakini hakupona homa hiyo. Kwa sababu walimpenda sana binti yao, Bwana Kidahizo na mke wake walimpeleka kwa waganga na waaguzi, lakini hali yake ikazidi kudhoofu. Wakakaa chini na kutafakari kwa kina. Baada ya kutafakari, Kidahizo akamwambia mkewe, "Tusipopambana kwa ajili ya afya ya binti yetu tutampoteza." Mke wake akamjibu, "Tumepambana sana mume wangu, lakini hakuna nafuu. Unadhani tufanyeje sasa?"

Bwana Kidahizo akajibu,"Mimi nadhani twende kwa Mzee Fasili ambaye huwa anatoa ushauri kwa watu waliotingwa na dhiki na shida mbalimbali. Tukimwambia shida yetu, huenda anaweza kutusaidia. Yeye amejaliwa hekima na ana elimu kubwa ya mambo lukuki," Kidahizo alishauri.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 84 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kidahizo na mke wake Maarifa pamoja na binti yao Kitomeo walikwenda kwa Mzee **Fasili**. Mzee Fasili alikuwa mzee mwenye hekima hapo kijijini kwao. Watu walizoea kumwita "Mzee wa hekima." Walifika na kueleza shida yao. Wakasema, "Binti yetu ameugua kwa muda mrefu. Amepata matibabu ya kila aina, lakini hakupata ahueni yoyote." Mzee Hekima akafumbua kinywa na kuwaambia, "Mmehangaika kwa muda mrefu kutafuta matibabu ya binti yenu, lakini shida aliyonayo jawabu lake ni **maana** tu." "Maana!" Wazazi wakashikwa na mshangao. "Ndiyo! Maana ndiyo dawa itakayomtibu Kitomeo." Alisisitiza Mzee Hekima. "Una maana gani Mzee Hekima?" Wazazi waliuliza. "Nina maana hiyohiyo." Mzee Hekima alijibu na kufafanua, "Siku mkijua maana ya jina lake, binti yenu Kitomeo atapona papo hapo." Baada ya kauli ya Mzee Hekima, wazazi walihamaki. Wakasema, "Hiyo maana tutaitoa wapi sasa, kwani sisi tulimpa tu jina hilo na hatujui maana yake." Mzee Hekima akawaambia, "Safirini mwende katika nchi ya Ughaibuni. Huko kuna pacha wangu anaitwa **Kamusi**. Huyu ni tajiri wa maana. Atawajulisha maana ya jina Kitomeo. Si hivyo tu, atawajulisha pia kuhusu aina na kazi ya Kitomeo. Vilevile, atawajulisha maana ya **maneno** yote ya **lugha** kama mtahitaji." Wazazi wakabaki wanatazamana na kushangaa.

Kesho yake asubuhi, Kidahizo akaondoka pamoja na binti yake Kitomeo. Wakasafiri kuelekea nchi ya Ughaibuni kwenda kutafuta maana ya jina la Kitomeo. Safari hii iliwachukua muda wa siku saba. Hatimaye, walifika kwenye nchi hiyo. Walimkuta askari aliyeitwa **Msamiati**, wengine walimwita Bwana Maneno kwa kuwa alikuwa akiongea sana kama chiriku. Askari aliwapeleka moja kwa moja mpaka kwa Bwana Kamusi. Walipoeleza shida yao, Bwana Kamusi aliwachukua akawapitisha kwenye barabara iliyojengwa na kupangiliwa vizuri iitwayo **Alfabeti**. Humo barabarani, walipishana na watu wengi ambao salamu yao haikuwa ya kawaida, bali ilikuwa "**herufi**". Baada ya dakika kama tano hivi, walipotazama mbele kulia wakamwona mtu aliyefanana kabisa na Kitomeo. Wakastaajabu na kumsabahi kwa salamu yao, "Herufi." Yeye akajibu, "Ka." Huyu akawaingiza kwenye chumba cha daktari aliyewapa maana ya majina yao wote.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 85 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



k

**kidadisi** /kida'di:si/ *nm.* (*vi-*) {*ki-/vi-*} orodha ya maswali inayotumiwa kama zana ya utafiti inayoandaliwa kwa lengo la kutafuta taarifa kutoka kwa watu wakataojibu ***kis.:*** hojaji

**kidahizo** /kida'hizɔ/ *nm.* (*vi-*) {*ki-/vi-*} neno kuu katika kamusi ambalo agh. huingizwa kwa rangi iliyokoza na pengine tofauti hutolewa fasili, pia huendelezwa kwa kuonyesha matamshi, aina ya neno, ngeli yake kutegemeana na aina ya kamusi inayoandikwa

**kidaka** /ki'da:ka/ *nm.* (*vi-*) {*ki-/vi-*} pia **kidanga** nazi changa kabisa yenye rangi ya kijani ambayo hutokea kwenye hatua ya pili ya ukuaji wa nazi iliyo katikati ya maua na dafu ***mat.:*** *Watoto wa kike hupenda kuigiza mapishi ya nazi kwa kutumia ~.* ***kis.:*** kidanga

**kidakatonge** **kidaka+tonge** /kidaka'tɔŋgɛ/ *nm.* (*vi-*) {*ki-/vi-*} kinyama kidogo nyuma ya ulimi mithili ya kidole ambacho hujifunga wakati wa kumeza kitu kuzuia chakula kisiingie kwenye njia inayokwenda kwenye mapafu ***vis.:*** kilimi, kimeo, kimegedu

**kidako**[1] /ki'dakɔ/ *nm.* (*vi-*) {*ki-/vi-*} taz. **kizio**[1] **a.**

**kidako**[2] /ki'dakɔ/ *nm.* (*vi-*) {*ki-/vi-*} (*kibah*) sehemu ambayo nahodha hukaa anapo-ongoza chombo cha majini

**kidako**[3] /ki'dakɔ/ *nm.* (*vi-*) {*ki-/vi-*} sehemu ambayo ngoma ya kupunga shetani husimama na kupigwa kwa muda kisha kuendelea na safari

**kidakuzi** /kida'kuzi/ *nm.* (*vi-*) {*ki-/vi-*} biskuti ambayo ina ladha nzuri sana

**kidamu** /ki'damu/ *nm.* (*vi-*) {*ki-/vi-*} (*kibah*) sehemu iliyoko upande wa mbele katika chombo cha majini

**kidanga** /ki'daŋga/ *nm.* (*vi-*) {*ki-/vi-*} taz. **kidaka**

**kidangedange** /kidaŋgɛ'daŋgɛ/ *kiv.* -enye kukosa utulivu, -enye kuhangaika

K

linalopikwa kwa kutiwa nazi na sukari; kipopoo

**kitobwe** /ki'tɔbwɛ/ *nm.* (*vi-*) {*ki-/vi-*} sehemu ya ardhi agh. bondeni ambapo kuna matope; kitoso

**kitobwesha** /kıtɔ'bwɛʃa/ *nm.* (*vi-*) {*ki-/vi-*} taz. **kitobosho**

**kitokono** /kitɔ'kɔnɔ/ *nm.* (*vi-*) {*ki-/vi-*} mfupa wa mwisho kabisa kwenye uti wa mgongo; kidundumavi ***vis.:*** kinyunguu, kifandugu

**kitoleo** /kitɔ'lɛwɔ/ *nm.* (*vi-*) {*ki-/vi-*} kifaa kinachotumika kutolea kitu

**kitoma** /ki'tɔma/ *nm.* (*vi-*) {*ki-/vi-*} **a.** kibuyu kinachotumika kutunzia vioevu k.v. maji, maziwa n.k. **b.** mfuko unaotunza kende **ch.** kijumba cha kutunzia ndege; kirimba ***vis.:*** ndio, susu

**kitomeo** /kitɔ'mɛjɔ/ *nm.* (*vi-*) {*ki-/vi-*} kidahizo kinachoingizwa kwenye kamusi kikiwa na ufafanuzi wake pamoja na taarifa zake nyingine

**kitone** /ki'tɔnɛ/ *nm.* (*vi-*) {*ki-/vi-*} (*saruf*) alama ya uakifishi ya mviringo (.) inayotumika kuonyesha agh. mwisho wa sentensi; nukta ***kis.:*** kituo

**kitonge** /ki'tɔŋgɛ/ *nm.* (*vi-*) {*ki-/vi-*} **a.** unga wa nafaka unaokandwa kwa lengo la kutengeneza chakula jamii ya maandazi; kinyunya **b.** kikundi cha viumbe agh. wanyama au watu; mkusanyiko

**kitongo**[1] /ki'tɔŋgɔ/ *kiv.* **a.** -a kukingama, -a mshazari, -a upandeupande, -a chongochongo **b.** -a wasiwasi, -a shaka ***mat.:*** *Tazama mtu ~* = mwangalie mtu kichongochongo, kimshazari

**kitongo**[2] /ki'tɔŋgɔ/ *nm.* (*vi-*) {*a-/wa-*} nyuni mdogo jamii ya sigi; kisengenye ***kis.:*** kitororo

**kitongoji** /kitɔ'ŋgɔɟi/ *nm.* (*vi-*) {*ki-/vi-*} **a.** eneo la makazi ya watu agh. dogo kuliko kijiji; kijiji kidogo, kiambo **b.** sehemu ya mji iliyotengwa kwa ajili ya makazi ya watu; mtaa ***vis.:*** kata, hara

Alianza na jina la baba, akasema, “Kidahizo ni maneno yaliyo katika kamusi na yaliyokolezwa kwa wino ili kupewa ufafanuzi.” Pia akasema, “Kitomeo ni kidahizo, pamoja na **taarifa** zake zote.”

Baada tu ya kusikia maana hiyo, Kitomeo akapona papo hapo na kuanza kutabasamu. Baada ya matibabu hayo, Kidahizo na binti yake Kitomeo wakashukuru na kuaga, kisha wakaondoka kurejea kwao.

Walipofika nyumbani, mama alifurahi sana kumwona binti yake Kitomeo akiwa mzima mwenye afya. Kitomeo akamwambia mama yake, “Mama tulipofika huko kwa Bwana Kamusi, tuliona mambo mengi. Yeye ana akili na maarifa



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 86 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

mengi sana. Pia, ana hospitali yenye madaktari wanaotibu akili kwa kudokeza maana za maneno, kutaja na kubainisha aina za maneno.

Pia, wanaonesha **matamshi** sahihi ya maneno. Vilevile, Bwana Kamusi anaonesha wingi na umoja pamoja na mifano ya matumizi ya maneno.

"Ama kweli huyo ni Bwana Kamusi, nami nitamtembelea siku moja ili anipe maana za maneno mbalimbali nisiyoyajua," mama alihitimisha.

## Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Taja jina la mtoto wa pekee wa Bwana Kidahizo.
2. Taja jina lingine la Mzee Fasili.
3. Eleza kazi mbili za Mzee Hekima.
4. Mtoto wa Bwana Kidahizo alikuwa anaumwa ugonjwa gani?
5. Pacha wa Mzee Fasili anaitwa nani?
6. Bwana Kamusi anafanya kazi gani?
7. Kidahizo kina maana gani kama ulivyosoma kwenye habari?
8. Madaktari walikuwa wanawatibu watu akili kwa kufanya nini?
9. Mwishoni mama aliahidi kufanya nini?
10. Habari hii inatufundisha nini?

## Zoezi la pili: Msamiati

**Tumia kamusi kutafuta maana ya maneno yafuatayo, kisha tunga sentensi moja kwa kila neno.**

1. kidahizo
2. maarifa
3. kitomeo
4. tafsiri
5. maana
6. kamusi
7. maneno
8. lugha
9. msamiati
10. alfabeti
11. herufi
12. taarifa
13. matamshi

## Zoezi la 3: Nahau na misemo

**Chagua jibu sahihi na uliandike kwenye nafasi zilizoachwa wazi.**

(i) Sema maneno kwa kusitasita …………………..
(a) gonga maneno
(b) chapa maneno
(c) gugumiza maneno
(d) shindwa kuongea

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 87 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(ii) Kuwa na hofu au wasiwasi ……………..

(a) gwaya moyo
(b) kaa ange
(c) guu kwa guu
(d) kutetemeka

(iii) Kasirika sana ……………..

(a) iva miguu
(b) iva macho
(c) lainika moyo
(d) iva nyonga

(iv) Toa uamuzi wa mwisho ……………..

(a) kata hukumu
(b) kata mkia
(c) kata kiu
(d) kata maneno

(v) Kucheka sana ……………..

(a) furahi sana
(b) cheka mno
(c) kufa mbavu
(d) kufa kifua

(vi) Kuwa na sifa ya kufanya mambo polepole ……………..

(a) kuwa na mkono mrefu
(b) kuwa na mkono mzuri
(c) kuwa na mkono mfupi
(d) kuwa na mkono mzito

(vii) Macho yasiyoonesha haya ……………..

(a) macho mabichi
(b) macho makavu
(c) macho bila miwani
(d) macho yenye utando

(viii) Nenepa au kuwa na mwili mnene ……………..

(a) pata nafuu
(b) pata tija
(c) pata mwili
(d) pata kichwa

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 88 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(ix) Chukua muda katika jambo fulani …………….

(a) weka muhula
(b) weka jambo
(c) kamata muda
(d) weka sawa

(x) Anzisha jambo ……………..

(a) weka majira
(b) weka msingi
(c) weka shule
(d) weka wanafunzi

## Zoezi la 4: Mazoezi ya lugha

**A. Oanisha maneno kutoka safu A na vinyume vyake kutoka safu B.**

| Safu A | Safu B |
|---|---|
| (i) swali | (a) zima |
| (ii) hodari | (b) funua |
| (iii) bandika | (c) huzunisha |
| (iv) furahisha | (d) adui |
| (v) rafiki | (e) bandua |
| (vi) washa | (f) jibu |
| (vii) panga | (g) mvivu |
| (viii) funika | (h) haribu |
| (ix) shika | (i) pangua |
| (x) tengeneza | (j) acha |

**B. Badili sentensi zifuatazo ziwe katika hali ya mazoea.**

**Mfano:** Mwajuma anakwenda shuleni siku tano za wiki.
*Mwajuma huenda shuleni siku tano za wiki.*

(i) Bibi anakula mahindi ya kuchoma.
(ii) Babu anamenya miwa kwa kasi.
(iii) Mbwa wetu anabweka usiku.
(iv) Subira anafua sare zake za shule vizuri.
(v) Pikipiki inakimbia sana.
(vi) Askari anashusha bendera.



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(vii) Abiria wanagombania nafasi ya kuketi.
(viii) Kijana anapanda ukuta kwa urahisi.
(ix) Watoto wanapenda maziwa ya mama.
(x) Panya wanajificha kwenye kabati.

## C. Andika visawe vya maneno yafuatayo:

**Mfano:** fasili – *ufafanuzi*
juma - *wiki*

(i) beseni
(ii) chumvi
(iii) mgumba
(iv) treni
(v) gari
(vi) msamiati
(vii) chapuchapu
(viii) changarawe
(ix) gulio
(x) jamvi

## D. Panga maneno yafuatayo kialfabeti.

| |
|---|
| mama, miti, polisi, mtu, mwalimu, shule, kikombe, kataza, nguo, kijiji, sahani, dada, kituo, ndoo, alfabeti, herufi, maneno, Januari |

## E. Tunga sentensi kumi (10) kutokana na jedwali lifuatalo.

**Mfano:** *Yeye akija atatupeleka uwanja wa ndege.*

| | | |
|---|---|---|
| Tatu na rafiki yake | | tutapata maziwa yatakayosaidia afya zetu |
| Garimoshi | ikija | atatupeleka uwanja wa ndege |
| Mwalimu Zakayo | akija | tutaanza safari |
| Kimbunga | wakija | tutaitangaza nchi yetu |
| Mvua | kikija | kitaezua paa letu tukose mahali pa kulala |
| Yeye | likija | itaokoa mazao yaliyoathiriwa na jua |
| Watalii | | kila kitu kitakuwa rahisi mno |
| Ng'ombe | | |

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 90 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**F. Andika maneno kumi na tano (15) kutokana na jedwali lifuatalo:**

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A | A | S | A | L | Z | K | A | K | A |
| M | L | M | A | E | E | A | U | I | I |
| A | U | F | K | F | T | Y | S | T | B |
| T | L | E | A | A | U | A | O | O | U |
| A | K | A | M | B | O | N | I | W | E |
| N | Z | I | I | B | E | I | D | E | E |
| O | O | K | L | N | E | T | I | O | A |
| W | A | K | I | L | I | N | I | N | A |

**G. Zungushia herufi ya jibu sahihi.**

**Mfano:** Mwanafunzi huyu ni mwaminifu. Neno huyu ni:
(a) kihisishi (b) kielezi (c) kiwakilishi ⓓ kivumishi

(i) Watoto wakorofi wamelala. Neno wakorofi ni:
(a) kitenzi (b) nomino (c) kivumishi (d) kiwakilishi

(ii) Mtoto wa ng'ombe anaitwa:
(a) maksai (b) mtamba (c) mdoli (d) ndama

(iii) Tulikula ugali kwa mtindi. Neno mtindi lina maana gani?
(a) Maziwa yaliyoganda (b) maziwa yasiyoganda (c) maziwa baridi (d) maziwa

(iv) Yule ni mzee Hamisi. Neno lililopigiwa mstari ni la aina ipi ya maneno?
(a) kielezi (b) kiunganishi (c) nomino (d) kiwakilishi

(v) Jumanne hula ugali kila Jumatano. Sentensi hii iko katika hali ipi?
(a) mazoea (b) umaskini (c) majigambo (d) dhanifu

(vi) Neno linaloingizwa kwenye kamusi ili lipatiwe maana huitwaje?
(a) nomino (b) kidahizo (c) kitomeo (d) kitenzi



FOR ONLINE USE ONLY

KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 91 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(vii) Mtu anayefanya kazi ya kufundisha darasani anaitwa nani?

(a) tabibu (b) utingo (c) mwalimu (d) mwanafunzi

(viii) Bakari _____ mvulana mtanashati.

(a) huwa (b) na (c) ni (d) lakini

(ix) Mtu mwenye taaluma ya sheria huitwaje?

(a) mwanataaluma (b) mwanagenzi (c) mwanahabari
(d) mwanasheria

(x) Kisawe cha neno adimu ni kipi?

(a) patikana (b) changa (c) chache (d) chenga

**H. Tunga sentensi mbili zenye maana tofauti kwa kila neno.**

**Mfano:** Mdomo - *Juma amevimba mdomo.*
*Chupa hii ina mdomo mkubwa*.

(i) mguu
(ii) kona
(iii) chemba
(iv) chombo
(v) mpira
(vi) uso
(vii) kupe
(viii) kichwa
(ix) kimbia
(x) choma

## Zoezi la 5: Kazi ya kufanya

**Soma kurasa tatu tofauti za kamusi kisha andika vidahizo sita na vitomeo vyake.**

## Zoezi la 6: Utungaji

**Tunga ukurasa mmoja wa kamusi wenye maneno manne na maana zake. Zingatia yafuatayo:**

(a) Mpangilio wa alfabeti
(b) Maana sahihi ya maneno
(c) Umoja na wingi

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 92 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Moja

## Matangazo ya biashara

### Utangulizi

*Katika sura hii, utajifunza kuhusu mambo ya kuzingatia katika uandishi wa matangazo ya biashara. Pia, utajifunza kuandika matangazo ya biashara, kusoma habari na kujibu maswali. Umahiri huu utakusaidia kuandika tangazo lolote la biashara.*

### Fikiri



1. Je, umeshawahi kuona tangazo lolote la biashara?
2. Uliliona wapi?
3. Je, tangazo hilo lilikuwa linahusu biashara gani?

### Ufahamu

*Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

**Nkosi asoma tangazo la biashara**

Ilikuwa ni siku ya Jumatano mwanana. Siku ambayo Nkosi, mtoto mwenye umri wa miaka kumi na miwili, alikuwa akitoka nyumbani kuelekea shuleni. Alipokuwa akikatiza mtaa wa Mikindani, kwa mbele, aliona kitambaa kikubwa cheupe chenye maandishi meusi kwa mbali. Kitambaa hicho kilikuwa kimefungwa kamba na kuning'inizwa juu ya miti. Alijiuliza kimoyomoyo, "Kile ni nini?" Aliamua kusogea mbele zaidi ili aone vizuri. Alipokikaribia kile kitambaa, aligundua kuwa ni **tangazo** la **biashara.** Aliamua kusogea karibu zaidi ili aweze kusoma tangazo lile. Tangazo liliandikwa hivi:

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 93 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY

**JIPATIE VITABU KWA BEI NAFUU**

Ewe mzazi, mlezi au mmiliki wa shule, jipatie vitabu bora kwa bei nafuu kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania. Tunauza vitabu vya Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari kwa shule zinazotumia lugha ya Kiswahili na Kiingereza kufundishia na kujifunzia. Tunapatikana Mwenge, Dar es Salaam. Pia, unaweza kununua vitabu vyetu kupitia maktaba mtandao na kwa mawakala wetu wote nchini.

*"Vitabu bora kwa elimu bora."*

Wasiliana nasi kupitia,

Simu: +255 222 773005

Nukushi: +255222774420

Baruapepe: director.general@tie.go.tz

Tovuti: www.tie.go.tz

Nkosi alisoma tangazo hilo kwa umakini sana. Alifurahi sana kusoma tangazo hilo na alipanga kwenda kumwambia mwalimu na baba yake.

Baada ya kumaliza kusoma tangazo hilo, Nkosi alichukua kalamu na karatasi kutoka kwenye begi lake la shule. Aliandika **mawasiliano** ya tangazo hilo. Baada ya kumaliza kuandika mawasiliano hayo, aliondoka kwa kasi kuelekea shuleni. Alipofika shuleni, aliingia darasani na masomo yakaendelea. Wakati wa mapumziko, alikutana na Mwalimu Huruma akiwa anaelekea ofisini kwake. Huruma ni mwalimu wa Kiswahili Darasa la Sita. Baada ya kukutana, mazungumzo yao yalikuwa kama ifuatavyo:

**Nkosi:** Shikamoo mwalimu!

**Mwalimu Huruma:** Marahaba Nkosi! Hujambo?

**Nkosi:** Sijambo mwalimu.

**Mwalimu Huruma:** Unaendeleaje na masomo?

**Nkosi:** Ninaendelea vizuri. Halafu mwalimu nimekumbuka, Leo nimeona tangazo la biashara.

**Mwalimu Huruma:** Umeliona wapi?

**Nkosi:** Nimeliona Mtaa wa Mikindani.

**Mwalimu Huruma:** Tangazo hilo linahusu nini?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Nkosi:** Linahusu uuzwaji wa vitabu bora kwa Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari.

**Mwalimu Huruma:** Tangazo hilo lina sifa gani?

**Nkosi:** Tangazo hilo limeandikwa kwa kutumia lugha rahisi na inayoeleweka.

**Mwalimu Huruma:** Nani ametoa tangazo hilo?

**Nkosi:** Taasisi ya Elimu Tanzania.

**Mwalimu Huruma:** Vizuri sana Nkosi. Tangazo hilo lina sifa gani nyingine?

**Nkosi:** Kichwa cha tangazo kimeandikwa kwa herufi kubwa.

**Mwalimu Huruma:** Vizuri sana. Je, tangazo hilo limetaja mambo gani ya msingi?

**Nkosi:** Tangazo hilo limetaja aina ya vitabu vinavyouzwa na mahali vinapouzwa.

**Mwalimu Huruma:** Je, ni vitabu gani vinauzwa na Taasisi ya Elimu Tanzania?

**Nkosi:** Vitabu vinavyouzwa ni vya masomo yote ya Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari. Vitabu hivyo ni kwa shule zinazotumia lugha ya Kiswahili na Kiingereza.

**Mwalimu Huruma:** Wauzaji wanapatikana wapi?

**Nkosi:** Wauzaji wanapatikana katika ofisi zao zilizoko Mwenge, Dar es Salaam. Pia, kwenye tangazo wameeleza kuwa unaweza kununua vitabu hivyo kupitia maktaba mtandao.

**Mwalimu Huruma:** Kweli nimekumbuka. Wakati wa uzinduzi wa uuzwaji wa vitabu hivyo, niliona na kusikia kupitia **taarifa** ya **habari**. Walisema kuwa maktaba mtandao ni maktaba inayotumia **mtandao** wa **intaneti.** Ama kweli **teknolojia** inarahisisha mambo. Nkosi, kwenye tangazo hilo kulikuwa na nini tena?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Nkosi:** Wametaja mawasiliano yao kama mtu anataka kununua vitabu.

**Mwalimu Huruma:** Mawasiliano yao ni ya aina gani?

**Nkosi:** Mawasiliano yao ni kwa njia ya simu, **tovuti**, **nukushi** na **baruapepe.**

**Mwalimu Huruma:** Je, umechukua mawasiliano yao?

**Nkosi:** Ndiyo mwalimu. Nimeyaandika kwenye karatasi ili nikampe baba aninunulie vitabu.

**Mwalimu Huruma:** Vizuri sana Nkosi. Utawapa wanafunzi wenzako waya**hifadhi** na kuwapelekea wazazi wao ili wawanunulie vitabu vya masomo yote.

**Nkosi:** Sawa mwalimu.

**Mwalimu Huruma:** Asante sana Nkosi. Kwaheri.

**Nkosi:** Kwaheri mwalimu.

## Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Nkosi ni mtoto mwenye umri wa miaka mingapi?
2. Nkosi alipoona tangazo la biashara, alikuwa anaelekea wapi?
3. Nkosi aliona tangazo la biashara siku gani?
4. Nkosi aliona tangazo la biashara kwenye mtaa upi?
5. Nani alitangaza tangazo alilolisoma Nkosi?
6. Tangazo la biashara alilolisoma Nkosi, lilikuwa linahusu nini?
7. Huruma ni mwalimu wa darasa la ngapi?
8. Taja sifa za matangazo ya biashara.
9. Umejifunza nini kutokana na habari uliyoisoma?
10. Mambo gani ya kuzingatia katika uandishi wa tangazo la biashara?

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 96 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la pili: Msamiati

**Eleza maana ya msamiati ufuatao, kisha tunga sentensi moja kwa kila msamiati.**

**Mfano:** *mwanana - tulivu au shwari*

*Upepo **mwanana** ulivuma kutoka baharini.*

1. tangazo
2. biashara
3. mawasiliano
4. taarifa
5. habari
6. mtandao
7. intaneti
8. teknolojia
9. tovuti
10. nukushi
11. baruapepe
12. hifadhi

## Zoezi la 3: Methali

**Kamilisha methali zifuatazo:**

**Mfano:** Mzoea punda ……………..

Mzoea punda, hapandi farasi.

1. Mbaazi ukikosa maua, ……………………………
2. ……………………………, hali wali mkavu.
3. Hasira ya mkizi, …………………………
4. ………………………., ulimwengu shujaa.
5. Cha kuzama, …………………………
6. ……………………………… ni mpenzi wa Mungu.
7. ………………………., kuliko meno.
8. Wingi …………………………
9. …………………, furaha ya kunguru.
10. Vita ya panga, ………………………………………

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 97 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 4: Mazoezi ya lugha

**A. Tumia herufi za maneno yafuatayo kuunda maneno mengine mapya.**

**Mfano:** *lima - mali*

(i) koa ______________
(ii) zoa ______________
(iii) boa ______________
(iv) taka ______________
(v) koza ______________
(vi) mila ______________
(vii) ole ______________
(viii) pewa ______________
(ix) lewa ______________
(x) bakia ______________

**B. Andika kinyume cha maneno yafuatayo:**

**Mfano:** *tega - tegua*

(i) ita ______________
(ii) mvulana ______________
(iii) mkubwa ______________
(iv) mkali ______________
(v) mwenyeji ______________
(vi) mwerevu ______________
(vii) mchapakazi ______________
(viii) mtoto ______________
(ix) mwalimu ______________
(x) mwanga ______________


FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 98 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## C. Jaza fumbo lifuatalo kwa kutumia maelezo ya kwenda chini na kulia.




**Kwenda chini**

1. Mtu anayefundisha (herufi 7)
2. Mdudu anayeeneza ugonjwa wa malaria (herufi 3)
3. Hali ya kuwa na uhasama kati ya mtu na mtu (herufi 5)
4. Mateso au faini anayotozwa mtu kwa kuvunja kanuni au sheria (herufi 6)
5. Mtu anayesoma shuleni (herufi 10)

**Kwenda kulia**

1. Mfuatano au msururu wa watu wengi wanaotembea pamoja kuelekea mahali ili kutimiza lengo fulani (herufi 10)
6. Kifaa kinachotumika kukunia nazi (herufi 5)

## D. Kanusha sentensi zifuatazo:

**Mfano:** Nkosi alikuwa kijana mwenye umri wa miaka ishirini.

*Nkosi hakuwa kijana mwenye umri wa miaka ishirini.*

(i) Vijana wengi wanapenda kukaa bila kufanya kazi.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 99 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(ii) Nkosi aliona tangazo kuhusu uuzaji wa kiwanja.
(iii) Maganga anafanya kazi ya ualimu.
(iv) Tangazo la biashara limetumia lugha inayoeleweka.
(v) Maganga aliona tangazo la biashara Mtaa wa Kijiweni.
(vi) Shuleni ni mahali pa kwenda kucheza.
(vii) Mimi nimesoma tangazo la biashara.
(viii) Mwalimu amefundisha kuhusu uandishi wa matangazo ya biashara.
(ix) Baba amesoma gazeti leo.
(x) Unaweza kulipia vitabu kwa njia ya nukushi.

## E. Andika umoja au wingi wa maneno yafuatayo:

| Mfano: | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| | *mwaka* | *miaka* |
| | *mashine* | *mashine* |

| | | |
|---|---|---|
| (i) | mkoa | ____________ |
| (ii) | ____________ | majengo |
| (iii) | mtumishi | ____________ |
| (iv) | ____________ | mitaa |
| (v) | cheo | ____________ |
| (vi) | mnunuzi | ____________ |
| (vii) | ____________ | matangazo |
| (viii) | biashara | ____________ |
| (ix) | kijana | ____________ |
| (x) | gazeti | ____________ |

## F. Kamilisha sehemu zilizoachwa wazi kwa kujaza maneno yaliyo kwenye kisanduku.

**nzuri, kizuri, vizuri, wazuri, mzuri, mizuri, pazuri**

(i) Kiti ____________ kimenunuliwa.
(ii) Ofisi ____________ imefunguliwa.
(iii) Mti ____________ hutoa maua mengi.
(iv) Vyoo ____________ vimejengwa shuleni kwetu.
(v) Juma anaandikia kalamu ____________.
(vi) Chakula ____________ kinapikwa jikoni.
(vii) Mwalimu ____________ huwapenda wanafunzi wake.
(viii) Wazazi na walezi ____________ huwafundisha watoto wao adabu.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 100 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(ix) Tabia ___________ za watoto hujenga heshima kwa wazazi na walezi.
(x) Vikombe ___________ vimevunjika.
(xi) Mahali ___________ panavutia.

**G. Oanisha maneno ya sehemu A na maelezo yake kutoka sehemu B kwa kuandika herufi ya jibu sahihi mbele ya maelezo ya sehemu A kwenye nafasi iliyoachwa wazi.**

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| (i) Kichwa cha tangazo___ <br> (ii) Aina ya bidhaa inayouzwa___ <br> (iii) Mahali ambapo bidhaa hiyo inapatikana___ <br> (iv) Mawasiliano ya wauzaji wa bidhaa___ | (a) Taasisi ya Elimu Tanzania inauza vitabu bora vya Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari kwa bei nafuu sana <br> (b) Wasiliana nasi kupitia simu namba: +255 222773005 <br> (c) JIPATIE VITABU KWA BEI NAFUU <br> (d) Vitabu vinapatikana katika ofisi zetu zilizoko Mwenge, Dar es Salaam na kwa mawakala wetu wote nchini |

## Zoezi la 5: Utungaji

**Andaa tangazo la biashara kwa kuzingatia kanuni na taratibu zinazotakiwa katika uandishi wa tangazo la biashara.**

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 101 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Mbili

## Uundaji wa maneno

### Utangulizi

*Katika sura hii, utajifunza namna ya kuunda maneno ya lugha ya Kiswahili kwa kutumia njia mbalimbali. Pia, utasoma shairi la "Yai au Kuku (Jibu)" na kujibu maswali. Maarifa utakayoyapata, yatakusaidia kukuza na kuongeza msamiati wa lugha ya Kiswahili.*

### Fikiri



1. Taja maneno ya lugha ya Kiswahili unayoyafahamu.
2. Je, unafikiri maneno uliyotaja yalipatikanaje?

### Ufahamu

*Soma na ghani shairi lifuatalo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

**Yai au Kuku (Jibu)**

1. Mtunzi nawatungia, **mzozo** nilioona,
Yai eti abishia, asema kuku ni mwana,
Mzozo nau**tatua**, kuku ndiye mwenye jina,
Yai wewe ni mtoto, kuku kwako ndiye mama.

2. Mzozo wa mwaka jana, kule Darasa la Tano,
Yai ajidai sana, wakakosa mapatano,
Na kuku alikazana, kuleta **maelewano**,
Yai wewe ni mtoto, kuku kwako ndiye mama.

3. Alileta **taharuki**, kuwa kama mwanahewa,
Kutamani pikipiki, heshima lipotelewa,
Bora atafute TUKI, apate kukombolewa,
Yai wewe ni mtoto, kuku kwako ndiye mama.

4. Kitendawili teguka, kuku ndiye mwanzilishi,
Kuku ndiye kaumbika, duniani akaishi,
Kaumbwa hakuanguka, naumaliza **ubishi**,
Yai wewe ni mtoto, kuku kwako ndiye mama.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 102 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

5. Yai wewe bwamdogo, silete yako makeke,
Toka mwanzo ni mdogo, usije pigwa mateke,
Usishindane na gogo, epuka hasira zake,
Yai wewe ni mtoto, kuku kwako ndiye mama.

6. Kuku kapata uzima, kwa Mungu muumba vyote,
Alipewa na heshima, ajaze dunia yote,
Kaagizwa **himahima**, duniani akulete,
Yai wewe ni mtoto, kuku kwako ndiye mama.

7. Vifaranga watotoa, yai unacho**ringia**,
Fikiri wewe ni njia, si wewe uloanzia,
Si maarufu tambua, njia ni pakupitia,
Yai wewe ni mtoto, kuku kwako ndiye mama.

8. Wewe mtoto mdogo, yai nenda polepole,
Mheshimu mamdogo, uache kimbelembele,
Uepuke na mitego, siwe kama walewale,
Yai wewe ni mtoto, kuku kwako ndiye mama.

9. Kuku kapewa uwezo, kutaga na kutamia,
Yai iache mizozo, kuangua wajifia,
Unageuka uozo, **jalala**ni kuingia,
Yai wewe ni mtoto, kuku kwako ndiye mama.

10. Kifaranga ni cha kuku, wewe ni nguo ya mwili,
Bishia huko na huku, nguo haishiki mali,
Ni kuku amekupiku, uko hoi huna hali,
Yai wewe ni mtoto, kuku kwako ndiye mama.

11. Nasema kwa **ufasaha**, yai upate fahamu,
Yai iache mizaha, na kuharibu nidhamu,
Acha na huko kuhaha, usoni u**tabasamu**,
Yai wewe ni mtoto, kuku kwako ndiye mama.

12. Naona umeelewa, haki na wajibu wako,
Ndiwe uliyezaliwa, wacha zako chokochoko,
Kuku aliteuliwa, akawa mzazi wako,
Yai wewe ni mtoto, kuku kwako ndiye mama.

13. Hapa mwisho nasimama, yai nimekueleza,
Haya mafunzo ni mema, usije ukaya**beza**,
Kuku apewe heshima, yai acha kumzoza,
Yai wewe ni mtoto, kuku kwako ndiye mama.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 103 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Katika mzozo wa mwaka jana, yai alijigamba juu ya nini?
2. Yai alikujaje duniani?
3. Nini maana ya "Ni kuku amekupiku?"
4. Eleza jinsi kuku alivyotokea duniani.
5. Kitendawili cha yai na kuku kinateguliwaje?
6. Mwisho wa yai ni nini?
7. Nani anastahili heshima kati ya kuku na yai? Kwa nini?
8. Kama wewe ungekuwa mtunzi wa shairi ungeteguaje kitendawili hiki?
9. Umejifunza nini kutokana na shairi hili?

## Zoezi la pili: Msamiati

**Tunga sentensi mbili kwa kila neno.**

1. mzozo
2. tatua
3. maelewano
4. taharuki
5. ubishi
6. himahima
7. ringa
8. jalala
9. ufasaha
10. tabasamu
11. beza

## Zoezi la 3: Kazi ya kufanya

**Igiza na wenzako shairi ulilolisoma.**

## Zoezi la 4: Mazoezi ya lugha

**A. Andika vifupisho vya maneno yafuatayo:**

**Mfano:** Baraza la Kiswahili la Taifa - *BAKITA*

Kiwanda cha Uchapishaji cha Taifa - *KIUTA*

(i) Upungufu wa Kinga Mwilini____________

(ii) Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa____________

(iii) Jeshi la Kujenga Taifa____________

(iv) Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa____________

(v) Teknolojia ya Habari na Mawasiliano____________

(vi) Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Walioikosa____________

(vii) Umoja wa Michezo na Taaluma kwa Shule za Msingi Tanzania____________

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(viii) Chama cha Walimu Tanzania____________

(ix) Taasisi ya Elimu Tanzania____________

(x) Chama cha Netiboli Tanzania____________

(xi) Baraza la Sanaa la Taifa____________

(xii) Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania____________

## B. Unda nomino kutokana na vitenzi vifuatavyo:

**Mfano:** cheka - *kicheko, ucheshi, kichekesho, mchekeshaji, uchekeshaji*

| | |
|---|---|
| (i) imba | (vi) burudika |
| (ii) soma | (vii) cheza |
| (iii) shinda | (viii) chora |
| (iv) andika | (ix) lima |
| (v) lewa | (x) ongoza |

## C. Unda maneno mengine kwa kudondosha silabi moja.

**Mfano:** umiza – *uza*
tegua – *tegu*

| | |
|---|---|
| (i) kondoo | (vi) mlima |
| (ii) sabuni | (vii) shairi |
| (iii) chelewa | (viii) mtoto |
| (iv) mzinga | (ix) okoa |
| (v) maziwa | (x) kikombe |

## D. Andika sentensi zifuatazo kwa usahihi.

**Mfano:** Matango <u>maine</u> yameoza bustanini.
Matango <u>manne</u> yameoza bustanini.

(i) Ng'ombe inakula mahindi shambani.
(ii) Watoto zangu wanacheza nje.
(iii) Unga zimemwagika uwanjani.
(iv) Mimi ninakwendaga shuleni asubuhi.
(v) Wantiko ni lafiki yangu.
(vi) Tuliposafiri tulirara siku mbili njiani.
(vii) Aliponea chupachupa.
(viii) Alikula baazi ya matunda tu.
(ix) Moto yanawaka kwa kasi.
(x) Nitafika jana arasiri.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 105 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**E. Andika maneno yafuatayo kwa kirefu.**

**Mfano:** BAKITA - *Baraza la Kiswahili Tanzania*

mamaye - *mama yake*

(i) mamdogo ________
(ii) bwamdogo ________
(iii) babayo ________
(iv) dadaye ________
(v) TUKI ________
(vi) UKIMWI ________
(vii) TEHAMA ________
(viii) UMISETA ________
(ix) UMITASHUMTA ________
(x) BMT ________

## Zoezi la 5: Miundo

**Tunga sentensi mbili tofauti kwa kila muundo.**

1. ……………….. kidogo tu …………………

   **Mfano:** *Nikilima **kidogo tu**, ninachoka.*

2. ………….. ___na ……………

   **Mfano:** *Mimi ni**na** madaftari mengi.*

3. ……………. ___pigwa ………………..

   **Mfano:** *Yeye ali**pigwa** na Kido.*

4. ……………….. amba___ ……………………...

   **Mfano:** *Fedha **amba**zo zimeokotwa ni zangu.*

## Zoezi la 6: Kazi ya kufanya

**Jadiliana na wenzako maneno matano mengine ya Kiswahili yaliyoundwa kwa vifupisho. Andika virefu vya maneno hayo.**

## Zoezi la 7: Utungaji

**Andika kifungu cha habari chenye maneno mia moja (100) kuhusu michezo ya shuleni kwenu.**

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 106 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Tatu

## Ufupisho

### Utangulizi

*Katika sura hii, utasoma hadithi ya maisha ya kuku. Utajifunza kufupisha habari bila kupotosha maana kwa kuzingatia alama za uandishi. Umahiri huu utakusaidia katika uandishi wa ripoti na ufupisho wa maandiko mbalimbali katika maisha yako.*

### Fikiri



1. Ulishawahi kusoma hadithi yoyote?
2. Unaweza kuielezea hadithi hiyo kwa ufupi?

### Ufahamu

*Soma hadithi ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

**Maisha ya kuku**

Koba ni nchi iliyopo katika Bara la Hekaheka. Wakazi wa nchi hiyo ni wanyama wa aina mbalimbali kama vile panya, vicheche, nguchiro, vyura, vinyonga na ndege wa aina mbalimbali. Kuku ni miongoni mwa ndege wanaoishi nchini humo. Kuku hawana uwezo wa kuruka na kupaa angani kama ndege wengine. Kwa muda mrefu, kuku wamekuwa wakionewa na baadhi ya wanyama. Walikumbwa na **dhiyaa** isiyo na **kifani**. Vifaranga wa kuku walikamatwa na kuuawa mara kwa mara bila hatia. Hivyo, uzao wa kuku ulikuwa ukipukutika kwa kasi. Katika jamii ya kuku, alikuwepo jogoo maarufu aliyejulikana kwa jina la Mzee Jimbi. Mzee Jimbi alionekana kuwa na hekima na busara. Hivyo, ali**tawazwa** na wazee vikongwe wa jamii yake kuwa mfalme wa Kuku.

Siku moja Mzee Jimbi aliitisha mkutano wa Kuku wote hapo nchini kujadili mambo yanayowasibu. Kuku wote walimiminika kwenye mkutano. Mfalme alimruhusu kila Kuku aseme na kueleza kero zake. Mkutano ulikuwa mkubwa sana. Kuku vikongwe nao hawakutaka kusimuliwa. Kila mmoja aliweza kufika ili kujua hatima ya mateso ya muda mrefu yanayoikabili jamii yote ya kuku.

Baada ya kero zote kuwasilishwa, mfalme aliwaeleza Kuku kuwa haya yote

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 107 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

yanatupata kwa sababu ya umaskini na kukosa elimu. Kuku hana mtetezi katika vyombo vya sheria na hawezi kujitetea hata kama ameonewa. Hali hii inatokana na kutoifahamu sheria. Ni dhahiri kwamba, hata pale Kuku aliposimama mahakamani dhidi ya Mwewe aliyepora vifaranga wake, Mwewe alishinda kesi.

Mkutano uliendelea na mwafaka ukapatikana. Azimio la mkutano lilikuwa kupendekeza vijana watakaosomeshwa na jamii ya kuku kupitia kodi na harambee za wananchi. Mkutano uliwapendekeza vijana wawili **hodari** watakaosomeshwa kwa kodi za wananchi. Vijana hao ni Chogi na Wakili. Bibi Kikongwe, kwa kuafiki maazimio, alisimama na kusema, “Kofi hazilii ila kwa viganja viwili.” Aliwapongeza wote walioshiriki katika mkutano huo. Pia, aliwapongeza vijana waliopendekezwa na mkutano. “Vijana hawa wataitumia elimu watakayoipata, ili kuleta ukombozi na tumaini hapa nchini,” alisema bibi huyo.



Chogi alipewa ufadhili wa kusomea mafunzo ya kijeshi kutokana na maazimio ya mkutano. Wakili naye alipelekwa **ng’ambo** kusomea sheria. Kila kijana ali**dhamiria** kutekeleza jukumu alilokabidhiwa. Hii haikuwa kazi ndogo. Wakati wote wa masomo, Chogi na Wakili walitambua kazi kubwa iliyopo mbele yao. Walisoma kwa bidii.



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 108 26/07/2021 16:26
FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Wakiwa masomoni, kila mmoja alikumbuka jinsi ndugu zake walivyoonewa na baadhi ya wanyama kama vile mwewe, vicheche, kipanga na nguchiro. Uonevu huu uli**kithiri** na kuvuka mipaka. Hali hii iliwafanya Chogi na Wakili wasome kwa bidii.

Walipokamilisha mafunzo, walirejea kisiwani tayari kwa kazi. Baada ya kufanya **utafiti**, vijana hawa walimshauri Mfalme Kihero na jamii yote ya kuku kuhama kutoka nchi ya Koba na kufanya makazi katika nchi ya Utando. Walitaka waishi na Buibui ambao tayari walikuwa wanaishi nchini Utando. Waliamini kwamba, wakiungana na Buibui, hakuna adui atakayewashinda tena. Utando ni miongoni mwa nchi zilizopo katika Bara la Hekaheka.

Wakiwa nchini Utando, walijenga shule, hospitali pamoja na vituo vya afya. Walianzisha mashirika ya misaada na ajira nyingi zikapatikana. Hakika walishuhudia ukweli wa maneno ya wahenga yasemayo, “Baada ya dhiki, faraja.” Faida ya kusoma ikaanza kuonekana. Kila Kuku aliyekuwa na ujuzi, alipata **ajira** na wengine walifungua miradi mingi ya ujasiriamali. Ajira zilizopewa kipaumbele ni pamoja na jeshi, uhandisi, ualimu, sheria, utabibu na usanifu majengo.

Tangu zamani, Buibui ni rafiki mkubwa wa Kuku. Kuku na Buibui walishakula yamini ya kutodhulumiana. Wanaishi pamoja kama ndugu. Buibui ana ujuzi wa usanifu majengo. Hivyo, Buibui walishirikiana na Kuku kujenga **ngome** kuzunguka miji yote. Mitambo ya ulinzi iliimarishwa.

Chogi alikusanya vijana wakakamavu ndani ya jamii ya kuku na wengine kutoka jamii ya buibui ili kupata mafunzo ya kijeshi. Walijifunza mbinu za kivita na mafunzo ya uzalendo kwa vitendo. Aliimarisha vikosi vya ulinzi. Aliweka ulinzi katika kila lango la kuingilia. Hakuna mgeni aliyeruhusiwa kuingia katika nchi ya Utando bila kibali. Kibali kilitolewa kwa masharti makubwa.

Maisha ya Kuku yakawa ni ya furaha na amani. Elimu ikawa silaha muhimu sana kwa Kuku katika kupambana na maadui. Jamii yoyote inayothamini na kuwekeza katika elimu, haiwezi kumwogopa adui. Elimu huifanya jamii iheshimike kama inavyoonekana kwa Kuku nchini Utando.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 109 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Taja majina ya nchi zilizotajwa kwenye hadithi hii? Eleza sifa zake.
2. Nchi hizo zilikuwa katika bara gani?
3. Kwa mujibu wa habari uliyosoma mfalme wa kuku anaitwa nani?
4. Taja vijana wawili waliopata ufadhili wa kusoma.
5. Kuku aliyefadhiliwa kusomea mafunzo ya kijeshi anaitwa nani?
6. Rafiki mkubwa wa kuku ni nani?
7. Nchi ya mfano wa kuigwa katika ulimwengu wa wanyama inaitwaje?
8. Taja maadui wawili wa kuku.
9. Kuku walipohama kutoka nchi ya Koba, walielekea nchi gani?
10. Kwa mujibu wa habari uliyosoma, kati ya kuku na mwewe ni nani alipendelewa na mahakama?
11. Umejifunza nini kutokana na habari uliyoisoma?

## Zoezi la pili: Msamiati

### Eleza maana ya misamiati ifuatayo:

1. dhiyaa
2. kifani
3. tawazwa
4. hodari
5. ng'ambo
6. dhamiria
7. kithiri
8. utafiti
9. ajira
10. ngome

## Zoezi la 3: Miundo

### Tunga sentensi mbili kwa kila muundo.

1. ……………… palipo na ………………………………
   **Mfano:** *Kila **palipo na** moshi pana moto.*

2. ……………… kati ya …………………
   **Mfano:** *Joni atakwenda shuleni **kati ya** saa sita na saa saba.*

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 110 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. ……………… nyuma ya ………………………………
**Mfano:** *Mtoto hapendi kukaa **nyuma ya** pazia.*

4. …………….. kilicho_____ ………………………………….
**Mfano:** *Kikombe **kilicho**vunjika kimetupwa jalalani.*

5. ………………. vilivyo____ ………………………………
**Mfano:** *Viatu **vilivyo**potea vilinunuliwa bei ghali.*

6. ………………. iliyo____ …………………………..
**Mfano:** *Kalamu **iliyo**potea imepatikana leo asubuhi.*

7. ……………… palipo_____ ………………………
**Mfano:** *Mahali **palipo**bomoka pamejengwa.*

8. ………………. miongoni mwa ……………………
**Mfano:** *Jumanne ni **miongoni mwa** wanafunzi waliofaulu mtihani.*

9. ……………… ndani ya ……………………………
**Mfano:** *Panya ameingia **ndani ya** shimo.*

## Zoezi la 4: Mazoezi ya lugha

### A. Chagua jibu sahihi katika maswali yafuatayo:

(i) Yeye ________ shahada ya uhandisi.
(a) alitunukiwa
(b) walitunukiwa
(c) tulitunukiwa
(d) vilitunukiwa

(ii) Wao walijikita katika kuimarisha ulinzi. Wao ni aina gani ya neno?
(a) nomino
(b) kiwakilishi
(c) kiunganishi
(d) kihisishi

(iii) Elimu ni mkombozi wa jamii nyingi. Wa ni aina gani ya neno?
(a) kivumishi
(b) kihisishi
(c) kiunganishi
(d) kihusishi

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 111 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(iv) Mama amekata chungwa. Mama ni ________

(a) mtenda
(b) mtendewa
(c) mtendesha
(d) mtendeka

(v) Mahindi yamekobolewa vizuri. Mahindi ni ________

(a) mtendwa
(b) mtenda
(c) mtendeka
(d) mtendesha

(vi) Watoto wamebadilishana viatu vyao. Katika sentensi hii watenda ni ________

(a) mwalimu
(b) viatu
(c) wote
(d) watoto

(vii) Mwaka ujao tutaingia Darasa la Saba. Sentensi hii iko katika wakati gani?

(a) wa sasa
(b) uliopo
(c) uliopita
(d) ujao

(viii) Nchi ya Koba________katika bara la kufikirika liitwalo Hekaheka.

(a) kipo (b) lipo (c) yako (d) ipo

(ix) Zifuatazo ni hatua za kuzingatia wakati wa kufanya ufupisho isipokuwa .........

(a) Kusoma habari yote na kuitafakari
(b) Kubaini wahusika na uhusika wao katika habari
(c) Kurudia kusoma habari kwa mara ya pili
(d) Kuandika neno hadi neno kutoka kwenye habari

(x) Wageni wamesalimiana kwa kupeana mikono. Wageni ______

(a) wametendewa
(b) wametendeka
(c) wametendwa
(d) wametendeana

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 112 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**B. Jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuandika NDIYO kama maelezo ni ya kweli na HAPANA kama maelezo ya sentensi si kweli.**

(i) Ufupisho ni sawa na muhtasari. ________

(ii) Soma habari yote kwa umakini ili kufanya ufupisho. _______

(iii) Watu wakisoma ufupisho, wanapata stadi za kutatua matatizo ya jamii. ______________

(iv) Ufupisho unatumia maneno mengi ili kueleza wazo kuu. ______

(v) Ufupisho unaelezea wazo la mwanzo kwa kifupi. __________

(vi) Ufupisho ni lazima uwe katika aya moja tu. __________

(vii) Ufupisho husaidia kutunza kumbukumbu. _________

(viii) Wazo kuu katika ufupisho hupatikana katika aya ya mwisho. ______

(ix) Ufupisho ni sawa na hitimisho. ________

(x) Kuna hatua muhimu za kufanya ufupisho. ______

**C. Kanusha sentensi zifuatazo:**

**Mfano:** Jogoo wanataga mayai.
*Jogoo hawatagi mayai.*

(i) Kuku wanajitambua.

(ii) Maisha ya kuku yanavutia ndege wengine.

(iii) Kuku anaweza kupambana na kicheche.

(iv) Swea ni kifaranga mdadisi.

(v) Koba ni kisiwa cha amani.

(vi) Kuku wana jeshi imara.

(vii) Wakili alipenda kusoma vitabu na magazeti.

(viii) Vijana wana umoja.

(ix) Amejenga kiwanda cha kusindika samaki.

(x) Buibui atasanifu majengo.

**D. Tumia maneno yafuatayo kujaza nafasi zilizoachwa wazi.**

| |
|---|
| **dhiyaa, hadithi, mkato, thubutu, msamiati, aya, alama ya kuuliza, kufupisha, alama ya mshangao, yamini** |

(i) Huonesha pumziko fupi wakati wa kusoma habari au kisa ________

(ii) Kifungu cha maneno katika habari kinachobeba wazo moja _________

(iii) Kuandika kisa au habari ndefu kwa kupunguza maneno _______

(iv) Hutumika kuonesha hisia ___________

(v) Hutumika kuuliza swali kwenye sentensi __________

(vi) Simulizi yenye mvuto kusikiliza ____________



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 113 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(vii) Neno linalohitaji kutafutiwa maana ____________
(viii) Kiapo cha kutokwenda kinyume na maridhiano ____________
(ix) Hali ya kuwa na mateso au unyonge ____________
(x) Jaribu kufanya jambo ____________

## E. Pigia mstari jibu sahihi kwa kila swali.

**Mfano:** Mimi na baba________hadithi kwenye gazeti.
(anasoma, wanasoma, <u>tunasoma</u>)
Mvua iliyonyesha jana, ________ daraja.
(<u>ilibomoa</u>, ilibomoka, ilibomokea, ilibomokewa)

(i) Mtoto alikwenda sokoni _______ miguu.
(na, kwa, ya, wa)

(ii) Jiwe lilidondoka _________ maji.
( juu ya, mbele ya, ndani ya, ndani mwa)

(iii) Watoto__________ ni wapole sana.
(yangu, chao, wangu, vyangu)

(iv) Babu ____________ maembe jana jioni.
(anakula, alikula, atakula, amekula)

(v) Kesho baba ___________ mjomba salamu za pongezi.
(atamtumia, alimtumia, walimtumia, akimtumia)

(vi) Mfalme ___________ mkutano wa kuku wote pale kisiwani.
(aliitwa, aliita, aliitisha, aliitishwa)

(vii) Panya _____ mnyama mjanja katika jamii ya wanyama.
(ndiyo, ndilo, ndicho, ndiye)

(viii) Wingi wa neno shule ni _________ .
(mashule, kashule, shuleni, shule)

(ix) Kuku hawakuonewa ___________ na mnyama mwingine tena.
(kamwe, ila, thubutu, punde)

(x) Mnubi ___________ shuleni sasa hivi.
(akatembea, alikwenda, huenda, anakwenda)

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 114 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**F. Panga herufi zilizochanganywa ili kuunda neno sahihi.**

**Mfano:** lemui - elimu
kiof - kifo

(i) matachu ____________
(ii) kimimani ____________
(iii) ifna ____________
(iv) bututhu ____________
(v) mwaek ____________
(vi) rikithi ____________
(vii) jumihi ____________
(viii) niami ____________
(ix) omeng ____________
(x) ng'maob ____________

## Zoezi la 5: Utungaji

**A. Panga hatua za kufanya ufupisho kwa mtiririko sahihi.**

(i) Kusoma habari tena kwa mara ya pili
(ii) Kupitia ufupisho wa habari ili kuondoa makosa.
(iii) Kuandika ufupisho wa habari
(iv) Kusoma habari yote ili kubaini mawazo muhimu
(v) Kubaini wahusika katika habari

**B. Fupisha hadithi ya Maisha ya kuku kwa maneno kati ya sitini (60) na themanini (80).**

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 115 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Nne

## Kumbukumbu za mikutano

### Utangulizi

*Katika sura hii, utajifunza namna ya kuandika kumbukumbu za mikutano. Pia, utajifunza elimu ya afya na uzazi na utafanya mazoezi mbalimbali ya lugha. Umahiri huu utakuwezesha kuandika kumbukumbu za mikutano na kutatua changamoto anuai za afya na uzazi.*

### Fikiri



1. Je, uliwahi kuhudhuria mkutano wowote?
2. Mkutano huo ulifuata utaratibu gani?

### Ufahamu

*Soma hadithi ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

**Kisiwa cha Masaibu**

Kisiwa cha Masaibu kilikuwa baharini, mbali kabisa na bara. Wavuvi wengi wa maeneo ya bara walifika kwa taabu katika kisiwa hicho. Wavuvi wachache walioweza kukifikia, walisimulia mambo mengi ya kutisha yanayowahusu wakazi wa kisiwa hicho. Walidai kuwa wakazi wa Masaibu walikuwa na tabia zisizofanana na za watu wa jamii nyingine.

Siku moja kulitokea **dhoruba** kali baharini. Ma**nahodha** walishindwa kuongoza vizuri vyombo vyao. Vyombo vingi walivyosafiria wavuvi siku hiyo vili**enda mrama**. Kijana mmoja aitwaye Janja naye siku hiyo aliongozana na wenzake kwenda baharini kuvua samaki. Mashua yao ilipepesuka kwa upepo mkali uliokuwa ukivuma. Janja na wenzake waliingiwa na hofu kubwa. Kila mmoja alishikilia roho mkononi akimwomba Mungu wake awaepushe na hatari ile.

Dhoruba ile ilidumu kwa kitambo kirefu hadi giza likatanda. Janja na wenzake hawakujua tena walikokuwa wakielekea. Mara, wakaona moto kwa mbali. Mashua yao ilikuwa ikipeperushwa kuelekea wasikokujua. Baada ya muda, mashua yao iligota nchi kavu. Ingawa hawakujua mahali walipokuwa, Janja na wenzake walifurahi na kumshukuru Mungu kwa kuwaokoa.

Kwa mbali, waliweza kusikia sauti zinazoshabihiana na sauti za watu, kisha wakasikia jogoo anawika. “Kumbe kunakaribia kukucha!” Walisema. Janja na wenzake wakapata matumaini kwamba mahali hapa kuna makazi ya watu.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 116 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Njaa ilikuwa inawa**furukuta** kwelikweli. Wali**kata shauri** waanze kutafuta mahali yalipokuwa makazi ya watu. Walitoka pale ufukweni na kuelekea nchi kavu. Kadiri walivyosonga mbele, ndivyo walivyozidi kusikia sauti mbalimbali. Kulikuwa na vilio, mayowe, na kelele mbalimbali. Ingawa hawakujua sababu ya vilio vile, hawakutishika. Waliamua kuelekea upande huohuo. Waliamini kuwa huko wangeonana na watu ambao wangewasaidia kutoka katika dhiki waliyokuwa nayo.

Baada ya mwendo mfupi, walisikia mtu akikohoa kikohozi kikavu. Walishtuka na kufurahi kwa wakati mmoja kuona kuwa tayari wamefika mahali palipo na watu. Janja akajikoholesha ili mtu huyo awasikie. Mara, wakasikia sauti ikiuliza, "Ni nani huyo?" Ilikuwa sauti ya mtu mwanaume mzee sana. Janja akamjibu, "Ni sisi."

"Nyie ni akina nani?" Sauti iliuliza tena.

"Sisi ni akina Janja."

"Mnatoka wapi?" Sauti ile iliuliza tena.

"Tulikuwa baharini tunavua samaki. Dhoruba ikapeperusha mashua yetu hadi tukagota hapa. Hapa ni wapi?" Janja aliuliza.

"Hapa panaitwa Masaibu. Hapa ni kisiwani," Sauti ile ilijibu.

Akina Janja waliposikia kwamba mahali walipokuwa ni kisiwani Masaibu, walianza kutetemeka. Kwa muda mrefu, wamekuwa wakisikia madhila yanayowapata watu wanaokwenda kisiwani hapo. Waliingiwa na **kimuyemuye**. Furaha yote waliyokuwa nayo ikawatoka. Mmoja wao akawaambia wenzake, "Tukimbie! Mahali hapa si salama! Tutateswa!"

Mtu yule akawatuliza na kuwaambia, "Msikimbie! Hakuna mtu atakayewatesa. Watu wakisikia habari za ujio wenu, watafurahi sana. Tumeteseka kwa muda mrefu sana hapa kisiwani. Tafadhali, msiondoke!"

Maneno hayo yaliwa**tia moyo** upya. Baadaye yule mtu alitoka kichakani na mkongojo wake. Wakati huo, nuru ya jua ilianza kuonekana kwa mbali. Yule mtu alionekana kuwa mgonjwa wa siku nyingi. Alikuwa amekondeana, akitembea kwa kupepesuka.

Janja na wenzake walimwonea huruma mtu huyo. Janja alimsogelea na kumtazama vizuri usoni. Macho yake yalikuwa yameingia ndani. Janja akang'amua kuwa mtu huyo alionekana kama mzee ingawa alikuwa ni kijana. **Maradhi** yalikuwa yamemdhoofisha.

Mara kwa mara, mtu yule alisikika aki**gugumia** kwa maumivu makali ya ugonjwa aliokuwa nao. Hata hivyo, ali**jikaza kiume** ili kujibu maswali mbalimbali aliyoulizwa na akina Janja kuhusu kisiwa hicho.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Janja alimshangaa mtu yule kwa kuwa alishikilia kijiti kwa muda wote. Mara, akamwona anapandisha juu shati lake na kupitisha mkono wenye kijiti mgongoni. Ngozi yake ilikuwa na ukurutu mwingi. Hapo ndipo Janja akajua kazi ya kile kijiti. Kumbe alikitumia kujikuna!

Walipoona njaa inazidi kuwauma, Janja na wenzake walimuuliza mwenyeji wao mahali ambapo wangeweza kupata chakula wakati huo. Aliwaambia kuwa migahawa yote ilikuwa bado imefungwa; hivyo, akawaelekeza mahali lilipo shamba lake la mihogo.

Janja na wenzake walimshukuru sana na kuondoka harakaharaka kuelekea huko. Sehemu nyingi walizopita kisiwani hapo, zilikuwa na harufu kali. Wakahisi kuwa wakazi wengi wa kisiwa hicho hawakuwa na vyoo.

Walipofika, walivamia shamba kwa fujo na kuanza kuchimba mihogo, kisha, walianza kui**fakamia** wakaila na kusaza. Wakati huo, jua lilikwishachomoza na miale yake iliuangaza uso wa dunia. Waliweza kuona vizuri **mandhari** ya kisiwa hicho. Kilikuwa na ardhi nzuri na uoto wa kupendeza. Walifurahi sana kufika mahali hapa. Walibeba mihogo waliyobakiza, wakaanza safari ya kurudi nyumbani kwa mwenyeji wao.

Njiani, walikutana na kundi la watu wakienda makondeni. Waliwaamkia na kupishana nao. Wengi wao walikuwa wanawake. Baada ya muda mfupi, walikutana na kundi lingine la watu. Walikuwa wanalia kwa huzuni. Bila shaka, walielekea msibani. Waliendelea kupishana na watu wengine wakati wanapita kwenye makazi ya watu.

Mara, Janja akawauliza wenzake, "Jamani, mmegundua nini kwa hawa watu tunaopishana nao?" Mmoja wao akajibu, "Mimi naona tunapishana na makundi ya watu. Wengi wao ni wanawake." Janja akasema, "Umesema kweli." Akaongeza kusema, "Ukiwachunguza vizuri wanawake hao, utaona kuwa ni wa marika mbalimbali. Kuna wasichana wadogo na watu wazima. Wanachonishangaza, kila mmoja wao anaonekana amebeba mtoto mgongoni. Kama hana mtoto mgongoni, utaona ni mjamzito."

Walipokaribia kufika nyumbani kwa mwenyeji wao, walishtuka kuona umati wa watu wakiwa nje ya kijumba chake. Jasho jembamba lilianza kuwatoka. Walihisi kuwa ugonjwa ulimzidi mwenyeji wao, akaaga dunia. Nguvu ziliwatoweka, miguu ikawalegea, hatua wakaziona nzito. Walipokumbuka wema aliowafanyia, machozi yalianza kuwatoka.

Wakati wakiwaza hivyo, waliona mlango wa kijumba chake unafunguliwa, wakamwona mwenyeji wao akijikongoja kutoka ndani. Walishusha pumzi ndefu kwa faraja kuu. "Mungu ni mwema!" alisema Janja.

Walipofika, waliwaona wale watu wakiwa na nyuso za furaha. Wote walisimama na kuwalaki akina Janja kwa mioyo mikunjufu. Mmoja wao aliyeonekana kuwa kiongozi wao, alisimama na kuanza kuwaeleza sababu iliyowaleta hapo. Kiongozi huyo alitoa mfukoni mwake bahasha iliyokuwa na karatasi mbili.



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 118 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Aliwaeleza akina Janja kuwa bahasha hiyo ililetwa kisiwani hapo na watu wasiowafahamu. Watu hao walipofika tu u**fukwe**ni, waliirusha bahasha hiyo nchi kavu na kuondoka haraka kwa boti yao.

Kiongozi huyo aliwaeleza kuwa miaka mitatu ilikuwa imepita tangu bahasha hiyo ilipoletwa kisiwani hapo. Hata hivyo, hadi sasa, hawakujua maana ya kile kilichoandikwa katika karatasi zile. Alisema kuwa wakazi wote wa kisiwa hicho hawakujua kusoma na kuandika. Hapakuwa na shule kisiwani hapo. Janja aliposikia maneno hayo, alishuku iwapo yalikuwa ya kweli. Akanyoosha mkono wake akitaka apewe nafasi ya kuuliza jambo ili kuondoa wasiwasi aliokuwa nao. Kiongozi alimruhusu, Janja akasimama na kusema, "Ndugu zangu, Waswahili wanasema, 'Kuuliza si ujinga.' Kama nitawakosea kwa maneno nitakayosema, naomba mniwie radhi. Tulipokuwa tunatoka shambani, tumepita karibu na duka dogo hapo juu. Nimeona madaftari na kalamu zinauzwa pale dukani. Kama ni kweli watu wote wa hapa kisiwani hawajui kusoma na kuandika, kwa nini vitu hivyo vinauzwa madukani?"

Wale watu waliposikia hivyo, walicheka kwa aibu. Kiongozi wao akasimama na kujibu swali la Janja, "Ndugu yetu, haya ninayoyasema ni ya kweli tupu. Yale madaftari, sisi twayanunua kwa ajili ya kusokotea tumbaku na kuvuta na kalamu zinapendwa na hawa akina mama. Huchovya wino wake na kupamba kucha zao." Huyu mwenyeji wenu, Bwana Masumbuko, ni shahidi yangu."

Janja na wenzake walivunjika mbavu waliposikia habari ile. "Ama kweli, kutembea ni kuona mengi!", walisema kimoyomoyo.

Waliendelea kuwauliza wenyeji wao maswali ya hapa na pale, nao wakawajibu kwa ukamilifu. Waliwapa taarifa mbalimbali kuhusu kisiwa chao. Walisema kuwa matatizo mengi yaliwaandama. Hapakuwa na hospitali kisiwani hapo. Watu wengi waliumwa na kupoteza maisha kwa kukosa huduma za afya. Wajawazito wengi walifariki wakati wa kujifungua kwani walijifungulia majumbani. Wasichana wengi wa rika la **balehe** walibeba mimba na kushindwa kujifungua salama.

Kisiwani hapo kulikuwa na magonjwa mengi ya kuambukiza. Kulikuwa na kuhara, kipindupindu, kifuakikuu, UKIMWI na magonjwa mengine ya zinaa. Vilevile, hapakuwa na huduma nyingine muhimu kama vile barabara, umeme na maji safi na salama.

Kwa kuwa watu wengi walikuwa wakisikia habari za kutisha kuhusu Kisiwa cha Masaibu, waliogopa kutia nanga kisiwani hapo. Kwa hiyo, wakazi wa kisiwa hicho walikosa wageni kwa muda mrefu sana. Walikosa pia fursa na huduma mbalimbali ambazo zingeletwa na wageni. Walijuta sana kwa tabia zao mbaya walizowafanyia wageni siku za nyuma.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Waliwaomba sana akina Janja wawasomee mambo yaliyoandikwa kwenye karatasi zile. Janja alisimama na kupokea bahasha ile kutoka kwa kiongozi na kukuta kuna kumbukumbu za mkutano. Aliifungua na kutoa karatasi zile. Haya ndiyo maneno yaliyokuwa yameandikwa. Akayasoma kwa sauti.



**Halmashauri ya Wilaya ya Tupendane**

**Kumbukumbu za Mkutano wa Baraza la Madiwani**

**Mahali pa mkutano: Ukumbi wa Mkutano wa Halmashauri**

**Tarehe ya mkutano: 5/6/2016**

**Majina ya waliohudhuria**

1. Bw. Juhudi D. Maendeleo – Mwenyekiti wa Baraza la Madiwani, Mwenyekiti wa mkutano
2. Bi. Zuwena R. Mchapakazi – Diwani, Katibu wa mkutano
3. Bi. Esta G. Maarifa – Diwani, Mjumbe
4. Bw. Abdala M. Msemakweli – Diwani, Mjumbe
5. Bw. Kazimoto K. Mshindi – Diwani, Mjumbe
6. Bi. Huruma H. Nguvumali – Diwani, Mjumbe



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 120 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

7. Bw. Furaha F. Kaulimali – Diwani, Mjumbe

**Majina ya wasiohudhuria kwa taarifa**

1. Bw. Fadhili Z. Mpendawatu – Diwani, Mjumbe (Ruhusa ya kumpeleka mkewe kliniki)
2. Bi. Imani K. Utubora – Diwani, Mjumbe (Ruhusa ya kumpeleka mtoto kwenye chanjo)
3. Bi. Rehema M. Maliyamungu – Diwani, Mjumbe (Ruhusa kwa ziara ya mafunzo)

**Majina ya wasiohudhuria bila taarifa**

1. Bi. Fitina W. Chakupewa
2. Bw. Lupa Z. Utuwao

**Ajenda za mkutano**

1. Kufungua mkutano
2. Kujadili kuhusu maeneo ambayo bado yako nyuma kimaendeleo
3. Mengineyo
4. Kufunga mkutano

**1. Kufungua mkutano**

Mkutano huu uliitishwa na Mwenyekiti wa Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Tupendane. Mwenyekiti alifungua mkutano saa 2:00 asubuhi. Aliwakaribisha wajumbe wote kwenye mkutano. Aliwaomba wajumbe kumchagua katibu wa mkutano huo ili aandike kumbukumbu za mkutano.

**2. Kujadili kuhusu maeneo ambayo bado yako nyuma kimaendeleo**

Mwenyekiti aliwaarifu wajumbe kuhusu kuwepo maeneo kadhaa katika wilaya hiyo ambayo bado yalikuwa nyuma sana kimaendeleo. Baadhi ya maeneo hayo ni Kijiji cha Fofofo na Kisiwa cha Masaibu. Baada ya majadiliano marefu, wajumbe wa mkutano walikubaliana kuwa Halmashauri ya Wilaya iwaandikie barua viongozi wa maeneo hayo.

**3. Mengineyo**

Wajumbe wa mkutano walimpongeza mwenyekiti kwa mawazo yake mazuri yanayolenga kuleta ustawi kwa watu wote katika Halmashauri hii.

**4. Kufunga mkutano**

Mwenyekiti alifunga mkutano saa 6:28 mchana na kuwatakia wajumbe wote wa mkutano huo utekelezaji mwema wa majukumu yao.

| | |
|---|---|
| J. Maendeleo 21/6/2016 | Z. Mchapakazi 21/6/2016 |
| Juhudi D. Maendeleo | Zuwena R. Mchapakazi |
| Mwenyekiti | Katibu |

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 121 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Janja alipomaliza kuwasomea kumbukumbu hizo za mkutano, alishauri, "Ndugu zangu, mashua tuliyosafiria imepata hitilafu kwa dhoruba kali baharini. Ninawaomba tusaidiane ili tuivuke bahari hii, tufike bara. Tutaongozana na wawakilishi wenu hadi ofisini kwa mwenyekiti wa baraza la madiwani. Hapo watawapatia taarifa hizo zilizopotea na maelekezo mengine."

Watu wote walimpigia makofi Janja kwa mawazo yake mazuri. Mawazo yake yalipitishwa. Kuona hivyo, Janja aliinama, akamnong'oneza yule kiongozi, "Wakati wa kwenda, tuondoke na Masumbuko ili akatibiwe huko." Watu wote walifurahishwa na ujio wa akina Janja katika kisiwa chao. Walianza kuona mwanga wa namna ya kutatua matatizo yao.

## Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Hadithi uliyoisoma inahusu nini?
2. Je, kisiwa cha Masaibu kiko wapi?
3. Kwa nini watu wengi waliogopa kwenda kwenye Kisiwa hicho?
4. Janja na wenzake walifikaje kwenye kisiwa cha Masaibu?
5. Kwa nini maeneo mengi ya Kisiwa cha Masaibu yalikuwa na harufu kali?
6. Je, kulikuwa na hospitali ngapi kisiwani hapo?
7. Kwa nini wanawake wengi wa Masaibu walifariki wakati wa kujifungua?
8. Kwa nini Janja alimwomba kiongozi wa kisiwa waondoke na Masumbuko?
9. Kulikuwa na taarifa gani kwenye karatasi iliyosomwa na Janja?
10. Taja vipengele mbalimbali vinavyounda kumbukumbu za mikutano.

## Zoezi la pili: Msamiati

### Tunga sentensi kwa kila neno.

1. dhoruba
2. nahodha
3. furukuta
4. kimuyemuye
5. maradhi
6. gugumia
7. fakamia
8. mandhari
9. fukwe
10. balehe

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 122 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 3: Nahau

**Toa maana ya nahau zifuatazo, kisha zitumie kutunga sentensi.**

1. tia nanga
2. enda mrama
3. kata shauri
4. tia moyo
5. jikaze kiume

## Zoezi la 4: Vitendawili

**Malizia vitendawili vifuatavyo, kisha vitegue. Andika jibu la kitendawili hicho kwenye mabano mraba.**

**Mfano:** Saa yangu haijasimama tangu itiwe ufunguo. [*MOYO*]

1. Akibeba watoto wake hawezi ____________. [ __________ ]
2. Akitembea huringa hata akiwa ___________. [ __________ ]
3. Huchagui wala ______________. [ __________ ]
4. Hesabu yake haina ______________. [ __________ ]
5. Kwa mfalme, hawa wanatoka na hawa ________. [ __________ ]
6. Maskini huyu hata umchangie namna gani ________. [ ______]
7. Nimelala ila nachungulia ___________. [ __________ ]
8. Wanameza watu jua ___________. [ __________ ]
9. Nimeotesha mti wangu ila ________. [ __________ ]
10. Watoto wana mikia na wakubwa ______. [ __________ ]

## Zoezi la 5: Mazoezi ya lugha

**A. Jaza herufi zinazoendana na namba hizi ili kupata maneno sahihi.**

| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Z** | **Y** | **W** | **V** | **U** | **T** | **S** | **R** | **P** | **O** | **N** | **M** |
| **2** | **4** | **6** | **8** | **10** | **12** | **14** | **16** | **18** | **20** | **22** | **24** |

| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **L** | **K** | **J** | **I** | **H** | **G** | **F** | **E** | **D** | **CH** | **B** | **A** |
| **26** | **28** | **30** | **32** | **34** | **36** | **38** | **40** | **42** | **44** | **46** | **48** |

**Mfano:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 48 | 38 | 4 | 48 |
| *A* | *F* | *Y* | *A* |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(i)

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 24 | 28 | 10 | 12 | 48 | 22 | 20 |
| | | | | | | |

(ii)

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 16 | 48 | 24 | 48 | 22 | 32 |
| | | | | | |

(iii)

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 28 | 48 | 12 | 32 | 46 | 10 |
| | | | | | |

(iv)

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 22 | 20 | 24 | 32 | 22 | 20 |
| | | | | | |

(v)

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 12 | 10 | 22 | 36 | 20 |
| | | | | |

(vi)

| | | | |
|---|---|---|---|
| 6 | 40 | 6 | 40 |
| | | | |

(vii)

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 28 | 32 | 40 | 26 | 40 | 2 | 32 |
| | | | | | | |

(viii)

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 28 | 32 | 30 | 48 | 22 | 48 |
| | | | | | |

(ix)

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 2 | 48 | 6 | 48 | 42 | 32 |
| | | | | | |

(x)

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 40 | 26 | 32 | 24 | 10 |
| | | | | |

**B. Badili sentensi zifuatazo ziwe katika wakati uliopo na wakati uliopita.**

**Mfano:** Mvua italeta neema kijijini kwetu.

*Mvua inaleta neema kijijini kwetu. [Wakati uliopo]*

*Mvua ilileta neema kijijini kwetu. [Wakati uliopita]*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(i) Mbuga za wanyama zitaleta watalii wa kutosha.
(ii) Barua ya dada tutaipata kwa njia ya posta.
(iii) Mtoto atainama kuokota funguo.
(iv) Mazao yatahifadhiwa ghalani.
(v) Wakulima watauza korosho zao kwa bei nzuri.
(vi) Bibi afya atatuelimisha kuhusu afya ya uzazi.
(vii) Ngalawa itayumbayumba kwa sababu ya mawimbi makubwa.
(viii) Shangazi atapeta mahindi ili kuondoa pumba.
(ix) Kurunzi itatusaidia kupata mwanga wakati wa giza.
(x) Mwewe atawanyakua vifaranga wa kuku wetu.

**C. Andika neno lingine linalofanana na haya yafuatayo:**

**Mfano:** kuhofu, kutaharuki, kutetemeka, <u>kuogopa</u>

(i) chopeka, ingiza, chomeka, ______________
(ii) nderemo, vifijo, chereko, ___________
(iii) sumbua, kasirisha, udhi, ____________
(iv) tokeza, onekana, ibuka, _____________
(v) mwitu, pori, mbuga, _________________
(vi) twanga, vunjavunja, saga, _______________
(vii) mzizi, kiini, asili, ___________
(viii) soni, haya, fedheha, ________
(ix) wawiliwawili, pea, jozi, __________
(x) shida, mashaka, usumbufu, ____________

**D. Taja aina ya neno mojamoja lililotumiwa katika sentensi zifuatazo. Andika chini ya neno hilo herufi inayowakilisha aina ya neno hilo.**

**Mfano:** <u>Njiwa</u> <u>ametaga</u> <u>mayai</u> <u>mengi</u>.
N T N V

(i) Mvua ilinyesha siku nzima.
(ii) Viwavijeshi wamemaliza mahindi yetu.
(iii) Wanafunzi wangu wamechaguliwa wote.
(iv) Vitunguu saumu vinanukia vizuri.
(v) Mlango wa darasa umejibamiza.
(vi) Tutaenda mtoni kuchota maji.
(vii) Umeme hutuletea maendeleo.
(viii) Mwakani tutafanya mtihani wa Darasa la Saba.
(ix) Mwindaji alimlenga vizuri mnyama.
(x) Aa! Unanisingizia.
(xi) Yeye ni nani?



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 125 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**E. Tumia silabi "ri" au "li" kukamilisha maneno yafuatayo:**

(i) ___poti
(ii) mawasi___ano
(iii) asa___
(iv) ___sala
(v) ___nda
(vi) ___mau
(vii) lo___
(viii) mala___a
(ix) re___
(x) si___
(xi) se___ka___
(xii) ram___

**F. Ondoa silabi moja katika maneno uliyopewa ili kupata maneno mapya yaliyo sahihi.**

**Mfano:** mraba – *raba*
barafu – *bafu*
kituo – *kitu*

(i) kitasa
(ii) uani
(iii) duara
(iv) siafu
(v) tazama
(vi) mkufu
(vii) uzazi
(viii) maswali
(ix) yoyote
(x) hapotei

**G. Chagua jibu sahihi, katika maswali yafuatayo:**

(i) Mtu anayeandika kumbukumbu za mikutano huitwa:

(a) Katibu
(b) Mwenyekiti
(c) Mtunzi
(d) Kumbukizi

(ii) Kumbukumbu za mikutano kwa jina lingine huitwa:

(a) riwaya
(b) shairi

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(c) muhtasari
(d) mswada

(iii) Kumbukumbu za mikutano zina sehemu kuu:

(a) 3
(b) 4
(c) 5
(d) 2

(iv) Kumbukumbu za mikutano huandikwa ili:

(a) kuweka akiba ya karatasi za kuvutia tumbaku
(b) kunukuu kila kilichosemwa katika mkutano
(c) kuwasaidia watu maskini
(d) kutunza taarifa za mambo muhimu yaliyojadiliwa katika mkutano

(v) Kichwa cha habari, tarehe, utangulizi, kiini na hitimisho ni sehemu tano zinazojitokeza katika vipengele hivi vyote isipokuwa:

(a) barua ya kikazi
(b) insha
(c) barua ya kiofisi
(d) kadi za mwaliko

## Zoezi la 6: Utungaji

**A. Fikiria kuwa wewe ni katibu wa klabu ya michezo shuleni kwenu. Jana ulihudhuria mkutano wa klabu. Andika kumbukumbu za mkutano huo. Zingatia mambo yafuatayo:**

(i) Kichwa cha kumbukumbu ya mkutano
(ii) Mahali mkutano ulipofanyika
(iii) Tarehe ya mkutano
(iv) Muda wa mkutano
(v) Watu waliohudhuria
(vi) Mambo yaliyozungumzwa
(vii) Mambo yaliyokubaliwa
(viii) Mambo yaliyokuwa ya nyongeza
(ix) Muda wa kufunga mkutano

**B. Andika insha kuhusu huduma ya kliniki. Insha yako iwe na vipengele vifuatavyo:**

(i) Kichwa cha insha
(ii) Utangulizi wa insha
(iii) Kiini cha insha
(iv) Hitimisho la insha

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 127 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Tano

## Umiliki katika lugha

### Utangulizi

*Katika sura hii, utasoma habari kuhusu "Kijiji chao". Pia, utajifunza kuhusu maneno yanayoonesha umiliki na utaweza kuyatumia maneno hayo katika mawasiliano yako ya kila siku.*

### Fikiri



1. Je, umewahi kuwa na kitu chako?
2. Je, kitu hicho ulikipata wapi?

### Ufahamu

*Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

**Kijiji chao**

Dungo ni mwanafunzi wa Darasa la Sita katika Shule ya Msingi Kidosa. Dungo anaishi katika kijiji kiitwacho U**miliki**. Kijiji chao kimepiga hatua katika maendeleo kutokana na kumiliki huduma mbalimbali za kijamii. Mwenyekiti wao huwa**hamasisha** katika shughuli za maendeleo kama vile kilimo, ufugaji na huduma za kijamii. Kwa hiyo, wanakijiji wake hujishughulisha na shughuli mbalimbali.

Kwa upande wa kilimo, mwenyekiti wao amewahamasisha kupanda mazao ya chakula na biashara. Mazao yao yame**stawi** sana. Aliwasisitiza kila mwanakijiji ahakikishe anapanda mazao yake kwa ajili ya chakula ili isiwepo kaya itakayokumbwa na njaa. Pia, aliwahimiza kufuga mifugo mbalimbali. Wanafuga mifugo kama vile kuku, bata, mbuzi na ng'ombe. Mifugo yao ilizaliana na kuongezeka sana. Kwa hiyo, wanakijiji walipata manufaa makubwa kutokana na kuuza mazao na mifugo yao na kujipatia chakula.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 128 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Vilevile, kijiji chao kinamiliki shule ya msingi na sekondari. Wanakijiji wa kijiji hicho walishirikiana kwa pamoja katika ujenzi wa shule zao. Dungo ni mmoja wa wanafunzi wanaosoma katika shule ya msingi ya kijiji chao. Shule zao huwapa fursa watoto wengi kupata elimu. Hivyo, wengi wao wanajua kusoma na kuandika. Pia, wengine wanapata nafasi ya kuendelea mbele katika elimu. Kwa hiyo, elimu hiyo huwasaidia kutoa **mchango** wa mawazo kwa ajili ya maendeleo ya kijiji chao.

Siku moja, Dungo alikutana na rafiki yake anayeishi kijiji cha jirani. Katika maongezi yao, Dungo alimwambia, “Rafiki yangu siku moja uwaombe ruhusa wazazi wako uje katika kijiji chetu uone tofauti iliyopo kati ya kijiji chetu na chenu. Kijiji chetu kinamiliki vitu mbalimbali kwa manufaa ya wanakijiji wote. Hivyo, uje ujionee mwenyewe kwa macho; si kusimuliwa.”



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 129 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Pia, alieleza kuwa kijiji chao kinamiliki **zahanati.** Zahanati yao inatoa huduma kwa wagonjwa wanaokuja kutibiwa na kuondoka bila kulazwa. Wagonjwa wanapotakiwa kulazwa, hupelekwa katika hospitali ya wilaya iliyoko mbali na kijiji chao.

Siku moja, **Mganga** Mkuu wa zahanati aliushauri uongozi wa kijiji kuhusu kujenga **wodi** mbili. Alishauri ijengwe wodi ya watoto na wodi ya akina mama. Alishauri kuwa nje ya wodi ya watoto kuwe na sehemu ya kupimia watoto na kuwapatia chanjo mbalimbali, yaani **kliniki**. Pia, alieleza kuwa katika wodi ya akina mama, pawe na mahali pa kupimia wajawazito ili wapate vipimo vyao hapohapo kijijini kwao. Mganga mkuu alishauri hivyo ili kuwaondolea adha wazazi wenye watoto wadogo na akina mama wajawazito. Hii ilitokana na huduma ya kliniki kupatikana mbali.

Viongozi wa kijiji waliunga mkono wazo lake. Waliwahamasisha wanakijiji kuchangia ujenzi wa wodi ya watoto na wodi ya akina mama. Wanakijiji walitoa michango yao kwa moyo. Pia, walijitolea nguvu zao pale walipohitajika kufanya hivyo.



FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 130 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Walipomaliza kujenga ukuta, walitengeneza **paa**. Hatimaye, kliniki na wodi hizo ziliezekwa mara moja. Wanakijiji walimshukuru Mganga Mkuu kwa kutoa wazo la ujenzi wa wodi ya watoto na ya akina mama. Kwa sasa, kijiji chao kina wodi na kliniki ya kisasa ya watoto na akina mama wajawazito. Wanakijiji wote wanafurahia kupata huduma hizo katika kijiji chao kwa sababu wameondokana na kero ya kupata matibabu nje ya kijiji chao, hasa akina mama na watoto, pale wanapotakiwa kulazwa. Ama kweli penye wengi hapaharibiki jambo.

## Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Dungo anaishi kijiji gani?
2. Wananchi wa kijiji hicho hujishughulisha na nini?
3. Kwa nini mwenyekiti wa kijiji alisisitiza kila mwanakijiji ahakikishe anapanda mazao yake?
4. Wanakijiji walipata faida gani kutokana na kilimo?
5. Eleza umuhimu wa kuwa na shule ya msingi na sekondari katika kijiji hicho.
6. Kwa nini Mganga Mkuu wa zahanati alitoa wazo la ujenzi wa wodi?
7. Wanakijiji walishiriki vipi katika ujenzi wa wodi hizo?
8. Wanakijiji walipata nini kutokana na ujenzi wa wodi hizo?
9. Methali "Penye wengi, hapaharibiki jambo" ina maana gani katika habari uliyoisoma?
10. Umejifunza nini kutokana na habari uliyoisoma?

## Zoezi la pili: Msamiati

**Tunga sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo:**

1. miliki
2. hamasisha
3. stawi
4. mchango
5. zahanati
6. kero
7. mganga
8. wodi
9. kliniki
10. paa

## Zoezi la 3: Nahau

**Tunga sentensi mbili kwa kila nahau.**

1. kaza mwendo

   **Mfano:** *Wanakijiji walikaza mwendo katika kupata maendeleo yao.*

2. piga marufuku

   **Mfano:** *Wananchi wamepiga marufuku ukataji miti ovyo.*

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 131 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. unga mkono

**Mfano:** *Wazazi wali<u>unga mkono</u> watoto wao kushiriki katika shughuli za kijamii.*

4. fanya juu chini

**Mfano:** *Viongozi wa kijiji wali<u>fanya juu chini</u> kuhakikisha wodi mbili zinajengwa.*

5. bega kwa bega

**Mfano:** *Wanafunzi walishirikiana <u>bega kwa bega</u> kusoma kwa bidii.*

## Zoezi la 4: Mazoezi ya lugha

**A. Chagua neno sahihi kutoka kwenye mabano ili kujaza nafasi zilizoachwa wazi.**

**Mfano:** *Wafugaji wamechimba bwawa ili kupata maji kwa ajili ya mifugo <u>yao</u>. (vyao, chake, yao, lao)*

*Wageni wote wameketi kwenye viti <u>vyao</u>. (chao, vyao, chake, changu)*

(i) Kitabu __________ kimechanika chote. (chake, yake, lake, vyetu)

(ii) Nyumba __________ zimeezekwa kwa bati. (yetu, zetu, lako, vyao)

(iii) Shati __________ limechafuka mno. (yetu, zenu, chao, lake)

(iv) Mama __________ amekwenda sokoni. (yake, wake, chao, lake)

(v) Madawati __________ yametengenezwa vizuri. (lake, zake, yao, vyetu)

(vi) Gari __________ ni jipya kabisa. (chetu, chake, lake, zao)

(vii) Lugha __________ ni Kiswahili. (yetu, chao, chetu, vyake)

(viii) Viatu __________ ni vizuri. (chake, lake, langu, vyake)

(ix) Kaka __________ analima bustani. (lake, lao, chake, yao)

(x) Chumba cha darasa __________ ni kidogo sana. (chao, chetu, vyake, letu)

(xi) Magodoro ya wanafunzi __________ yamekabidhiwa leo. (yetu, wetu, chake, chao)

(xii) Funguo __________ zilizopotea, zimeletwa na msamaria mwema. (zangu, vyake, chake, vyao)

(xiii) Mazao __________ yamestawi vizuri. (yao, chetu, chake, vyao)

(xiv) Mgeni __________ amewasili leo alfajiri. (yake, yetu, wangu, vyao)

(xv) Kalamu __________ inaandika vizuri. (yake, vyao, chetu, chake)

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**B. Andika umoja au wingi wa maneno yafuatayo:**

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| **Mfano** | *mgeni* | *wageni* |
| | *bakuli* | *mabakuli* |
| (i) | karatasi | ___________ |
| (ii) | ___________ | nyungo |
| (iii) | ___________ | mashamba |
| (iv) | ___________ | mipini |
| (v) | kikapu | ___________ |
| (vi) | galoni | ___________ |
| (vii) | likizo | ___________ |
| (viii) | ___________ | vyangu |
| (ix) | ___________ | ndizi |
| (x) | mboga | ___________ |

**C. Badili sentensi zifuatazo kuwa katika hali ya mazoea.**

**Mfano:** *Bibi anakula mahindi ya kuchemsha.*
*Bibi hula mahindi ya kuchemsha.*
*Juhudi aliendesha baiskeli kwa uangalifu kwenda shuleni.*
*Juhudi huendesha baiskeli kwa uangalifu aendapo shuleni.*

(i) Babu Mpande amepanda maua nyumbani kwake.
(ii) Gari la mjomba linatoa moshi mwingi.
(iii) Wakulima wanapalilia mikorosho mara mbili kwa mwaka.
(iv) Mbwa wetu anabweka akiona wageni.
(v) Dada yangu anafanya mazoezi kila siku asubuhi.
(vi) Shangazi atakuja na mtoto wake nyumbani.
(vii) Mtoto wa mjomba anaitwa binamu.
(viii) Joni atatembelea daraja la Mto Rufiji wakati wa likizo.
(ix) Mvua nyingi zitanyesha msimu wa masika.
(x) Kaka anajibu barua zote alizoandikiwa na rafiki zake.

**D. Pigia mstari vivumishi katika sentensi zifuatazo:**

**Mfano:** *Wachezaji machachari wameshinda mechi ya mpira wa miguu.*
*Baba amenunua pikipiki mpya.*

(i) Mwanafunzi hodari anajua kusoma vizuri.
(ii) Uchafu wote umemwagwa mbali.
(iii) Mpira wetu umepotea kabisa.
(iv) Mboga zote za majani ni nzuri.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 133 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(v) Mama yao ni mpole.
(vi) Shule ile ina walimu wengi.
(vii) Wimbo huu ni mzuri.
(viii) Kiranja huyu amepata kura nyingi.
(ix) Nyumba hii inapangishwa.
(x) Watu hawa wana ushirikiano kama siafu.
(xi) Babu Mapande ana mashamba makubwa ya mpunga.
(xii) Mjukuu wangu anapenda kulia.

**E. Tunga sentensi sahihi kumi (10) kwa kutumia jedwali lifuatalo:**

**Mfano:** *Gesi ni mojawapo ya nishati mbadala.*

| | | |
|---|---|---|
| Gesi<br>Korosho<br>Ukisoma<br>Kilimo cha matuta<br>Kusalimia<br>Uchoraji<br>Ugali<br>Kupanda miti<br>Ukifanya kazi | kwa bidii<br>ni mojawapo ya | mazao ya biashara<br>nishati mbadala<br>utafanikiwa maishani<br>njia ya kutunza mazingira<br>utafaulu mtihani<br>kitendo cha heshima<br>vyakula vya asili<br>kazi ya sanaa |

**F. Andika maneno matano yenye maana kutokana na jedwali, kisha tunga sentensi moja kwa kila neno.**

**Mfano:** Neno - *zoa*
Sentensi - *Wanafunzi walipomaliza kufagia, walizoa takataka zote.*

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | K | A | A | G | E | S | I | H |
| A | M | K | A | E | L | I | M | A |
| K | I | M | A | U | E | M | A | P |
| A | D | A | I | K | Z | A | R | A |
| Z | I | K | W | A | E | M | A | N |
| I | G | I | Z | O | A | A | S | A |

**G. Panga herufi zifuatazo ili kupata neno sahihi.**

**Mfano:** *limumwa - mwalimu*
*nofma - mfano*

(i) amso ____________

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 134 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(ii) idibi ____________
(iii) saho ____________
(iv) ooggma ____________
(v) maazi ____________
(vi) chime ____________
(vii) ngaap ____________
(viii) utpese ____________
(ix) tisanih ____________
(x) riaafs ____________

**H. Panga sentensi zifuatazo katika mtiririko wenye kuleta maana.**

(i) Niliogopa, lakini nilipiga moyo konde.
(ii) Nilikimbia hadi nyumbani.
(iii) Jumamosi iliyopita, mama alinituma sokoni.
(iv) Nilipokuwa ninarudi, nilikuta kunguru wanamla yule nyoka niliyemuua.
(v) Nilirudi nyuma kidogo nikaokota fimbo.
(vi) Nilipokuwa njiani, nilimwona nyoka.
(vii) Nilimpiga nyoka kwa ile fimbo akafa.
(viii) Aliniambia ninunue nyanya, vitunguu, sukari, mchele na mafuta.
(ix) Nilikimbia hadi sokoni.

## Zoezi la 5: Utungaji

**Malizia habari ifuatayo kwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kutumia maneno yanayoonesha umiliki.**

Wavuvi walichukua nyavu______kuelekea ziwani. Walipofika huko, walikuta wavuvi wengine wameshaingia kwenye mitumbwi _______. Kando ya ziwa, kulikuwa na wachuuzi mbalimbali wakiwa na vikapu _______ mikononi. Wachuuzi hao walikuwa wanawasubiri kwa hamu wavuvi watoke ziwani. Baada ya muda, wavuvi waliwasili na mitumbwi ______ ikiwa imejaa samaki wa kila aina. Walipofika ufukweni, walianza kuuza samaki _______ kwa wachuuzi. Kila mvuvi alipanga bei _______ kulingana na ukubwa wa samaki. Wachuuzi walinunua samaki kulingana na vipato ______. Baada ya shughuli ya kununua na kuuza samaki, kila mmoja alishika njia ____. Wachuuzi wengine walikwenda kuuza samaki ________ wakiwa wabichi, wengine walikwenda kuwauza baada ya kuwakaanga.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 135 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Sita

## Kuandika habari

### Utangulizi

*Katika sura hii, utasoma habari inayohusu "Likizo yangu." Kutokana na habari hiyo utajifunza kazi mbalimbali zinazofanywa katika jamii yetu. Pia, utatunga habari kuhusu kazi mbalimbali zinazofanywa katika jamii. Umahiri huu utakusaidia kuchagua fani utakayoisomea na itakayokusaidia katika maisha yako.*

### Fikiri



1. Je, wazazi/walezi wako wanafanya kazi gani?
2. Je, wewe unapenda kufanya kazi gani? Kwa nini?

### Ufahamu

*Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

**Likizo yangu**

Ninaitwa Nyakitwe. Ninasoma Darasa la Sita katika Shule ya Msingi Maji ya Moto iliyoko Mkoa wa Ruvuma, Wilaya ya Songea. Kaka yangu anaitwa Mtimbi na dada yangu anaitwa Zawadi. Wote wanaishi pamoja jijini Dar es Salaam eneo linaloitwa Gongo la Mboto. Kaka yangu ni **rubani** wa ndege za Shirika la Ndege la Tanzania. Dada Zawadi ni **mhadhiri** wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Siku moja, nilimwandikia kaka yangu barua ya kumwomba niende kumtembelea wakati wa likizo ya mwezi Desemba. Kaka alikubali ombi langu. Tulipofunga shule mwezi Novemba mwishoni, nilijiandaa kwa safari ya kwenda likizo Dar es Salaam. Nilikwenda ofisi ya basi Songea na kukata tiketi.

Siku ya safari ilikuwa Jumamosi. Nilidamka na kujiandaa. Dereva wa bodaboda alikuja kunichukua hadi stendi ya mabasi. Nilipanda basi na safari ya kuelekea Dar es Salaam ilianza. Njiani, nilifurahia kuona safu za milima na mabonde yaliyovutia. Pia, niliona wakulima wakiendelea na shughuli zao za shambani. Walilima kwa kutumia matrekta na wengine walitumia jembe la mkono. Safari ilikuwa ndefu. Ilinichosha sana. Pamoja na kuchoka huko,

FOR ONLINE USE ONLY




KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 136 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

nilikuwa na shauku ya kuliona Jiji la Dar es Salaam. Kila mara, nilimuuliza abiria aliyekuwa amekaa karibu yangu kama tumekaribia kufika Dar es Salaam.

Hatimaye, tulifika jijini Dar es Salaam mnamo saa mbili usiku. Nilishangaa kuona taa nyingi zilizorembesha jiji hilo. Pia, niliona majengo na madaraja makubwa ambayo magari hupita juu na mengine chini. Nilijisemea moyoni, "Kweli hawa wajenzi wa haya madaraja wame**bobea** katika **uhandisi**."

Dada yangu alikuja kunipokea. Niliposhuka kwenye basi, nilifurahia sana kumwona dada yangu. Alinipokea begi na kuniongoza hadi kwenye gari lake. Tulianza safari kuelekea nyumbani kwa kaka. Dada alikuwa anaendesha kwa uangalifu mkubwa sana. Alisimama kwenye taa za kuongozea magari pale ambapo taa zilimwongoza kufanya hivyo. Nilishangaa kuona msururu mrefu wa magari ya kila aina. Baadhi ya sehemu niliona askari polisi ambao walikuwa wamesimama pembezoni mwa barabara. Dada aliniambia kuwa askari hao wanasimamia sheria za usalama barabarani. Pia, niliona maduka mengi ya vitu mbalimbali. Vilevile, katika baadhi ya maeneo, niliona watu wakifanya biashara mbalimbali pembezoni mwa barabara.






KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 137 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Tulifika nyumbani kwa kaka, lakini hatukumkuta. Dada aliniambia kwamba kaka bado yupo kazini na atachelewa kurudi. Tulikula chakula, tukalala. Siku iliyofuata ilikuwa Jumapili. Niliamka mapema nikiwa na hamu ya kumwona kaka. Nilifurahi sana kumwona. Tuliongea mambo mengi kuhusu nyumbani Songea. Baadaye kaka aliaga kwamba anaenda kazini. Nilibaki na dada Zawadi. Siku hiyo tulishinda tu nyumbani.

Kesho yake, dada Zawadi aliniaga na kwenda kazini. Jioni aliporejea nyumbani, alianza kunisimulia kuhusu maendeleo ya miundombinu ya jiji la Dar es Salaam. Aliahidi kwamba angenitembeza jijini ili nijionee mwenyewe kwa macho yangu. Siku zilizofuata, dada alianza kunitembeza katika maeneo mbalimbali.

Miongoni mwa maeneo aliyonipeleka ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Alinipeleka katika Maktaba Kuu ya chuo hicho. Maktaba hiyo ilikuwa kubwa sana iliyosheheni vitabu vingi. Tulikaribishwa na **mkutubi** aliyetueleleza utaratibu wote wa maktaba. Miongoni mwa utaratibu ni pamoja na kuazimisha vitabu na kusoma vitabu kwa njia ya mtandao wa intaneti.

Vilevile, dada alinipeleka Kigamboni. Tulifika eneo la feri na kuvuka kwa kutumia **kivuko**. Kivuko hicho kiliongozwa na **nahodha.** Aliongoza kivuko kwa ustadi mkubwa. Hatimaye, kivuko kili**tia nanga**. Abiria wote tuliokuwemo kwenye kivuko, tulishuka. Nilifurahia kuona maghorofa marefu na meli kubwa mithili ya nyumba. Meli hizo zilikuwa zimebeba mizigo. Pia, niliona boti za wavuvi waliokuwa wakitoka kuvua samaki na wengine wakienda kuvua samaki. Tuli**barizi** kwa muda kandokando ya bahari.

Baada ya saa moja, tulipanda kivuko na kurejea feri ili kuendelea kujionea uzuri wa jiji. Huko tuliwaona wafanyabiashara na watu wengine wengi kila mmoja akiwa anajishughulisha na kazi. Pia, niliona kundi kubwa la **wanajeshi** barabarani. Walikuwa wanakimbia kando ya barabara huku wakiimba nyimbo. Moyo wangu uli**gutuka**. Nilimuuliza dada, "Kulikoni leo hao wanajeshi?" Alinijibu, "Wanajeshi hao wanatoka kwenye michezo. Nadhani watakuwa wameshinda ndiyo maana wanaimba kwa furaha, wala usihofu." Moyo wangu ulitulia.

Dada alinipeleka sehemu mbalimbali kila alipopata nafasi. Nilitembelea pia uwanja wa ndege wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Nilijionea mambo mengi ikiwa ni pamoja na namna ndege zinavyotua na kupaa. Kwa kweli, niliifurahia sana likizo yangu. Nilijifunza na kuvutiwa na mambo mengi. Hivyo, nimeazimia kusoma kwa bidii ili siku moja niwe **mhandisi**. Likizo ilipomalizika, nilirejea nyumbani kwetu kuendelea na masomo.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Mtimbi anafanya kazi gani?
2. Mkutubi hufanya kazi wapi?
3. Mtu anayeongoza kivuko anaitwa nani?
4. Nyakitwe alikwenda likizo wapi?
5. Mtu anayeendesha gari anaitwa nani?
6. Mtimbi anakaa wapi?
7. Nyakitwe alisafiri kwenda Dar es Salaam kwa kutumia nini?
8. Mhandisi anafanya kazi gani?
9. Nyakitwe anatamani kuwa nani?
10. Umejifunza nini kutokana na habari uliyoisoma?

## Zoezi la pili: Msamiati

**Oanisha msamiati katika sehemu A na maana zake katika sehemu B katika jedwali lifuatalo:**

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| (i) shirika | (a) shangaa kutokana na kitu unachokiona au jambo unalolisikia |
| (ii) gutuka | (b) basi dogo linalosafirisha abiria ndani ya mji au jiji |
| (iii) barizi | (c) kumilikiwa kwa pamoja |
| (iv) uhandisi | (d) ujuzi wa kutengeneza, kukarabati na kuhudumia miundo mbinu |
| (v) damka | (e) kifaa aghalabu cha chuma kizito chenye ncha ambacho hufungwa kwenye kamba au mnyororo na kushushwa majini ili kukifanya chombo kisitembee na kuyumbayumba |
| (vi) nanga | (f) fahamu jambo kwa kina |
| (vii) bobea | (g) chombo cha majini kinachovusha magari, mizigo na watu |
| (viii) daladala | (h) punga upepo |
| (ix) kivuko | (i) amka asubuhi na mapema |
| | (j) shtuka |

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 139 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 3: Mazoezi ya lugha

### A. Chagua jibu sahihi katika maswali yafuatayo:

(i) Mtu anayelima mazao mbalimbali shambani anaitwaje?

(a) mkulima
(b) mwindaji
(c) mpanda maua
(d) rubani

(ii) ___________ anarusha ndege.

(a) Nahodha
(b) Rubani
(c) Mwanajeshi
(d) Mhandisi

(iii) __________ hufanya kazi ya kuazimisha vitabu maktaba.

(a) Mhandisi
(b) Mwanajeshi
(c) Mhadhiri
(d) Mkutubi

(iv) Mtu anayeongoza chombo kinachosafiri majini anaitwaje?

(a) dereva
(b) mhandisi
(c) nahodha
(d) mwanajeshi

(v) Mtu aliyeajiriwa kulinda nchi yake anaitwaje?

(a) mhadhiri
(b) mkulima
(c) machinga
(d) mwanajeshi

(vi) _________ hufanya kazi ya kununua na kuuza bidhaa.

(a) Daktari
(b) Mfanyabiashara
(c) Mhadhiri
(d) Mwanajeshi

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 140 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(vii) Mtu anayefundisha Chuo Kikuu anaitwa:

(a) mhadhiri
(b) mkutubi
(c) dereva
(d) mwanajeshi

(viii) Mtu anayefanya kazi ya kutunza amani katika nchi anafanya nini?

(a) analinda nchi
(b) anarusha na kuongoza ndege
(c) anafanya biashara
(d) anajenga miundombinu

(ix) Chombo maalumu cha majini kinachotumika kuvusha watu na mizigo kwenda ng'ambo ya pili huitwa____________.

(a) daladala
(b) pikipiki
(c) basi
(d) kivuko

(x) Mtu mwenye taaluma ya ujuzi wa kubuni, kutengeneza au kurekebisha majengo, barabara, madaraja au mitambo anaitwaje?

(a) rubani
(b) dereva
(c) mkutubi
(d) mhandisi

## B. Tumia maneno yaliyoko kwenye kisanduku kukamilisha sentensi.

| |
|---|
| mwindaji, hakimu, machinga, dobi, seremala, mkalimani, mkunga, mwashi, mfinyanzi, mvuvi, sonara, mfugaji, kocha, daktari, dalali |

**Mfano:** Mtu anayeuza bidhaa katika mnada kwa kushindanisha bei, anaitwa dalali.

(i) Mtu anayefanya kazi ya kufasiri mazungumzo kutoka lugha moja kwenda nyingine, anaitwa_______.
(ii) Mtu anayetengeneza mapambo kwa kutumia madini, anaitwa____________.
(iii) Mtu anayeamua kesi mahakamani, anaitwa_________.
(iv) Mtu anayefanya kazi ya kujenga nyumba kwa kutumia matofali au mawe, anaitwa_________.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 141 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(v) Mtu anayefuga wanyama mbalimbali, anaitwa__________.
(vi) Mtu anayefanya kazi ya kutengeneza samani kwa kutumia mbao au miti, anaitwa__________.
(vii) Mtu anayefanya kazi ya kusaidia wajawazito kujifungua, anaitwa___________.
(viii) Mtu anayetengeneza vyombo vya udongo kama vile vyungu, anaitwa_________.
(ix) Mtu anayefanya kazi ya kutibu wagonjwa hospitalini, anaitwa___________.
(x) Mtu anayefanya kazi ya kufundisha mchezo wa soka, anaitwa________.
(xi) Mtu anayefanya kazi ya kufua na kupasi nguo, anaitwa__________.
(xii) Mtu anayeuza bidhaa rejareja kwa kuzunguka na bidhaa mitaani, anaitwa__________.
(xiii) Mtu anayefanya kazi ya kuwinda wanyama, anaitwa__________.
(xiv) Mtu anayefanya kazi ya kuvua samaki, anaitwa___________.

## C. Andika visawe vya maneno yafuatayo:

**Mfano:** *chotara - suriama au shombe*

(i) makubaliano
(ii) utajiri
(iii) chanzo
(iv) chuki
(v) teremka
(vi) daima
(vii) changamana
(viii) chapuchapu
(ix) chache
(x) kasoro

## D. Andika kinyume cha maneno yafuatayo:

**Mfano:** *safisha - chafua*

(i) mnunuzi
(ii) kusanya
(iii) refusha
(iv) fumba
(v) jenga
(vi) sifu

FOR ONLINE USE ONLY

(vii) panga
(viii) funika
(ix) upendo
(x) pona

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**E. Jaza chemshabongo ifuatayo kwa herufi kubwa kwa kuzingatia maelezo ya kwenda kulia na chini. Kila kisanduku kiandikwe herufi moja tu.**

**Mfano: Kwenda kulia**

1. Mtu anayetunga na kuimba mashairi (herufi 7) – **MSHAIRI**

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 M | 2 S | 3 H | A | I | 4 R | I | ■ | 5 | ■ |
| 6 | | | ■ | ■ | | ■ | ■ | | ■ |
| 7 | | | | ■ | 8 | | | | ■ |
| | | | ■ | 9 | | ■ | ■ | ■ | ■ |
| | ■ | ■ | ■ | | ■ | ■ | 10 | ■ | 11 |
| ■ | ■ | ■ | ■ | | ■ | ■ | | ■ | |
| 12 | | | | | | ■ | | ■ | |
| ■ | ■ | ■ | ■ | | ■ | ■ | | ■ | |
| ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | |
| 13 | | | | | | 14 | ■ | ■ | |
| ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | 15 | | | |
| 16 | | | | | ■ | | ■ | ■ | |
| ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | 17 | | |
| 18 | | | | | | | ■ | ■ | ■ |
| ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | 19 | | |
| 20 | | | | | | ■ | ■ | ■ | ■ |

**Kwenda kulia**

1. Mtu mwenye ujuzi wa kutunga mashairi (herufi 7)
6. Tawanya mbegu shambani au bustanini ili ziote (herufi 3)
7. Kupata maumivu au dhoofu mwili kutokana na maradhi (herufi 4)
8. Uwanja wa maarifa ambapo mtu amebobea (herufi 4)
12. Mtu anayerusha ndege (herufi 6)
13. Mtu anayefanya kazi ya kutunza fedha na taarifa za matumizi (herufi 7)



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 143 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

15. Kitendo cha kufunika sehemu iliyo wazi (herufi 4)
16. Mtu anayefanya kazi ya kuvua samaki (herufi 5)
17. Kiasi cha fedha kilichopangwa kuuzia au kununulia bidhaa (herufi 3)
18. Mtu anayefanya kazi ya kuazimisha vitabu maktaba (herufi 7)
19. Pungua joto (herufi 3)
20. Mtu ambaye hufanya kazi ya kuwakilisha wananchi bungeni (herufi 6)

**Kwenda chini**

1. Mtu anayefanya kazi ya kusuka (herufi 5)
2. Kifaa tunachotumia kuwasiliana (herufi 4)
3. Kibainishi cha nafsi ya tatu wingi (herufi 4)
4. Mtu anayefanya uamuzi katika mchezo wa soka (herufi 4)
5. Kiungo laini kilichomo ndani ya mwili wa mnyama chenye kazi ya kutoa sumu (herufi 3)
9. Ahadi ya utekelezaji wa jambo fulani (herufi 5)
10. Mtu anayefanya kazi ya kufua na kupasi nguo (herufi 4)
11. Mtu anayefanya kazi ya kufasiri mazungumzo (herufi 9)
14. Hutumika kushonea nguo (herufi 3)

## Zoezi la 4: Utungaji

**Andika habari ya maneno mia moja (100) kuhusu kazi unayoipenda.**

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Saba

## Shairi la mabadiliko ya hali ya hewa

### Utangulizi

*Katika sura hii, utajifunza kuhusu shairi la mabadiliko ya hali ya hewa. Utatunga shairi la kimapokeo kuhusu hali ya hewa na kulighani. Pia, utaweza kusimulia kisa kinachohusu hali ya hewa. Umahiri huu utakuwezesha kubaini mabadiliko ya hali ya hewa katika mazingira yako na jinsi ya kukabiliana nayo.*

### Fikiri



1. Umewahi kuona mvua ikinyesha?
2. Upepo unaweza kusababisha madhara gani?

### Ufahamu

*Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali.*

**Mabadiliko ya hali ya hewa**

Matera ni mwanafunzi wa Darasa la Sita katika Shule ya Msingi Ngongongare iliyoko mkoani Arusha. Anaishi na babu yake aitwaye Mtundi. Matera humsaidia babu yake kuchunga mbuzi.

Siku moja Matera alimwomba babu yake wakachunge mbuzi porini. Babu yake alikubali, wakaondoka kwenda kuchunga. Ghafla wakiwa huko, hali ya hewa ilianza kubadilika. Mawingu meusi yalitanda, anga zima likawa mithili ya moshi. Upepo mkali ulivuma ukiambatana na radi. Nazo **ngurumo** za mvua zili**rindima**. Kila mmoja akatamani kujichimbia ardhini. Ghafla, mbuzi waliingia kwenye pango lililokuwa karibu. Matera na babu yake, kwa haraka, waliwafuata mbuzi na kujihifadhi humo pangoni kwa muda.

Matera alitaka kujua sababu ya hali ile kutokea. Alimuuliza babu yake, “Babu, kwa nini hali hii imetokea?” Babu yake, kwa kusitasita, alimwondolea wasiwasi, “Mjukuu wangu, haya ni mabadiliko ya hali ya hewa.” Kuna kipindi cha mvua ambacho wakati mwingine huambatana na radi, ngurumo na upepo mkali. Pia, kuna wakati mvua tulivu isiyokuwa na **dhoruba** yoyote hunyesha. Mara nyingi, mvua yenye upepo mkali na mawe huleta maafa. Huweza kuezua mapaa ya nyumba, kubomoa madaraja, kuharibu mazao na kusababisha vifo vya watu na wanyama.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 145 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Zamani hali ya hewa ilikuwa nzuri. Uchafuzi wa mazingira unaofanywa na binadamu umesababisha hali ya hewa kubadilika. Siku hizi mvua si ya uhakika na huweza kunyesha bila kufuata muda wake, tofauti na zamani. Tunapata kipindi kirefu cha kiangazi ukilinganisha na zamani. Watu wanachoma moto misitu na kukata miti ovyo. Pia, shughuli za viwanda zimeharibu anga na kusababisha ongezeko la joto.

Jua likiwaka kwa muda mrefu huweza kukausha mito, chemchemi na vijito. Hali hii ikiendelea kwa muda mrefu bila mvua kunyesha, huweza kuleta ukame na njaa.

Matera alikumbuka jinsi mwalimu alivyowafundisha darasani kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa. Kwa kuwa babu yake anapenda mashairi, Matera alitunga shairi haraka kuhusu hali ya hewa na kumwimbia babu.

1. Hapa kwetu Tanzania, nyakati zimetukuka,
   Kuna nyakati za jua, kwa wengi hutamanika,
   Nazo nyakati za mvua, kwa viumbe ni baraka,
   Anga ni kama **pazia**, mengi limeyafunika.



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 146 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2. Twalipenda sana jua, kuzikausha nafaka,
Afya hutuongezea, miili kuimarika,
Likiwaka pindukia, **ukame** huongezeka,
Anga ni kama pazia, mengi limeyafunika.

3. Pia ya chakula **njaa**, redioni husikika,
Sababu yake ni jua, mimea inakauka,
Na ya upepo **fukaa**, mazao kutaabika,
Anga ni kama pazia, mengi limeyafunika.

4. Maji nayo twawazia, chemchemi kufutika,
Anga limejifungia, watu wanaathirika,
Lini itatunyeshea, mbona tunaduduika,
Anga ni kama pazia, mengi limeyafunika.

5. Anga limejifunua, na mvua inamwagika,
Viumbe kushangilia, vijito vinapanuka,
Vyura wanaitikia, na mito inafurika,
Anga ni kama pazia, mengi limeyafunika.

6. Mimea kujiotea, imefurika baraka,
Kwa hesabuye sikia, inazidi ongezeka,
Maisha nayo sawia, binadamu **hakahaka**.
Anga ni kama pazia, mengi limeyafunika.

7. Anga linajishitua, siku isotabirika,
Upepo linafyatua, na mvua kumiminika,
Miti inainamia, mapaa kuezulika,
Anga ni kama pazia, mengi limeyafunika.

8. Limetokea balaa, shida isotamanika,
Hata aloji**shaua**, imekuwa patashika,
Asojua ogelea, amepata hangaika,
Anga ni kama pazia, mengi limeyafunika.

9. Ni vigumu simulia, hali kama ya **gharika**,
Baridi sije chezea, kifua kutetemeka,
Sweta utang'ang'ania, mifupa sijekauka.
Anga ni kama pazia, mengi limeyafunika.

10. Baridi bila ya mvua, ni ya vipindi hakika,
Arusha inaanzia, na Iringa hu**gubika**,
Baridi ukichelea, katu haina dhihaka,
Anga ni kama pazia, mengi limeyafunika.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 147 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

11. Ukungu ukitokea, ngedere hurukaruka,
Mazao husogelea, hadi ndani ya mpaka,
Pasipo kujitambua, mtegoni hunasika,
Anga ni kama pazia, mengi limeyafunika.

12. Mawingu yakitandia, viumbe kuhangaika,
Pasi mtu tegemea, na joto hubadilika,
Watoto nao walia, wakifunikwa na shuka,
Anga ni kama pazia, mengi limeyafunika.

13. Tamati nimefikia, utungo umetukuka,
Ufahamu itikia, hakika ninang'atuka,
Utunzi nakuachia, ili uje **tajirika,**
Anga ni kama pazia, mengi limeyafunika.

Baada ya muda wa takribani nusu saa, mvua kubwa iliyoambatana na upepo mkali ilinyesha na kusababisha madhara mbalimbali. Baadhi ya nyumba ziliezuliwa mapaa yake. Aidha, baadhi ya miti mikubwa ilianguka na kuhatarisha usalama wa watu. Mvua hiyo ilidumu kwa muda wa saa mbili na nusu. Baada ya mvua hiyo kwisha, Matera na babu yake, waliwakusanya mbuzi na kurudi nyumbani, ambapo walishuhudia uharibifu mkubwa wa makazi ya watu pamoja na mimea katika mashamba ya watu.

## Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Matera anasoma darasa la ngapi?
2. Shule ya Msingi Ngongongare iko mkoa gani?
3. Matera anaishi na nani?
4. Babu yake Matera anaitwa nani?
5. Matera na Babu yake walikwenda kuchunga mbuzi wapi?
6. Orodhesha madhara manne yatokanayo na mabadiliko ya hali ya hewa.
7. Kwa mujibu wa habari, ni nani aliyetunga shairi kuhusu hali ya hewa?
8. Kwa nini Matera na babu yake walikimbilia pangoni?
9. Mshairi anaposema "**anga linajishitua**" anamaanisha nini?
10. Taja mawazo matatu yanayopatikana katika ubeti wa nne.
11. Shairi hili linatufundisha nini?

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 148 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la pili: Msamiati

**Eleza maana ya maneno yafuatayo, kisha tunga sentensi moja kwa kila neno:**

1. ngurumo
2. rindima
3. dhoruba
4. pazia
5. ukame
6. njaa
7. fukaa
8. hakahaka
9. shaua
10. gharika
11. gubika
12. tajirika

## Zoezi la 3: Mazoezi ya lugha

**A. Kanusha sentensi zifuatazo, kisha upigie mstari neno ulilokanusha:**

**Mfano:** *Matera alimwomba babu yake akachunge mbuzi porini.*

*Matera <u>hakumwomba</u> babu yake akachunge mbuzi porini.*

*Theluji iliyeyuka na kutiririsha maji.*

*Theluji <u>haikuyeyuka</u> na <u>haikutiririsha</u> maji.*

(i) Matera anampenda babu yake.
(ii) Babu anapenda kuimba shairi.
(iii) Walikula chakula kitamu.
(iv) Tunapaswa kuwapenda na kuwajali maadui.
(v) Matera anasoma Darasa la Sita.
(vi) Mvua ilinyesha kwa kishindo.
(vii) Radi ni rafiki kwa maisha ya binadamu.
(viii) Doto aling'atwa na nyuki jana akiwa shambani.
(ix) Nyumba iliezuliwa na upepo.
(x) Mimi nilifurahia safari ya kwenda kwa babu.

**B. Andika wingi wa sentensi zifuatazo:**

(i) Mimi ni mtoto mdogo.
(ii) Mwanafunzi anapaswa kuwa na heshima.
(iii) Shairi linavutia.



FOR ONLINE USE ONLY

KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 149 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(iv) Chui ni mnyama hatari.
(v) Ukungu ulinigubika; sikuweza kuona mbele.
(vi) Mtoto anajua kuruka.
(vii) Mwalimu anasoma gazeti.
(viii) Mzee anaimba wimbo vizuri.
(ix) Yule anajua kusoma vizuri.
(x) Chakula kiliungwa kwa nyanya iliyoiva.

## C. Andika NDIYO kama unakubaliana na maelezo au HAPANA kama hukubaliani na maelezo ya sentensi.

**Mfano:** *Wanafunzi wanatakiwa kutii sheria za shule. NDIYO*
*Radi hupiga miti mifupi. HAPANA*

(i) Upepo ukivuma kupita kiasi, huangusha miti na kuezua nyumba. ________
(ii) Tahadhari kubwa inapaswa kuchukuliwa unapotembea barabarani, hasa wakati wa ukungu. ________
(iii) Hakuna faida yoyote ya kujifunza mabadiliko ya hali ya hewa. ________
(iv) Mvua ikinyesha sana, husababisha ukame. ________________
(v) Baridi inatosha kukuza mazao bila mvua kunyesha. ____________
(vi) Tunapaswa kuvaa sweta wakati wa baridi. ___________
(vii) Baridi kali haina madhara mwilini. ___________
(viii) Shairi linawasilisha ujumbe kwa njia ya mkato.___________
(ix) Shairi la kimapokeo hufuata urari wa vina na mizani. ___________
(x) Mashairi huandikwa kwa kuzingatia alama za uandishi.__________

## D. Badili sentensi hizi kuwa katika kauli taarifa.

**Mfano:** "Mtoto anacheza vizuri," dada amesema.
*Dada amesema kwamba mtoto anacheza vizuri.*

Mwalimu ametuambia, "Kaka amepewa medali ya dhahabu baada ya kuibuka mshindi wa riadha."

*Mwalimu ametuambia kwamba kaka amepewa medali ya dhahabu baada ya kuibuka mshindi wa riadha.*

"Nitasafiri kesho asubuhi," mama alisisitiza.
*Mama alisisitiza kuwa atasafiri kesho asubuhi.*

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 150 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(i) "Mwaka huu nitavuna mazao mengi," mjomba amesema.
(ii) "Kaka yako ni mkorofi sana," Amina aliniambia.
(iii) Kinyonga alitueleza, "Sitahudhuria mkutano."
(iv) Dada aliniambia, "Nitakuletea zawadi."
(v) "Njugumawe zote zimeisha shambani," bibi alisema.
(vi) "Kesho tutakula ubwabwa kwa maharage," mtoto alisema.
(vii) "Mti umeanguka mtoni," mtoto alituarifu.
(viii) "Mimi nitachezea timu ya taifa," mwanafunzi alisema.
(ix) Babu alisema, "Mwaka huu kilimo kimekubali sana."
(x) Mwalimu alitueleza, "Kiswahili kinafundishwa hadi nje ya nchi yetu."

## E. Zungushia herufi katika jedwali hili ili kupata maneno sahihi.

**Mfano:** *CHAI*

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| D | H | U | L | U | M | A | H |
| H | U | R | I | A | H | M | CH |
| A | S | O | N | L | A | A | A |
| H | I | G | R | I | S | N | I |
| A | S | O | I | M | I | I | R |
| M | H | P | M | U | B | E | I |
| A | A | A | U | U | U | A | E |

## F. Jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kutumia maneno yaliyopo kwenye kisanduku.

| |
|---|
| chui, radi, msanii, ukame, ngurumo, pango, ghani, mbuzi, upinde wa mvua, kimbunga |

(i) Sauti ya mvumo inayosikika angani, hasa wakati wa mvua kubwa. _______________
(ii) _________________ ni moja ya wanyama wanaofugwa na binadamu.
(iii) _________________ una rangi saba.
(iv) Upepo unaovuma kwa nguvu na kwa kasi kiasi cha kubomoa majengo, unaitwa _______________
(v) ___________ ni mnyama hatari sana kwa binadamu.
(vi) ___________ ni sehemu kubwa yenye uwazi iliyopo ardhini, kwenye mwamba au mti mkubwa.
(vii) Mng'ao unaotokea ghafla angani kama umeme wakati mvua inanyesha hujulikana kama ____________.



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(viii) __________ ni hali ya kukauka kwa ardhi kutokana na mvua kutonyesha kwa muda mrefu.

(ix) Imba kwa sauti ya kishairi maana yake ni ______________

(x) Mtunzi wa kazi mbalimbali za sanaa huitwa ______________

## G. Jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuchagua neno sahihi kutoka kwenye mabano.

**Mfano:**

Wafuatao ni wanyama wa kufugwa isipokuwa______ (kondoo, mbuzi, nyati, mbwa)

*Wafuatao ni wanyama wa kufugwa isipokuwa nyati.*

Mazoea alikuwa______bustanini. (wanalima, wakilima, analima, wamelima)

*Mazoea alikuwa analima bustanini.*

(i) __________ni aina mojawapo ya samaki.
(mamba, kenge, perege)

(ii) Kitabu __________ kinapendwa na wanafunzi wengi.
(nzuri, vizuri, kizuri)

(iii) Ndugu wa kiume wa damu moja ni ____________
(rafiki, jirani, kaka, mwalimu)

(iv) Hutembea kwa maringo _____________
(nyoka, kinyonga, kangaroo)

(v) Maandishi yaliyowekwa pamoja katika kurasa zilizoandikwa kwa mkono au kuchapwa na kutiwa jalada hujulikana kama ________
(kitabu, shairi, gazeti)

(vi) Kuku ___________ mayai.
(huzaa, hutaga, hutotoa)

(vii) Mimi __________ mtoto mkubwa kwenye familia yetu.
(ndiyo, ndiye, ndie)

(viii) Juma ________________ mpira kila siku.
(atacheza, hucheza, amecheza)

(ix) Jana baada ya timu yetu kushinda, ____________ kwa furaha.
(tutashangilia, tunashangilia, tulishangilia)

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(x) Baba ______________ mti alioupanda kwa panga.
(ameukata, umekatika, umekatwa)

**H. Andika kinyume cha maneno yafuatayo, kisha tunga sentensi moja kwa kila neno:**

**Mfano:** *cheka - nuna*

*Dada alipoanguka alinuna sana.*

(i) kelele ______________
(ii) kunja ______________
(iii) anika ______________
(iv) vaa ______________
(v) ongeza ______________
(vi) giza ______________
(vii) panga ______________
(viii) bandika ______________
(ix) funika ______________
(x) fumba ______________

## Zoezi la 4: Utungaji

**Tunga shairi la kimapokeo lenye beti tano kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa.**

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Nane

## Kusikiliza habari ya madhara ya rushwa

### Utangulizi

*Katika sura hii, utasikiliza habari ya madhara ya rushwa. Pia, utajifunza madhara ya rushwa na namna ya kupambana nayo. Umahiri huu utakuwezesha kukataa, kukomesha na kuwafichua wala rushwa katika jamii.*

### Fikiri



1. Je, umewahi kusikia neno rushwa?
2. Taja mahali ulipolisikia na lilizungumzwaje?
3. Unafikiri ni kwa nini watu hutoa rushwa?

### Ufahamu

*Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

**Pete ya Mtemi Ndamanga**

Ndamanga alikuwa mtemi maarufu wa Nchi ya Mkinza. Umaarufu wake ulitokana na uwezo wake mzuri wa kutawala nchi yake. Pia, aliwaongoza kwa ujasiri askari wake wakati wa vita. Zaidi ya hayo, Ndamanga alimsaidia kila mtu aliyekwenda kwake kuomba msaada. Raia wake wote walimpenda.

Mtemi Ndamanga alikuwa na pete nzuri sana ya ajabu. Pete hiyo iliweza ku**ng'amua** mambo mema na mabaya. Iliweza kung'amua mambo yaliyotokea au yatakayotokea katika nchi yake katika kipindi kifupi kilichopita au kijacho. Iliweza pia kumwonesha mtemi sura za maadui wa nchi yake. Pete hiyo ilikuwa muhimu sana kwake. Kila siku aliitunza mfukoni na kwenda nayo kila mahali.

Siku moja Mtemi Ndamanga na baadhi ya watumishi wake walikwenda kuwinda **wanyamapori**. Siku hiyo haikuwa ya bahati kwao kwani walitembea msituni kwa muda mrefu bila kuua mnyama. Hata hivyo, hawakukata tamaa, kila mara, Mtemi Ndamanga aliwaambia washauri wake, "Siku hazifanani."

Ilipofika saa tisa alasiri, wawindaji walifanikiwa kumuua nyati. Nyati huyo alikuwa mkubwa. Mtemi Ndamanga akasema, "Mnaona sasa! Kila siku tunapata wanyama wadogowadogo, lakini leo tumepata ng'ombe-mwitu."



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 154 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kazi ya kumchuna nyati ikaanza mara moja. Mtemi Ndamanga akapumzika chini ya mti wakati watumishi wake wakimchuna yule nyati.

Walipomaliza kuchuna, Mtemi Ndamanga na watumishi wake wakaanza safari ya kurudi nyumbani. Walifika nyumbani jioni. Walipokaribia nyumbani, walianza kuimba. Walikuwa na kawaida ya kufanya hivyo ili watumishi wengine waharakishe kwenda kuwapokea. Baada ya kupumzika, mtemi Ndamanga alitaka kutazama pete yake. Alitaka kujua mambo yajayo na yaliyotokea alipokuwa mawindoni. Aliitafuta pete yake mfukoni na kila mahali, lakini hakuiona. Mke wake alimsaidia kuitafuta pete hiyo, lakini haikuonekana.

Usiku huohuo, baadhi ya watumishi na watu wengine wengi walikwenda msituni kuitafuta pete ya mtemi. Waliitafuta pete hiyo kwa muda wa siku tatu, lakini haikuonekana. Mtemi Ndamanga akawaambia watu, "Yeyote atakayeniletea pete yangu, nitampa zawadi atakayochagua mwenyewe."

Watu waliposikia ahadi ya mtemi, walikimbilia msituni kuitafuta. Walitafuta kila mahali. Walipekua majani na nyasi zote msituni, lakini hawakuambulia kitu. Mtemi Ndamanga akasikitika sana.

Siku moja kijana aitwaye Bahati aliiokota pete ya mtemi karibu na msitu. Mara tu alipoiokota, alianza safari ya kwenda kwa mtemi. Alipofika kwenye lango kubwa la nje, aliwakuta askari wawili wa zamu. Wale askari wakamkatalia kuingia. Mmoja wao akasema, "Kama unataka kumwona mtemi, lazima utuahidi kuwa utatupatia nusu ya zawadi utakayopata." Bahati akashangaa sana, kisha akasema, "Ninakubali, lakini ni lazima tuandikishane makubaliano haya." Wakaandikishana. Bahati akaiweka mfukoni mwake ile karatasi ya makubaliano, kisha akaongoza njia kwenda kwa mtemi.

Alipofika kwenye lango la pili, Bahati aliwakuta walinzi wengine wawili. Akawaeleza kuwa alitaka kumwona mtemi ili ampe pete yake. Wale walinzi nao wakasema kuwa wasingeweza kumruhusu akaonane na mtemi hadi aahidi kuwa angewapatia theluthi moja ya zawadi atakayopewa. Bahati akakubali, lakini akaomba waandikishane ahadi hiyo. Walipoandikishana, wale walinzi walimfungulia mlango. Bahati aliingia, akaenda moja kwa moja kumwona mtemi.

Bahati alipofika kwa mtemi, alipokelewa kwa mikono miwili. Mtemi Ndamanga alipomwona tu Bahati, moyo wake ulilipuka kwa furaha. Alihisi moyoni kuwa yule kijana alikuwa na jambo zuri la kumwambia. Punde si punde, Bahati alitoa pete akamkabidhi mtemi. Mtemi alifurahi sana. Aliimba na kurukaruka. Mke wake na watoto waliimba na kufurahi pamoja naye. Alipotulia, aliamuru Bahati apewe chakula cha mchana na **karamu** kubwa iandaliwe.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 155 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Usiku, watu wengi walikusanyika nyumbani kwa mtemi wao. Walipewa chakula wakala na vinywaji wakanywa. Baadaye, Mtemi Ndamanga alisimama. Aliwashukuru watu wote waliokusanyika pale na kueleza madhumini ya karamu ile. Alimshika Bahati mkono na kumuuliza, “Niambie, kijana wangu, nikupe zawadi gani? Je, unataka ng’ombe, dhahabu, almasi, au …,” alisita kidogo, kisha akaendelea, “… au unataka sehemu ya nchi yangu?” Bahati aliwaza kwamba amepata nafasi ya kuwakomesha wale walinzi waliomdai **hongo**.

Bahati alisimama, kisha akaanza kuvua nguo zake. Alivua shati na fulana na kuziweka chini. Aliinama, akashika kiti cha mtemi kisha akasema, “Sihitaji chochote kati ya vitu ulivyonitajia. Nataka viboko tisini tu.”

Watu wote pamoja na mtemi walishangazwa sana na maneno ya Bahati. Hawakutarajia kuwa Bahati angechagua viboko badala ya mali. “Viboko tisini!” Alisema Mtemi Ndamanga kwa mshangao. “Kwa kosa gani?” Aliuliza. “Viboko tisini,” alisema Bahati. “Kabla hujanichapa viboko hivyo, naomba niitiwe walinzi wako walioniruhusu kuja kukuona,” Bahati aliongeza.

Mara moja **tarishi** alitumwa kwenda kuwaita wale walinzi. Walipofika pale, kila mtu aliyekuwepo alikaa kimya kuona nini kingetokea. Ndipo Bahati alipomgeukia mtemi na kumkabidhi zile karatasi za makubaliano kati yake na wale walinzi. Bahati akasema, “Ninaomba nigawane zawadi yangu ya viboko tisini na hawa walinzi wako, kama makubaliano yetu yalivyoandikwa kwenye karatasi hizo,” alisema Bahati.


Mtemi Ndamanga alizisoma zile karatasi mbili, kisha akawaelezea watu yaliyoandikwa mle. Watu wote waligeuka na kuwatazama wale walinzi kwa mshangao. Mtemi akaamuru wale walinzi wacharazwe **henzirani** ishirini na tano kila mmoja. Baada ya adhabu hiyo, aliwafukuza kazi. Walinzi walijuta kwa kosa la kutaka kumdhulumu Bahati. Mtemi Ndamanga akawaonya watu wote wenye tabia kama ya wale walinzi, akasema, “Sheria ni **msumeno**, hukata mbele na nyuma.”

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 156 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Mtemi alimsifu Bahati kwa kuwafichua walinzi waovu, kisha akawaambia watu kuwa ahadi ni deni. Akamzawadia Bahati fedha nyingi, ng'ombe mia moja na punda kumi kwa kumpelekea pete yake.

## Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Mtemi Ndamanga alitawala nchi gani?
2. Kwa nini raia wake walimpenda?
3. Kwa nini Mtemi Ndamanga alisema kuwa siku zote hazifanani?
4. Taja majina mengine ya nyati.



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 157 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

5. Nani aliiokota pete ya Mtemi Ndamanga?
6. Ile pete ya ajabu ya Mtemi Ndamanga iliokotwa wapi?
7. Walinzi walitaka Bahati afanye nini ndipo wamruhusu kumwona mtemi?
8. Kama ahadi kati ya Bahati na walinzi wa lango la pili ingetimizwa, walinzi hao wangechapwa viboko vingapi kila mmoja?
9. Kama makubaliano baina ya walinzi wote na Bahati yangetimizwa, Bahati angechapwa viboko vingapi?
10. Methali "Sheria ni msumeno, hukata mbele na nyuma" inatuonya nini?
11. Kama wewe ungeiokota pete ya Mtemi Ndamanga, ungewaambia nini wale walinzi kama wangekulazimisha mgawane zawadi?
12. Umejifunza nini kutokana na habari uliyoisoma?

## Zoezi la pili: Msamiati

**Tunga sentensi mbili kwa kila neno.**

1. ng'amua
2. mnyamapori
3. karamu
4. hongo
5. charazwa
6. henzirani
7. msumeno

## Zoezi la 3: Methali

**Kamilisha methali zifuatazo kwa kuchagua jibu sahihi:**

(i) Hauchi hauchi:

(a) unakucha
(b) unalala
(c) unaamka
(d) ni usiku

(ii) Zimwi likujualo:

(a) liogope
(b) linatisha
(c) halikuli likakwisha
(d) halikuogopi

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(iii) Usipoziba ufa:

(a) watu watakuchungulia
(b) wadudu wataingia
(c) mchwa atakula ukuta
(d) utajenga ukuta

(iv) Mwanzo wa ngoma ni:

(a) mdundo
(b) lele
(c) nyumbani
(d) kucheza

(v) Kwenye miti:

(a) kuna giza
(b) kuna wakwezi
(c) hakuna wajenzi
(d) kunatisha

(vi) Juhudi si:

(a) pato
(b) kazi
(c) mwendo
(d) umakini

(vii) Ari ya mjinga ni:

(a) kilio
(b) jeuri
(c) kusudi
(d) hasara

(viii) Gurudumu la maisha ni:

(a) kubwa
(b) jeusi
(c) duara
(d) tamaa

(ix) Lisilokuja asubuhi:

(a) litakuja mchana
(b) litakuja jioni
(c) haliji tena
(d) halifai

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 159 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(x) Nzi kufa juu ya kidonda:

(a) ni vizuri
(b) si haramu
(c) ni ujinga
(d) si kupenda

## Zoezi la 4: Nahau


**Tunga sentensi kwa kutumia nahau zifuatazo:**

**Mfano:** kata tamaa
*Mvua zilipochelewa kunyesha wakulima walikata tamaa ya kupata mazao mengi.*
pata wakati mgumu
*Wasafiri walipata wakati mgumu basi lao lilipoharibika.*

1. kata tamaa
2. pata wakati mgumu
3. tia hatiani
4. kula yamini
5. pata ahueni
6. tia moyo
7. kaza kamba

## Zoezi la 5: Mazoezi ya lugha

**A. Jaza chemshabongo hii kulingana na maelezo ya kwenda chini na kwenda kulia.**




FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kwenda chini:**

1. Mnyamapori afananaye na ng'ombe (herufi 5)
3. Hali ya kutingishika (herufi 6)

**Kwenda kulia:**

2. Kitu kivaliwacho kidoleni (4)
4. Hali ya mtu kwenda kwa miguu (herufi 6)
5. Hutagwa (herufi 5)

## B. Kanusha sentensi zifuatazo:

**Mfano:** Fundi huyu ameshona nguo zangu vizuri.

*Fundi huyu hajashona nguo zangu vizuri.*

(i) Kiranja amewahi shuleni.
(ii) Mtemi Ndamanga aliwasifia walinzi wadanganyifu.
(iii) Kitabu hiki ni kipya.
(iv) Shule ina upungufu wa samani.
(v) Nyumbani kwetu ni mbali na shuleni.
(vi) Kazi ya kuwinda ina changamoto kubwa.
(vii) Amina aliishia Darasa la Saba.
(viii) Rushwa huwaathiri watu wenye fedha tu.
(ix) Kutembea gizani ni kuzuri.
(x) Maktaba ya shule ina vitabu vingi.

## C. Pigia mstari vielezi vilivyopo katika kifungu cha habari kifuatacho:

Juma na Roda ni watoto wazuri. Bibi yao huwahimiza kwenda shuleni. Juma na Roda wana bidii sana katika masomo. Wao hufanya vizuri kwenye masomo yao. Shuleni, wanapendwa na walimu pamoja na marafiki zao. Juma na Roda wanawatii walimu wao. Pia, wanamtii bibi yao. Bibi akiwaagiza waende kuteka maji, wote kwa pamoja huenda kuteka maji. Wakishaleta maji nyumbani, bibi huwapongeza. Mara kwa mara, bibi huwasimulia hadithi jioni.

## D. Badili kauli taarifa zifuatazo ziwe katika kauli halisi.

**Mfano:** Baba alisema kwamba atanisomesha.

*Baba alisema, "Nitakusomesha."*

(i) Mama aliguna na kusema kwamba nisiende tena kuzurura barabarani.
(ii) Alisema kwamba tumpe chakula chake.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 161 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(iii) Aliwaambia kwamba Mwenyekiti atahutubia mkutano.
(iv) Furaha alisema kwamba bora aache kazi.
(v) Mzee Mwaka alimwambia Adili kwamba rushwa ni adui wa haki.
(vi) Amina alisisitiza kwamba kila kazi ina changamoto zake.
(vii) Mzee Mwande alisema kwamba ni lazima amsomeshe binti yake ili aelimike.
(viii) Daktari alituomba kwamba tujenge wodi mbili.
(ix) Wananchi walisema kwamba watajenga zahanati.
(x) Mwalimu alisema kwamba kazi hiyo imemsaidia sana katika maisha yake.

**E. Unda nomino za mahali kutokana na jedwali lifuatalo:**

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A | B | CH | D | E | F | G | H | I | J | K | L |

| 13 | 14 | 15 | 16 | 17 | 18 | 19 | 20 | 21 | 22 | 23 | 24 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | N | O | P | R | S | T | U | V | W | Y | Z |

**Mfano:**

| 18 | 9 | 14 | 7 | 9 | 4 | 1 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| S | I | N | G | I | D | A |

(i)

| 11 | 9 | 12 | 9 | 13 | 1 | 14 | 10 | 1 | 17 | 15 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | | |

(ii)

| 4 | 15 | 4 | 15 | 13 | 1 |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |

(iii)

| 11 | 1 | 7 | 5 | 17 | 1 |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |

(iv)

| 1 | 17 | 20 | 18 | 8 | 1 |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(v)

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 13 | 22 | 1 | 14 | 24 | 1 |
| | | | | | |

(vi)

| | | | |
|---|---|---|---|
| 13 | 1 | 17 | 1 |
| | | | |

(vii)

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 7 | 5 | 9 | 19 | 1 |
| | | | | |

(viii)

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 13 | 2 | 5 | 23 | 1 |
| | | | | |

(ix)

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 19 | 1 | 2 | 15 | 17 | 1 |
| | | | | | |

(x)

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 17 | 20 | 21 | 20 | 13 | 1 |
| | | | | | |

## F. Panga maneno katika sentensi ili yalete maana.

**Mfano:** *sherehe ni sana chakula cha kitamu*
*Chakula cha sherehe ni kitamu sana.*
*Ndamanga Bahati pete na iliokotwa Mtemi ya*
*Pete ya Mtemi Ndamanga iliokotwa na Bahati.*

(i) shule mdogo awali ya wangu anasoma
(ii) kijijini likizo nitamtembelea wa bibi wakati
(iii) kulipa kukopa matanga harusi
(iv) wimbo kila hana budi mwananchi wa kuufahamu Taifa
(v) mama mkononi jana kwa na niliongea simu ya kutumia
(vi) sana vizuri mwalimu anafundisha wetu
(vii) lugha letu Kiswahili taifa ni ya
(viii) ya tulitembelea Taifa sisi maktaba

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(ix) amefaulu wake Baraka sana mtihani vizuri
(x) yetu miguu shule mashindano wa mpira ya imeshinda

**G. Tunga sentensi sahihi kumi (10) kutokana na jedwali lifuatalo:**

**Mfano:** *Mzee Mwaka alishtuka sana alipokuwa akiwasikiliza.*

*Pendo alitabasamu sana alipokuwa akisema haya.*

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Mzee Mwaka<br>Mjomba<br>Yeye<br>Pendo | alishtuka<br>alinyong'onyea<br>alifurahi<br>alitabasamu<br>alisikitika | sana | alipokuwa | akiwasikiliza<br>akisema haya<br>akisimulia hadithi<br>akiangalia picha |

**H. Oanisha maneno ya safu A na maelezo yake katika safu B ili kuleta maana sahihi. Andika herufi ya jibu kutoka safu B mbele ya neno la safu A.**

| Safu A | Safu B |
|---|---|
| (i) jandoni ______ | (a) kitu chenye thamani na heshima kubwa anachopewa mtu baada ya kufanya kazi nzuri au jambo fulani |
| (ii) unyago ______ | (b) fukuza au andama mnyama ili kumkamata |
| (iii) tuzo _____ | (c) maarifa yanayotolewa kwa mfumo rasmi na usio rasmi |
| (iv) alamsiki _____ | (d) mahali ambapo wavulana waliopevuka hufundishwa mambo ya utu uzima |
| (v) wodi ______ | (e) mtu wa kale |
| (vi) aha! ___ | (f) neno linaloonesha kushangaa |
| (vii) unajimu _____ | (g) elimu ya nyota |
| (viii) uguza ______ | (h) chumba cha hospitali kilichotengwa kwa ajili ya kulaza wagonjwa |
| (ix) winda _____ | (i) mafunzo yanayotolewa kwa wasichana waliopevuka yanayohusu mila za jamii yao |
| (x) mhenga ______ | (j) hudumia au tunza mtu anayeumwa |
| (xi) elimu ______ | (k) tamko la kumtakia mtu heri wakati wa kuagana usiku, usiku mwema |

## Zoezi la 6: Utungaji

**Tunga habari inayohusu rushwa yenye maneno kati ya mia moja (100) na mia moja ishirini (120).**



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 164 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Tisa

## Kubaini hoja katika majadiliano

### Utangulizi

*Katika sura hii, utajifunza namna ya kubaini na kuchambua hoja kuu zilizotolewa katika majadiliano. Umahiri huu utakusaidia kubaini na kuandaa hoja katika mikutano na vikao mbalimbali. Pia, itakusaidia kujifunza na kuelewa kwa urahisi masomo yako.*

### Fikiri



1. Ulishawahi kuhudhuria mdahalo?
2. Mdahalo huo ulihusu nini?
3. Mambo gani uliyojifunza katika mdahalo huo?

### Ufahamu

*Soma hadithi ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

**Urafiki wa mashaka**

Katika pori la Wachuki waliishi wanyama wengi na wa aina mbalimbali. Palikuwa na wanyama kama vile digidigi, twiga, tembo, nyati, chui, fisi, simba na wengine wengi. Wanyama hao waliishi kwenye vikundi vya **jamii** moja. Digidigi aliishi na digidigi wenzie. Fisi aliishi na fisi wenzie na simba aliishi na simba wenzie. Baadhi ya jamii za wanyama zilikuwa zinatawala wanyama wa jamii nyingine. Hivyo, jamii hizo zilichukiana na kuogopana sana. Siku moja, mtoto wa digidigi alipotea njia. Alipokuwa anahangaika kumtafuta mama yake alikutana na mtoto wa simba. Kila mmoja alimshangaa mwenzake kwa vile walikuwa hawajawahi kuonana. Walirukaruka huku na huko wakicheza michezo ya kitoto. Michezo iliwanogea kiasi kwamba mtoto wa simba alisahau kurudi kwao na mtoto wa digidigi alisahau kuendelea kumtafuta mama yake.

Huko nyuma, Mama Digidigi aliingiwa na wasiwasi. Alihofu kuwa mwanaye ameliwa na wanyama wakali. Alihangaika kumtafuta kwa uchungu hadi jioni, lakini hakumwona. Jua lilipokuwa likitua, alikumbuka kuwa kulikuwa na sehemu moja ambayo alikuwa hajaenda kumtafuta. Aliondoka mbio. Baada ya muda

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 165 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

mfupi, alifika huko. Alishangaa kumwona mwanaye anacheza na mtoto wa simba. Alipotaka kumchukua, mwanaye alikataa na kulia sana. Akasema, “Mama, mimi ninataka kwenda na huyu rafiki yangu.” Mama Digidigi aliposikia hayo, alizidi kuchanganyikiwa. Alimwambia mwanaye kuwa simba na digidigi ni maadui. Alimhimiza mwanaye waondoke waende nyumbani haraka wasije wakaliwa na simba.

Mtoto wa simba alimwomba Mama Digidigi akasema, “Mama naomba niende naye. Nitawaomba wazazi wangu wasim**dhuru** kwani yeye ni rafiki yangu. Nakuahidi kuwa nitamrudisha kwako akiwa salama kabisa”. Mtoto wa simba alipokuwa akisema maneno hayo, digidigi mdogo alirukaruka na kum**ng’ang’ania** mtoto wa simba.

Kwa shingo upande, Mama Digidigi alimruhusu mwanaye aende na mtoto wa simba. Alirudi nyumbani akiwa na **majonzi** makubwa. Moyoni aliwaza jinsi mwanaye atakavyo**raruliwa** na **nduli** wale. Kesho yake, Mama Digidigi alishtuka na kushangaa alipowaona Simba na wanawe wameongozana na mwanaye kuja nyumbani kwake. Alitetemeka kwa woga akataka kukimbia. Ali**shuku** kuwa huo ulikuwa mwisho wa maisha yao. Kwa kuwa alikuwa anampenda mwanaye, aliamua kutokimbia ili afe pamoja naye. Simba walimsogelea bila kuonesha chuki yoyote. Waliketi karibu naye wakionesha nyuso za tabasamu.

Walimweleza Mama Digidigi kwamba wao hawakuja kwa **shari** bali wamekuja kama marafiki. Walimwambia Mama Digidigi, “Sisi tumetumwa kwenu kuwaeleza kuwa, tuache uadui. Tangu sasa, jamii ya Simba na jamii ya Digidigi ni marafiki.” Kuanzia siku hiyo, Digidigi na Simba walianza kutembeleana. Walipelekeana zawadi nyingi.

Siku moja, kulikuwa na ngoma kwa akina Simba. Jamii ya akina Digidigi ilialikwa. Walipofika walikaribishwa wakapewa vyakula na vinywaji. Baada ya chakula shamrashamra za ngoma zilianza. Loo! Akina Digidigi walicheza mpaka jasho likawatoka. Simba nao walicheza vizuri. Kila mmoja alifurahi.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 166 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Kadiri muda ulivyokwenda, ndivyo utamu wa ngoma ulivyokolea. Baada ya muda, simba mmoja alijisahau akaanza kuonesha dalili za kutaka kumdhuru digidigi. Digidigi aliyekuwa akicheza naye alitambua. Ali**toa ishara** ya kuonesha kuwa kulikuwa na hatari. Aliwaambia wenzake kwa lugha yao "Jamani mimi nina wasiwasi na hawa wenzetu. Dalili ya mvua ni mawingu. Huyu simba ninayecheza naye ananimezea mate. Tukimbie tusije tukaliwa." Mara wote walikimbia kama mishale. Simba walipoona hivyo walisahau ahadi yao ya urafiki wakaanza kuwafukuza. Hata hivyo, hawakuambulia kitu. Digidigi walikuwa wepesi. Waliweza kukimbia kwa kasi na kufika kwao salama salimini.

Kesho yake asubuhi, Digidigi wote walikusanyika nyumbani kwa **kiongozi** wao. Yule kiongozi aliwaambia, "Ninyi hamkutaka kunisikiliza nilipowatabiria tangu mwanzo. Mimi nilijua ule haukuwa urafiki wa kweli. Zile zilikuwa mbinu za akina Simba za kutupata kwa urahisi. Nashukuru mmerudi salama. Nawaambia kwamba, tangu sasa, urafiki wa kinafiki kama huu uishe.

Tangu siku hiyo, uadui kati ya Digidigi na Simba ulirudi upya. Ndiyo maana kila mara digidigi wamwonapo simba hujihami kwa ku**timua mbio**.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 167 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la Kwanza: Ufahamu

1. Nani walikuwa chanzo cha kuanzisha urafiki kati ya Simba na Digidigi?
2. Kwa nini Mama Digidigi alishtuka alipomwona mwanaye anacheza na mtoto wa Simba?
3. Hoja gani ilitolewa na mtoto wa Simba mpaka Mama Digidigi akamruhusu mwanaye aende naye?
4. Je, ungekuwa wewe ni Mama Digidigi ungemruhusu mtoto wako aende na simba? Kwa nini?
5. Kwa nini Mama Digidigi alikuwa na huzuni alipomruhusu mwanawe aende kwa Simba?
6. Digidigi mmoja alijadiliana nini na wenzake kwa ishara?
7. Kulitokea nini wakati wa ngoma hata Digidigi wakaamua kukimbia?
8. Eleza maana ya methali “Dalili ya mvua ni mawingu” kama ilivyotumika katika hadithi.
9. Je, kama Digidigi na Simba wangeendelea kucheza ngoma kungetokea nini?
10. Kwa nini pori lile liliitwa pori la Wachuki?
11. Hadithi hii inatufundisha nini?

## Zoezi la pili: Kazi ya kufanya

**Igiza na wenzako hadithi uliyoisoma.**

## Zoezi la 3: Msamiati

**Andika maneno yenye maana sawa na haya yafuatayo, kisha tunga sentensi moja kwa kila neno:**

| |
|---|
| **jamii, dhuru, ng’ang’ania, majonzi, rarua, nduli, shuku, shari, kiongozi** |

**Mfano:** *shari – ugomvi*

*Mtoto mwema ni yule asiyependa shari na wenzake.*

## Zoezi la 4: Methali

**Kamilisha methali zifuatazo:**

1. Chanda chema, …………………………………….
2. ……………………………………., ndiyo upatao.
3. Mkono mmoja, …………………………..………

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 168 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

4. ……………………………, hufa angali maskini.
5. Siku njema, ………………………………
6. ……………………………, hakataziki maziwa.
7. Mfa maji, ………………………………
8. ………………………………, usiku atakuchoma.
9. ………………………, hata maji hujipaka.
10. Mkono uliotia jiwe majini, ……………………

## Zoezi la 5: Nahau na misemo

**Oanisha sehemu A na sehemu B ili kukamilisha maana za nahau na misemo ifuatayo:**

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| (i) teka nyara | (a) toka mahali mbio |
| (ii) nyoosha mambo | (b) kasirika |
| (iii) ota mizizi | (c) wasiliana kwa kutumia vitendo |
| (iv) miguu hii ni yako | (d) fikiri sana |
| (v) kaa chonjo | (e) stawi au dumu |
| (vi) chemshabongo | (f) fanya mambo yawe mazuri |
| (vii) nyoka wa ndumilakuwili | (g) chukua kama mateka |
| (viii) chanja mbuga | (h) nimekuja kwako kwa shida fulani |
| (ix) kunja ndita | (i) mjinga |
| (x) charaza maneno | (j) mtu hatari anayejifanya rafiki |
| (xi) kichwa maji | (k) kimbia ili kuepuka hali fulani |
| (xii) timua mbio | (l) sema harakaharaka kwa nia ya kudanganya |
| (xiii) piga ishara | (m) chukua tahadhari |

## Zoezi la 6: Mazoezi ya Lugha

**A. Unda maneno sahihi kumi (10) kwa njia ya kujirudiarudia.**

**Mfano:** taka - *takataka*
pili - *pilipili*

**B. Tunga sentensi mbili zenye maana tofauti kwa kutumia maneno yafuatayo:**

**Mfano:** Paa - ***Paa*** *la nyumba yetu limepakwa rangi nyekundu.*
*Tiara ili**paa** angani kama mwewe.*

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 169 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(i) paa
(ii) kaa
(iii) taa
(iv) sita
(v) ndege
(vi) meza
(vii) ua
(viii) mbuzi
(ix) jua
(x) mwezi

## C. Andika sentensi zifuatazo kwa usahihi.

**Mfano:** Mazao yamejaa wingi darini.
*Mazao yamejaa kwa wingi darini*.

(i) Behewa ya mizigo limedondoka.
(ii) Nywele wangu wamekuwa ndefu.
(iii) Mwanafunzi wengi waliwahi kupata chanjo.
(iv) Nyota imetanda anga yote.
(v) Macho ina kope.
(vi) Ndugu yangu unaitwa nini?
(vii) Funua ukurasa wa kitabu vyako.
(viii) Sisi sote afanye kazi kwa bidii.
(ix) Nta wananata sana.
(x) Mafisi wanacheka msituni.

## D. Panga herufi zifuatazo ili kupata maneno sahihi.

**Mfano:** IASRHA - *ISHARA*

(i) AONGTZA
(ii) JHAO
(iii) ALIJAMANODI
(iv) RUHEFI
(v) OTSE
(vi) THLAETHNII
(vii) LIKIHISWA
(viii) DGIIDGII
(ix) OMBGO
(x) IKANY

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 170 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**E. Badili sentensi zifuatazo kuwa katika uyakinishi**

**Mfano:** Mama na baba hawakuamka asubuhi kunitakia heri ya mtihani.
*Mama na baba waliamka asubuhi kunitakia heri ya mtihani.*

(i) Fundi seremala hakuja kwa wakati.
(ii) Hazifanyi kazi zake kwa umakini mkubwa.
(iii) Jiko lote halikujaa moshi kwa ajili ya kuni.
(iv) Barabara zote hapa kijijini kwetu hazipitiki kwa urahisi.
(v) Kazi ya uvuvi haifanyiki wakati wa usiku.
(vi) Dada na kaka hawakusafiri wakati wa likizo fupi.
(vii) Bibi hatafuni chakula kwa urahisi.
(viii) Hatukupalilia mazao yetu mapema mwaka huu.
(ix) Banda halitatosha vifaranga wote.
(x) Unga haukusagwa vizuri na mashine ya Mzee Kazimoto.

**F. Pigia mstari viwakilishi katika sentensi zifuatazo:**

**Mfano:** <u>Wale</u> ndiyo waliofanikiwa kufika katika kilele cha mlima Kilimanjaro.
<u>Mimi</u> ndiye kitinda mimba.

(i) Wao wanalima mazao yao ya biashara.
(ii) Nani atamfunga paka kengele?
(iii) Yeye anasumbua kula chakula.
(iv) Sisi tutafanya mitihani yetu ya kufunga shule wiki ijayo.
(v) Ninyi mtafyeka vichaka kuweka mazingira yote safi.
(vi) Wewe ndiye niliyekuwa nakutafuta.
(vii) Yule ni mchezaji hodari wa mpira wa miguu.
(viii) Mimi na yeye tunashirikiana katika masomo yetu.
(ix) Sisi na wao tutakwenda kutembelea mbuga za wanyama.
(x) Wale ni wauguzi waliokuja shuleni kwetu kutupatia chanjo ya homa ya manjano.

## Zoezi la 7: Utungaji

**Tunga habari ya maneno yasiyozidi mia moja (100) kuhusu likizo yako.**

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 171 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Ishirini

## Kusoma kwa ufasaha

### Utangulizi

*Katika sura hii, utajifunza kusoma kwa kuzingatia alama za uandishi. Pia, utajifunza mbinu za kusoma kwa kasi na kwa usahihi. Umahiri huu utakuwezesha kuwa msomaji mzuri katika hadhara yoyote.*

### Fikiri



1. Je ulishawahi kumsikiliza mtu akisoma kitabu au habari yoyote?
2. Je, ulivutiwa na usomaji wake? Kwa nini?

### Ufahamu

*Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

**Mafanikio ya Masaka**

Masaka ni mmoja kati ya watoto wa familia ya mzee Gibogo. Kipato cha familia yao kilikuwa kidogo sana kikilinganishwa na kipato cha majirani waliowazunguka. Chakula kilipatikana kwa kubahatisha. Mzee Gibogo hakuwa na shamba wala bustani ya kuotesha hata mboga za majani. Alijishughulisha na **vibarua** vya hapa na pale. Mama yake alijishughulisha na kazi ya kuuza maandazi. Hata hivyo, kipato cha familia kilizidi kuporomoka. Katika kupambana na ugumu wa maisha, Mzee Gibogo alianza kufanya kazi ya ulinzi.

Mzee Gibogo na mkewe aitwaye Teleza walijitahidi kutimiza wajibu wao wa kuitunza familia. Hata hivyo, mambo yaliwaendea **mrama** licha ya jitihada walizozionesha. Walipata fedha **kiduchu** ambazo hazikutosheleza mahitaji. Walikula mlo mmoja tu kwa siku. Kwa kuwa walikuwa na majukumu **lukuki** yaliyohitaji fedha, hali ya maisha ilizidi kuwa ngumu sana.

Mawazo yakawa mawazo, wakapanga na kupangua na majibu hayakupatikana. Mzee Gibogo hakuwa akipata usingizi tena kwani maisha yalionekana kumwelemea. Aliwaza na ku**nong'ona**, "Hali hii mwisho wake ni lini?" Mavazi ya Masaka yalionekana kuchakaa. Shuleni alivaa kaptura yenye **viraka**. Wanafunzi wenzake walimwangalia na kunong'onezana, lakini yeye hakujali. Badala yake, aliamini kuwa ipo siku maisha yatabadilika. Sabuni ya kufulia

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

ilipatikana kwa shida na, wakati mwingine, haikupatikana kabisa. Wadogo zake pia walitia huruma kwa mwonekano wa mavazi chakavu.

Ilikuwa yapata saa mbili jioni, siku ya Alhamisi. Masaka alikuwa amekaa na baba yake nje wakiota moto. Aliwaza na kumuuliza baba yake, "Samahani baba, ipo siku ambayo tutakula chakula kizuri kama wengine?" Baba yake hakuwa na jibu la haraka. Machozi yalimlengalenga kwa muda. Baadaye kidogo, mazungumzo yao yakaendelea. Masaka akamdokezea baba yake wazo la kuanzisha biashara ndogondogo kama ya kuuza karanga. Aliamini kwamba biashara itawasaidia kuondokana na maisha magumu. Vilevile, aliamini kuwa juhudi katika biashara yake italeta mabadiliko kwenye familia yao. Pia, aliamini kwamba biashara hiyo itaweza kusaidia upatikanaji wa chakula na mahitaji mengine.

Masaka hakuwa na mtaji wa kuanzisha biashara, ila wazo la biashara lilikuwa liki**gonga** akilini mwake. Ilimbidi amwombe baba yake kiasi chochote cha fedha ili kiwe **mtaji**. Baba yake alikubali kumpatia shilingi elfu ishirini. Masaka aliipokea fedha hiyo kwa furaha. Alishukuru sana kwani aliamini kupata mafanikio makubwa kupitia fedha hiyo. Muda si mrefu, Masaka akaanza kununua karanga kwa ajili ya kuuza. Alizikaanga vizuri na kuzifunga kwenye mifuko midogomidogo.

Masaka, alimwomba baba yake ruhusa ya kuuza karanga kila siku baada ya masomo. Baba yake alimruhusu naye akaanza kazi. Mtaji wa Masaka ulizidi kukua siku hadi siku. Baada ya miezi mitatu, mtaji ulikua na kufikia shilingi elfu hamsini. Baada ya miezi sita, mtaji uliongezeka na kufikia shilingi laki tatu.

Biashara ya Masaka ili**nawiri** kadiri siku zilivyosonga mbele. Familia yao ikaanza kula chakula kizuri. Masaka akatenga kiasi fulani cha fedha na kumpatia baba yake kama mtaji wa kuanzishia biashara ndogondogo. Mzee Gibogo hakuamini macho yake. Tangu siku hiyo, mzee Gibogo akaachana na kazi ya kufanya vibarua na kuanzisha biashara ya dagaa. Kwa kuwa aliona biashara itampatia mafanikio makubwa kuliko vibarua, aliongeza jitihada zaidi za kuiboresha. Alifahamu kuwa siri ya mafanikio katika biashara ni kutumia lugha nzuri kwa wateja. Kwa kufanya hivyo, alipata **wateja** wengi zaidi kuliko wauzaji wengine. Hakika ali**shuhudia** mafanikio makubwa. "Kumbe! Vibarua vinanipotezea muda", alijisemea mzee Gibogo.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Kwa upande mwingine, Masaka alisoma kwa bidii. Walimu walimpenda na wanafunzi wenzake pia. Kila walipofanya mitihani, Masaka alishika nafasi ya kwanza darasani. Matokeo ya mtihani wa Darasa la Saba yalipotoka, alikuwa miongoni mwa wanafunzi wachache waliofaulu na kuchaguliwa kujiunga na elimu ya sekondari. Masaka alifanya maandalizi na hatimaye, akajiunga na elimu ya sekondari. Aliendelea kufanya vizuri katika masomo yake.

Biashara iliendelea huku Masaka akiwa masomoni. Baba yake alimsaidia kusimamia biashara na kuajiri wafanyakazi. Aliajiri watu waliomsaidia kazi huku akiwa masomoni. Biashara ilizidi ku**shamiri** na kukua kwa kasi. Aliendelea na masomo na akahitimu kidato cha nne.

Alifaulu mtihani na kuchaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha tano. Huko, alisoma kufa na kupona. Alipofanya mtihani wa kidato cha sita, alifaulu vizuri. Alichaguliwa kujiunga Chuo Kikuu cha Dodoma. Huko, alisomea **Shahada** ya Uongozi katika Biashara. Baada ya kuhitimu masomo yake, alirejea nyumbani kwao. Alipokelewa kwa heshima kubwa na kufanyiwa sherehe ya kupongezwa.

Masaka alitumia elimu aliyoipata chuo kikuu kupanua miradi yake. Alijenga kiwanda cha mafuta ya karanga na ya alizeti. Pia, alianzisha **kampuni** ya usafirishaji. Hakika mambo yalimwendea vizuri. Kwa sasa, Masaka amefanikiwa kimaisha na ameajiri watu wengi kwenye miradi yake. Yeye ni mwaminifu katika kulipa **kodi.** Anajua umuhimu wa kutoa kodi katika kuchangia na kuinua pato la taifa. Pia, Masaka ana moyo wa uzalendo na anapenda mafanikio ya wengine. Kwa ubunifu wake, ametengeneza ajira na kuajiri watu wengi. Ameinua pato la kijiji na jamii yake kwa ujumla. Ama kweli wahenga walisema, “Penye nia pana njia.”

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Taja majina ya wazazi wa Masaka.
2. Mama yake Masaka anajishughulisha na nini?
3. Siku ipi Masaka alikuwa na mjadala na baba yake?
4. Masaka alipewa shilingi ngapi na babaye kama mtaji?
5. Katika hatua ya mwanzo, Masaka alifanya biashara gani?
6. Mtaji wa Masaka ulifikia shilingi ngapi baada ya miezi sita?
7. Baada ya kuachana na kazi ya kufanya vibarua mzee Gibogo alianzisha biashara gani?
8. Unafikiri ni kwa nini mzee Gibogo alikuwa na wateja wengi zaidi kuliko wauzaji wenzake?
9. Taja jina la chuo ambacho Masaka alisoma.
10. Masaka alipohitimu chuo kikuu, alifanya nini?
11. Eleza umuhimu wa kulipa kodi.
12. Wewe ungepewa mtaji kama aliopewa Masaka, ungefanya biashara gani? Kwa nini?

## Zoezi la pili: Msamiati

**Tunga sentensi moja kwa kila neno.**

1. vibarua
2. mrama
3. kiduchu
4. lukuki
5. nong'ona
6. viraka
7. gonga
8. mtaji
9. nawiri
10. wateja
11. shuhudia
12. shamiri
13. shahada
14. kampuni
15. kodi

## Zoezi la 3: Miundo

**Tunga sentensi mbili kwa kila muundo.**

1. ……………….. ndivyo ………………….

   **Mfano:** *Hivi **ndivyo** walivyotuelekeza walimu.*

2. ……………….. ndicho ……………………

   **Mfano:** *Hiki **ndicho** kikapu kilichosukwa kwa ukili.*

3. ……………….. ndimo ………………………

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Mfano:** *Humu* ***ndimo*** *wanamoishi siafu.*

4. ……………….. ndiko ………………………..

**Mfano:** *Nyumbani kwao* ***ndiko*** *kunakopatikana maembe mengi.*

5. ……………… ambalo ……………………….

**Mfano:** *Shamba* ***ambalo*** *limepandwa migomba, limeuzwa.*

6. …………………… ambayo …………………..

**Mfano:** *Mafuta* ***ambayo*** *tunayatumia yanatoka kwenye kiwanda cha Masaka.*

## Zoezi la 4: Mazoezi ya lugha

**A. Tunga sentensi kumi na tano (15) kwa kutumia jedwali lifuatalo.**

| | | |
|---|---|---|
| Mtoto wangu<br>Baba yangu<br>Shangazi<br>Mdogo wangu<br>Mwalimu | anasoma<br>anakwenda<br>anafundisha | Darasa la Sita<br>chuo kikuu<br>sekondari<br>shule ya msingi<br>Chuo cha Usafirishaji |

**B. Andika sentensi zifuatazo kwa kutumia alama sahihi za uandishi.**

(i) Umaskini mara nyingi unatokana na kutokuwa na mpangilio mzuri wa kazi
(ii) Juma aliweka akiba ya fedha na chakula kwa ajili ya maisha ya baadaye
(iii) Mama yako anafanya kazi gani
(iv) Kilimo cha matunda nafaka na mbogamboga kina manufaa kwa jamii
(v) Masaka alifanya biashara ya karanga dagaa vitumbua na magari
(vi) Loo mbuzi ameanguka shimoni
(vii) Baba yangu anaitwa Mashaka
(viii) Mafanikio huanza kwa kutunza fedha kidogokidogo
(ix) Mama anauza vitumbua baba anafanya kazi ya ulinzi
(x) Wewe unaitwa nani kaka aliuliza

**C. Andika sentensi hizi kwa usahihi.**

**Mfano:** Mtungi kimevunjika.
*Mtungi umevunjika.*
Mvua amesababisha utelezi njiani.
*Mvua imesababisha utelezi njiani.*

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 176 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(i) Mtoto lilianguka chini kwa kishindo.
(ii) Chuma kilichokatwa ameibwa leo.
(iii) Jifunze biashara ukiwa na elimu la msingi.
(iv) Dada kakubwa anacheza mpira vizuri.
(v) Mwalimu Kilima anatufundisha kasomo kamoja.
(vi) Baba changu ni mfugaji wa nyuki.
(vii) Kengele kaligongwa saa sita mchana.
(viii) Nyaigera ni kitongoji ndani ya kijiji la Kemakorere.
(ix) Doto ndimi mkulima wa pamba.
(x) Viti vilivyopangwa vizuri yameanguka chini.

**D. Andika neno moja linalobeba maana ya maneno yote kwa kila kifungu cha maneno.**

**Mfano:** parachichi, embe, ndizi, chungwa (matunda)
suruali, shati, sketi, gauni (mavazi)

(i) kitumbua, andazi, mkate, chapati ________________
(ii) nyama, samaki, dagaa ________________
(iii) Manyara, Mwanza, Kigoma, Mbeya ______________
(iv) Januari, Machi, Aprili, Julai ______________
(v) Serengeti, Saadani, Ruaha, Mikumi ______________
(vi) ghorofa, tembe, msonge ________________
(vii) Oksijeni, Haidrojeni, Kabonidaiyoksaidi, Naitrojeni ___________
(viii) nyanya, karoti, vitunguu, hoho ________________
(ix) kinyonga, nyoka, mjusi, kobe ______________
(x) hereni, shanga, mkufu, pete ______________

**E. Andika sentensi zifuatazo katika wakati ujao**

**Mfano:** Mjomba anapalilia vitunguu vyake.
*Mjomba atapalilia vitunguu vyake.*
Barabara nzuri zilijengwa hapa kwetu.
*Barabara nzuri zitajengwa hapa kwetu.*

(i) Familia ya mzee Gibogo iliishi maisha ya dhiki.
(ii) Masaka aliridhika na hali ya maisha.
(iii) Mzee Gibogo aliishi kwa kufanya vibarua.
(iv) Mke wa mzee Gibogo aliuza maandazi.
(v) Vijana wanapaswa kuwa na fikira chanya kama Masaka.
(vi) Kaka yangu alianzisha mradi wa kuuza karanga.
(vii) Mdogo wangu hashindwi kwenda shuleni kwa sababu ya kukosa sare za shule.



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(viii) Taifa linajengwa kwa kodi tunazolipa.
(ix) Maisha yalibadilika na kuwa mazuri sana.
(x) Masaka alionesha uthubutu kwa kufanya biashara.

**F. Badili sentensi zifuatazo ziwe katika kauli ya kutendewa.**

**Mfano:** *Babu amechonga kinyago kizuri.*
*Babu <u>amechongewa</u> kinyago kizuri.*
*Timu ilifunga goli la kwanza kwa kichwa.*
*Timu <u>ilifungiwa</u> goli la kwanza kwa kichwa.*

(i) Shangazi amepasua kuni zote zilizokuwa nje ya nyumba.
(ii) Mwanafunzi amesoma kitabu cha Kiswahili.
(iii) Dada amepika ugali laini sana.
(iv) Ng'ombe ameangusha mti uliokuwa pembeni mwa nyumba yetu.
(v) Mwanafunzi ametoka darasani.
(vi) Yahaya alichota maji ya kuoga.
(vii) Baba anapika viazi kwa kutumia jiko la gesi.
(viii) Masaka anafuga kuku wa kienyeji kwa ajili ya kuuza.
(ix) Kijana atacheza mpira vizuri.
(x) Msami ameandika barua kwenda kwa rafiki yake.

**G. Soma kifungu cha habari, kisha uweke alama za uandishi na herufi kubwa panapostahili.**

mimi ninaitwa fikiri na baba yangu anaitwa mawazo mimi na baba yangu tumejenga nyumba nzuri juu ya mlima mrefu tumeamua kufanya hivyo baada ya kuvamiwa na wanyama wakali wanyama hao walikuwa hatari kwa maisha yetu mwanzoni baba alitoa wazo la kuhamia kijiji kingine baada ya kufikiri sana nilimshauri baba tujenge nyumba juu ya mlima mrefu baba alikubali ushauri wangu.

Kazi ilianza na hatimaye nyumba ilikamilika nyumba ilikuwa imara sana ilijengwa kwa nondo matofali saruji mbao mawe juu ya mlima tuliojenga nyumba wanatua ndege wa kila aina hatupati shida ya kitoweo ndege hao wanaingia ndani ya nyumba na tunawakamata kwa urahisi pia miti ya matunda ya kila aina inapatikana juu ya mlima huo tunapata wageni wengi. Wanakuja kununua matunda na nyama ya ndege.

## Zoezi la 5: Utungaji

**Andika habari yoyote yenye maneno kati ya mia moja (100) na mia moja ishirini (120).**



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 178 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Ishirini na Moja

## Kusoma kwa burudani

### Utangulizi

*Katika sura hii, utajifunza kusoma hadithi kwa burudani kwa kuzingatia alama zote za uandishi. Vilevile, utafanya mazoezi mbalimbali ya lugha. Umahiri huu utakusaidia kujenga utamaduni wa kujisomea kazi mbalimbali za kawaida na za fasihi ambazo zitakuza uwezo wako katika matumizi ya lugha. Pia, itakusaidia kupata taarifa na maarifa mbalimbali.*

### Fikiri



1. Vitu gani vinakuburudisha? Kwa nini?

### Ufahamu

*Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

**Kisa cha Mamba na Mbuni**

Hapo zamani za kale, **Mamba** na **Mbuni** walikuwa marafiki. Walikuwa wakishirikiana katika mambo mengi. Pia, walikuwa wakitembeleana. Mamba alikuwa akimchukua Mbuni hadi nyumbani kwake kwenye miamba kandokando ya mto. Alikuwa anamwandalia samaki wazuri kwa ajili ya chakula. Mbuni naye alikuwa akimkaribisha Mamba nyumbani kwake kwenye **chaka** kubwa mbali kidogo na mto. Alikuwa anamtayarishia wadudu na wanyama wadogowadogo kama panya na mijusi. Mamba alikuwa anafurahia sana mlo huo. Mbuni alikuwa akipenda kwenda kunywa maji pembeni mwa mto.

Mamba naye alikuwa akiwinda wanyama wadogowadogo kandokando ya mto. Alikuwa haendi mbali kwani alikuwa anaogopa sana binadamu. Binadamu walikuwa wanamwinda Mamba ili wachukue ngozi yake. Ngozi ya Mamba ni mali. Hutumika kutengenezea viatu, mikanda na mikoba. Pia, hutumika kutengenezea mapambo. Tena, binadamu anapenda sana mafuta ya Mamba kwani ni dawa. Mbuni na Mamba walikubaliana kusaidiana katika ulinzi. Mbuni akienda kunywa maji, Mamba amchunge ili asije akapatwa na matatizo huko mtoni. Mamba alikuwa akizungukazunguka huku na kule ili aweze kumw**okoa** rafiki yake endapo atapatwa na shida. Mbuni naye alikuwa anachunga adui, yaani binadamu, ili wasije wakamdhuru Mamba awapo




KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 179 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

mawindoni. Mbuni akiona binadamu, alikuwa anampasha Mamba habari mara moja ili arudi zake mtoni. Kwa hiyo, urafiki wao uliendelea kwa muda mrefu.

Siku moja, Mamba alienda kumtembelea Mbuni. Wakati wote walipokuwa wanaongea, Mbuni alikuwa amekaa tu. Kumbe alikuwa anaatamia mayai yake. Mamba alimshangaa Mbuni kwa kuwa alikuwa hajui kama mayai hulaliwa. Yeye anapotaga ya kwake huyafukia kwenye udongo na kukaa pembeni kuyalinda hadi watoto wanapoanguliwa. Mamba akamuuliza Mbuni, “Unalalia mayai yako kwa muda gani?” Mbuni akajibu, “Ninayalalia kwa muda wa siku arobaini na mbili. Joto la mwili wangu hufanya kifaranga kikomae haraka ndani ya yai, na baadaye hu**anguliwa**.” Mbuni naye akauliza, “Je, wewe ukitaga mayai na kuyafukia unayangoja kwa muda gani hadi yatoe watoto?” Mamba akajibu, “Nikishayafukia, ninayangojea kwa muda wa miezi mitatu. Wakati wote huo ninakaa palepale karibu ili kulinda ma**adui** wasipite na kuyaharibu.”

Siku moja, Mbuni alikuwa akipita kando ya mto. Alitaka kunywa maji na kum**sabahi** rafiki yake. Mamba akajitokeza ukingoni mwa mto, wakaanza kuongea. Walipokuwa wakizungumza, Mbuni aligundua kuwa sauti ya Mamba haikuwa ya kawaida. Ilikuwa inakwaruza kidogo. Akamuuliza, “Rafiki yangu, mbona leo sauti yako imebadilika?” Mamba akajibu, “Ndiyo! Koo langu linawasha. Ninatamani kulikuna, lakini kila nikiingiza vidole havifiki huko. Labda pana vijipele vidogo.” Mbuni akasema, “Pole sana. Chuma majani ya mti uleee! Uyatumie. Ni dawa nzuri sana.”





KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 180 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mamba alifikiri kidogo, kisha akasema, "Rafiki yangu, naomba unisaidie kwa njia nyingine. Wewe una mdomo mrefu. Unaweza kunisaidia kukuna koo langu." Mbuni alifikiri, kisha akasema, "Naogopa hayo meno yako, makali sana. Yanaweza kuni**umiza**." Mamba akajibu, "Loo! Siwezi kukuumiza rafiki yangu. Naomba unisaidie kidogo tu ili nipate ahueni." Mbuni alikubali.

Mamba alifungua mdomo wake kwa nguvu. Mbuni aliingiza kichwa chake taratibu ndani ya kinywa cha Mamba. Alianza kudonoadonoa kooni mwa Mamba. Mwanzoni, Mamba alifurahia, lakini baadaye, alianza kupata maumivu. Kwa sababu alikuwa amefungua kinywa chake, hakuweza kuzungumza.

Mbuni aliendelea kudonoa. Ghafla, Mamba akafunga mdomo wake kwa nguvu. Mbuni alianza kuhangaika. Alijivuta kichwa chake lakini Mamba alikuwa amembana kwa meno yake. Mbuni aliendelea kujivuta na kutaka kuji**nasua** hadi jasho likamtoka. Alipigapiga mabawa yake na kulia kwa uchungu kwani alidhani kuwa angekufa. Alimkwaruza Mamba kwa makucha yake, lakini haikufaa kitu. Mbuni aliendelea kuvuta kichwa chake. Mwisho, Mamba akafungua kinywa chake, mbuni akatoka.

Mbuni alipotoka, alianguka chini puu, huku akihema kwa nguvu. Hakuelewa kwa nini rafiki yake alimtesa kiasi kile. Alishangaa kuona amekuwa mrefu. Akisimama anaona mbali kuliko ilivyokuwa mwanzo.

Mara, akagundua kuwa shingo yake imekuwa ndefu kwa sababu ya kujivuta. Mbuni alikasirika sana. Alimmwagia Mamba mchanga machoni. Akamwambia, "Sitaki urafiki na muuaji. Kumbe wewe si rafiki wa kweli. Ninaenda zangu. Tena nikikuta mayai yako mahali nitaya**fukua** na kuyavunja." Akaondoka mbio. Mamba alirudi zake mtoni. Tangu siku hiyo urafiki wao ukaishia pale.

## Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Mamba alikuwa rafiki wa nani?
2. Mamba alikuwa akiwinda nini kandokando ya mto?
3. Ngozi ya mamba hutumika kutengenezea vitu gani?
4. Mamba alikuwa akimchukua Mbuni hadi nyumbani kwake ili kumwandalia nini?
5. Nani alikuwa hajui kuwa mayai hulaliwa?
6. Mbuni alipoachiwa na Mamba, alianguka wapi?
7. Kwa nini binadamu walikuwa wakimwinda Mamba?
8. Nani alilia kwa uchungu akidhani kuwa angekufa?



KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 181 26/07/2021 16:26

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

9. Mbuni alipokasirika alimfanya nini Mamba?
10. Unafikiri ni mnyama gani mwingine aliyefanyiwa kitendo kama alichofanyiwa Mbuni? Kwa nini?
11. Taja mawazo makuu yaliyojitokeza katika kisa cha Mbuni na Mamba.

## Zoezi la pili: Msamiati

**Andika maana ya maneno yafuatayo, kisha tunga sentensi moja kwa kila neno.**

1. mamba
2. mbuni
3. chaka
4. okoa
5. angua
6. adui
7. sabahi
8. umiza
9. nasua
10. fukua

## Zoezi la 3: Methali

**Andika methali zenye maana tofauti kwa kila methali uliyopewa.**

1. Hakuna msiba usiokuwa na mwenziwe.
2. Mwendapole hajikwai.
3. Ngojangoja yaumiza matumbo.
4. Mchelea mwana kulia hulia mwenyewe.
5. Fimbo ya mnyonge ni umoja.
6. Kawaida ni kama sheria.
7. Damu ni nzito kuliko maji.
8. Maneno mengi hula vitendo.

## Zoezi la 4: Vitendawili

**Tegua vitendawili vifuatavyo:**

1. Huuawa na uzazi wake. __________
2. Bibi hupigwa virungu kila siku lakini hatoroki. __________
3. Mti wangu una matawi saba, manne mabichi, mawili makavu na moja lina kichaa. __________
4. Askari wangu akiniona hutikisa au kuficha mkia. __________

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

5. Wanangu watano wote wana kofia sawa. __________
6. Wanangu watatu, ukiona wanne chinja. __________
7. Hapotei hata akiwa gizani. __________
8. Nimefagia uwanja wangu miguu mirefu kaja kuuchafua. __________
9. Anajiingiza jela mwenyewe. __________
10. Kwetu hapakosi unga. __________

## Zoezi la 5: Mazoezi ya lugha

### A. Chagua jibu sahihi katika maswali yafuatayo:

(i) Mamba ____________ majini na nchi kavu.

(a) anaishi
(b) hajaishi
(c) ataishi
(d) aliishi

(ii) Mbuni ni ___________

(a) ndege mkubwa
(b) ndege kubwa
(c) samaki mkubwa
(d) dege mkubwa

(iii) Mamba anatembea _________ miguu.

(a) na
(b) kwa
(c) ni
(d) ya

(iv) Mbuni aliruka kwa kutumia _________ yake.

(a) mbawa
(b) bawa
(c) mabawa
(d) vibawa

(v) Mbuni _________ mayai yake baada ya miezi mitatu.

(a) kuangua
(b) hutungua
(c) huvunja
(d) huangua

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(vi) Mbuni alipomtembelea Mamba alimkuta ___________mwa mto.

(a) ndani
(b) pembeni
(c) katikati
(d) juu

(vii) __________ sauti ya Mamba ilikuwa si ya kawaida?

(a) Kwa sababu
(b) Kwa hivyo
(c) Kwa nini
(d) Kwa hiyo

(viii) Shingo ya mbuni ni ndefu _________.

(a) sana
(b) vizuri
(c) kuliko
(d) pembeni

(ix) Mamba aliogopa ________ gani?

(a) chiumbe
(b) kiumbe
(c) maumbe
(d) miumbe

(x) Mbuni anakula chakula kwa:

(a) kudonoa
(b) kufukua
(c) kutafuna
(d) kuigiza

**B. Chagua neno moja kutoka kila safu ili kuunda sentensi sahihi.**

| A | B | C |
|---|---|---|
| Mbuni | anaishi | mtoni |
| Mamba | huwika | porini |
| Maji | anaatamia | alfajiri |
| Jogoo | yamefurika | mayai |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**C. Kanusha sentensi zifuatazo:**

**Mfano:** *Tumelima shamba kubwa la mahindi.*
*Hatujalima shamba kubwa la mahindi.*

(i) Juma alisoma kitabu cha hadithi ya sungura.
(ii) Mimi nitaenda tena mtoni kuteka maji.
(iii) Wanafunzi walicheza mpira na kufunga magoli mengi.
(iv) Leo kuna upepo mkali sana.
(v) Wazazi wa Agata walilima mashamba makubwa.
(vi) Mtoto amevaa nguo zinazong'aa.
(vii) Mfuniko wa pipa lililonunuliwa jana, umetoboka.
(viii) Dada yangu anajua kuoka mikate mizuri sana.
(ix) Wananchi wamejiwekea utaratibu wa kufyeka nyasi pembezoni mwa barabara.
(x) Mariamu ameosha vyombo vyote vilivyotumika wakati wa sherehe.

**D. Andika maana mbili kwa kila neno, kisha tunga sentensi moja kwa kila maana ya neno.**

**Mfano:** *kaa - mnyama mdogo wa majini*
*Siku ya harusi ya dada tulikula wali na* ***kaa****.*
*kaa - kitendo cha kuketi*
*Wageni wali****kaa*** *kwenye mkeka wakati chakula kikiandaliwa.*

(i) poa
(ii) mto
(iii) mbuni
(iv) kibao
(v) angua
(vi) lia
(vii) kucha
(viii) hema
(ix) washa
(x) kuna

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**E. Oanisha sehemu A na Sehemu B ili kukamilisha maelezo ya sehemu A.**

| Na | Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|---|
| (i) | Hutokea ghafla na kusambaa kama moshi _____ | unyevu |
| (ii) | Hufanya watu watetemeke na kujikunyata _____ | mvua |
| (iii) | Ukosefu wa mvua kwa muda mrefu _____ | baridi |
| (iv) | Upepo unaovuma kwa kishindo na kuleta madhara_____ | ukungu |
| (v) | Hali ya kuwa na umajimaji_____ | mafuriko |
| (vi) | Sauti kubwa na nzito inayotokana na kitu kama vile radi, gari, eropleni au mnyama_____ | ukame |
| (vii) | Hustawisha mazao na mimea_____ | kimbunga |
| (viii) | Mvuke unaoganda na kuwa mzito uonekanao angani _____ | joto |
| (ix) | Husababisha watu watokwe na jasho _____ | ngurumo |
| (x) | Hali ya mito, vijito na maziwa kujaa maji kupitiliza _____ | wingu |

## Zoezi la 6: Utungaji

**Andika kisa chochote kuhusu wanyama chenye maneno yasiyozidi mia moja (100).**


FOR ONLINE USE ONLY





KISWAHILI_DARASA LA 6_KITABU CHA MWANAFUNZI_FINAL.indd 186 26/07/2021 16:26


## Vitabu vingine vya Darasa la Sita
## Taasisi ya Elimu Tanzania


### Darasa la Sita









ISBN 978-9987-09-049-5

*Mali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hakiuzwi*